# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Sita – Tarehe 14 Septemba, 2016**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 71

**Kiinua Mgongo kwa Wazee**

**MHE. KISWAGA B. DESTERY** aliuliza:-

Wazee wa nchi hii walilitumikia Taifa na kuchangia Pato la Taifa:-

Je, ni lini Serikali itaanza kuwapatia kiinua mgongo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kiswaga Boniventura Destery, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Namba 6 ya mwaka 2004, kiinua mgongo ni malipo yanayolipwa na mwajiri kama mkono wa ahsante kwa mfanyakazi wake baada ya kumaliza mkataba wa kazi. Hata hivyo, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama

cha Mapinduzi ya mwaka 2015 na kuwalinda wazee wa nchi hii na umasikini wa kipato, Serikali inaandaa mpango wa pensheni kwa wazee nchini. Aidha, hadi sasa Serikali imetekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuainisha idadi ya wazee wote nchini;

(ii) Kuainisha viwango vya pensheni;

(iii) Kuandaa utaratibu utakaotumika kulipa pensheni;

(iv) Kuandaa taratibu za kiutawala za kusimamia utoaji wa pensheni kwa wazee; na

(v) Kushirikisha wadau mbalimbali katika kuandaa Mpango wa Pensheni kwa Wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itakapojiridhisha kuwa taratibu zote ziko sawa itatoa taarifa ya kuanza kwa malipo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na kadri ambavyo imeanza kushughulikia jambo hili hasa kwa kuamini kwamba katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi tulifanya ahadi na wananchi, lakini ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa wazee hawa wengi ni wakulima ambao wakati wote Serikali inapokuwa na hali mbaya ya chakula huzuia mazao yao kuuzwa mahali popote ili kukidhi mahitaji ya nchi, kwa hiyo, hawa wazee wamechangia sana katika Taifa hili.

Je, ni lini sasa Serikali pamoja na hatua nyingine ambazo imezichukua itakamilisha mpango huu ili wazee hawa waweze kulipwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa sisi sote tuliopo humu ni wazee watarajiwa, je, Serikali inaweza kutuambia hapa itaanza kwa kutoa kiasi gani kila mwenzi na kwa kila mzee? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la kwanza la mpango huu utakamilika lini, kwenye majibu yangu ya msingi nimesema kwamba hatua ambayo tumefikia hivi sasa ni zile za kuainisha idadi ya wazee wote nchini, kuainisha

viwango vya pensheni, lakini baadaye tutakapojiridhisha taratibu zote hizi zimekamilika, Serikali itatoa taarifa ni lini sasa tutaanza kufanya kazi hii ya malipo. Nimuondoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa wazee katika nchi hii hasa kwa mchango wao mkubwa walioutoa katika ustawi wa Taifa letu. Kwa hiyo, pindi taratibu hizi zitakapokamilika basi tutakuwa tayari kutoa taarifa na kusema ni lini mchakato huu wa kuwalipa pensheni wazee utaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili la nyongeza ameuliza ni kiasi gani kitakacholipwa. Tumefanya tafiti mbalimbali katika nchi tofauti na tumejiridhisha na mapendekezo yaliyopo sasa katika kiwango cha kwanza cha kuanzia itakuwa ni shilingi 20,000 kwa kila mzee. Utaratibu uliowekwa ni kuanza na wazee wa kuanzia umri wa miaka 70 ambao wako takribani 1,570,000 na baadaye tutaendelea kuona jinsi ya kuongeza umri chini ya hapo kadri uwezo utakavyokuwa unaruhusu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni muda mrefu Wabunge tumekuwa tukiishauri Serikali kuwalipa wazee kiinua mgongo. Mimi tangu nimeanza Ubunge zaidi ya miaka 20 nadai hivyo na leo Serikali inasema wapo katika mipango, sasa mipango hii ni lini itaisha? Sisi tunaomba kama inawezekana katika bajeti hii wazee waanze kulipwa kiinua mgongo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia majibu yale yale tu ya kwamba suala la kuwalipa pensheni wazee kama ambavyo imesemwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM Serikali itatekeleza, kilichobaki hivi sasa ni kwamba mpango huu mwanzoni ulikuwa umeshakamilika katika awamu lakini baadaye likaingizwa pia suala la watu wenye ulemavu, kwa hiyo, ikabidi tuanze kuangalia na mazingira mengine ya watu wenye ulemavu. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu hizi ziko ukingoni kukamilika na Serikali itaanza kuwalipa pensheni wazee. Kwa sababu katika utaratibu wa jambo lenyewe jinsi lilivyo upo muundo wake ambao ni kuanzisha kamati mbalimbali kuanzia chini mpaka Taifa ambazo nazo pia zimeanza kufanyiwa kazi na zitakamilika muda siyo mrefu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mtuamini kwamba siyo maneno tu, lakini mikakati hii imeshakamilika Serikali itawalipa pensheni wazee kama ambavyo nimesema hapo awali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika jibu la nyongeza imeelezwa kwamba ulipaji wa pensheni kwa wazee hawa utaanza kwa wazee ambao wana miaka kuanzia 70 wakati ambapo watu wanastaafu wengine wakiwa na miaka 55, wengine miaka 60 na umri wa kuishi Tanzania unajulikana. Je, Serikali hii ya CCM haioni kwamba inasubiri mpaka wazee wengi wafe ndiyo waweke mpango wa kuwalipa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, ukiwa na hoja ya msingi uliza swali, huna haja ya kuzungumza mambo ya vitu ambavyo havipo, wala havina nini…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Hapana, uliza swali kuhusu uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi, usiingize mambo ambayo hayahusiani.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti)*.

**MWENYEKITI:** Ndiyo *ruling* yangu Mheshimiwa Mnyika na nikisema mimi wewe unakaa kimya. Inawezekana siku nyingi haupo Bungeni labda hujui taratibu za Kibunge. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuanzia ulipaji wa pensheni kwa wazee ukienda nchi zote duniani huwa wanakwenda kwa *categories* na huwa wanaangalia hali ya uchumi wa nchi katika wakati husika. Sisi kwetu tumeona tuanzie katika umri wa miaka 70 kwa kutambua kwamba bado wazee ambao wanastaafu katika kazi wanaanzia umri wa miaka 60. Ukienda kwa mfano Uganda wana kitu wanakiita *Senior Citizens' Grants* ambayo wenyewe wanalipa kuanzia miaka 70. Ukienda Nepal ambayo ndiyo nchi ya kwanza duniani ambayo imeboresha pensheni kwa wazee na wenyewe walianza kulipa kwa watu wenye umri wa miaka 70 kwanza baadaye walipoona hali inaruhusu wakashuka kwenye 65 na sasa hivi akina mama ambao ni wajane na wenyewe wameanza kulipwa pensheni hii katika umri wa miaka 55.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mnyika ondoa hofu kwamba hatua hii ya kwanza ni ya kuona kwa namna gani tunaweza tukafanya zoezi hili kwa watu hawa wenye umri wa miaka 70 na baadaye kwa kadri uwezo utakavyoruhusu tutaendelea kushuka ili kuwa-*cover* wazee wote, nikuondoe hofu tu Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 72

**Mpango wa Kuwawezesha Wanawake Kiuchumi**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Wanawake katika Mkoa wa Simiyu wamehamasika sana kujiunga kwenye vikundi ili kukusanya nguvu za kiuchumi kwa lengo la kujiendeleza kiuchumi zaidi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wanawake hawa mafunzo ya kimtaji ili waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi kwa ufanisi zaidi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiwawezesha kiuchumi wanawake kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ambao kila Halmashauri inatakiwa kutenga asilimia tano ya mapato yake ya ndani. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Mkoa wa Simiyu ulitoa mikopo kwa wanawake na vijana yenye thamani ya shilingi milioni 116.5 ambapo kati ya hizo wanawake walikopeshwa shilingi milioni 75.7 kwa vikundi vipatavyo 74. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Mkoa wa Simiyu umetenga shilingi milioni 978.08 kwa ajili ya vijana na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zote zimeelekezwa kulipa madeni ya fedha ambazo hazikupelekwa kwenye Mifuko ya Vijana na Wanawake kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Hazina iliweka kigezo kwa kila Halmashauri kuonesha fedha zilizotengwa kwa ajili ya vijana na wanawake kabla ya kupitisha bajeti yake na Halmashauri zote zimetenga fedha hizo jumla ya shilingi bilioni 56.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafunzo, Halmashauri kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii zimeendelea kutoa elimu ya masuala ya biashara na ujasiriamali kwa vikundi vya wanawake na vijana kabla na baada ya kupata

mikopo ili kuhakikisha kwamba mikopo inayotolewa inatumika na kusimamiwa ipasavyo. Katika utekelezaji wa jukumu hili, Serikali inashirikiana na sekta binafsi zikiwemo asasi za kiraia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa wanawake wa Mkoa wa Simiyu ni wajasiriamali wazuri sana. Je, ni lini Serikali itaanzisha Benki ya Maendeleo ya Wanawake ili wanawake wa Mkoa wa Simiyu waweze kujikomboa na kujinufaisha na benki hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais ni kupeleka kila kijiji na kila mtaa shilingi milioni 50 ili kuwawezesha wanawake na vijana. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kusimamia pesa hizo na kuhakikisha kwamba zimewafikia walengwa, zisije zikaishia mikononi mwa watu wachache, wajanja kama mapesa ya JK? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumbukumbu ya Wabunge yote wakati Waziri wa Afya ambaye anahusika na mambo ya maendeleo ya jamii ambapo Benki hii ya Wanawake iko katika dhamana yake, nakumbuka katika bajeti ya mwaka huu alizungumza wazi kwamba suala la ufunguaji wa matawi ya benki hii utafanyika kwa kadri rasilimali fedha inavyopatikana. Imani yangu ni kwamba kauli ile ya Mheshimiwa Waziri itaendelea kusimamiwa na katika Ukanda ule wa Ziwa benki hii itafunguliwa lengo kubwa likiwa ni kufikisha huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la shilingi milioni 50, ni kweli, sisi tunafahamu kwamba katika mchakato wa bajeti ya mwaka huu zile fedha zilitengwa na naamini Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inahusika na kusimamia jambo hili inapanga utaratibu mzuri na ndiyo maana wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anapita maeneo mbalimbali alikuwa akitoa maelekezo kwamba watu waache kuunda vikundi vya kitapeli ambapo mwisho wa siku fedha zile zitakuja kupotea. Imani yetu ni kwamba katika kipindi tutashirikiana vizuri wananchi wote na Serikali ili tusifanye makosa yale yaliyojitokeza katika kipindi cha nyuma katika fedha zile za mamilioni ya JK, sasa tunasema hatutarudia tena utaratibu ule wa mwanzo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selasini ajiandae Mheshimiwa Murad Saddiq.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Ni ukweli usiopingika kwamba wanawake katika nchi hii ndiyo wanaolisha Taifa hili kwa sababu akina mama wengi wanajishughulisha na kilimo na biashara ndogo ndogo. Ni kweli pia kwamba katika baadhi ya Halmashauri akina mama wengi wananyanyasika sana na biashara zao kwa kutozwa kodi mbalimbali ambazo hazina tija.

Je, ni lini Serikali itatoa tamko kwa Halmashauri zote ikiwepo Halmashauri yangu ya Rombo waache kuwatoza akina mama zile kodi ambazo zinawaletea bugudha na hivyo kushindwa kuendesha biashara zao kwa ufanisi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika kufanya hili nadhani tunafanya rejea, hata Mheshimiwa Rais alipokuwa akizunguka sehemu mbalimbali alikuwa akisema kwamba akina mama hawa wasinyanyaswe.

Naomba niseme wazi kwamba kutokana na agizo hilo la Mheshimiwa Rais, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunaandaa marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa inayohusiana na mambo ya Kodi, Sura Namba 290 na hivi sasa ipo katika mchakato wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuondoa zile kero mbalimbali siyo za akina mama peke yake bali ni pamoja na walemavu na makundi mbalimbali. Katika mchakato huu tutakwenda kuhakikisha tunaondoa kero hii siyo kwa akina mama na vijana tu, lakini na *group* la walemavu lazima wawezeshwe na Halmashauri.

Hata hivyo, watakapowezeshwa kitafanyika nini ili mitaji yao iende vizuri, ndiyo hiyo sheria inakuja sasa hivi. Imani yangu ni kwamba Wabunge wote kwa pamoja sheria ile itakapokuja hapa tutashirikiana kuipitisha kwa sababu jambo hili lina maslahi mapana sana kwa wananchi wetu lakini kikubwa zaidi lina maslahi katika uchumi wa nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Murad Saddiq.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Na mimi nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wanawake wa Simiyu wamehamasika vizuri sana na wanafanana kabisa na wanawake wa Mvomero na wanawake wa Sumve.

Je, Waziri atatueleza ni lini sasa katika suala zima la maendeleo zile shilingi milioni 50 zitakwenda Sumve na Mvomero kwa sababu wanawake wale wameshajiunga kwenye vikundi na vikundi vile vimeshasajiliwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwambie wanawake wa Mvomero na wale Wasukuma wa kule hawawezi kufanana, hilo ni jambo la kwanza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naomba nimtoe shaka, najua Mheshimiwa Murad ni mpiganaji mkubwa sana, Serikali itahakikisha watu wa Mvomero, Bariadi, Sikonge na wa maeneo yote fedha zile zinapatikana na zinawafikia wananchi ili mradi wahakikishe wanajihusisha katika shughuli za ujasiriamali. Suala hili Serikali imelisikia ndiyo maana imeweka katika bajeti yake ya mwaka huu wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Na. 73

**Upandaji Miti**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA (K.n.y. MHE. ALBERT O. NTABALIBA)** aliuliza:-

Wilaya ya Buhigwe ni Wilaya ambayo upandaji miti haujafanyika vya kutosha.

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuweka bajeti juu ya zoezi hilo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwepo kwa changamoto kwa baadhi ya wilaya ikiwemo Wilaya ya Buhigwe Mkoani Kigoma kutokufanya vizuri katika zoezi la kupanda miti. Changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa mbegu, miche na aina ya miti inayofaa kupandwa kwa kila wilaya. Aidha, suala la ukame, upatikanaji wa maeneo na ardhi ya kupanda miti, usimamizi dhaifu wa viongozi na watendaji na mwitikio mdogo wa jamii navyo huchangia kukwamisha zoezi la upandaji miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaona umuhimu wa kutenga bajeti kwa ajili ya zoezi la kupanda miti na kwa kutambua hilo, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 imetenga shilingi bilioni mbili katika Mfuko wa Mazingira ambazo zitatumika kwa ajili ya zoezi la upandaji miti nchini. Aidha, tunahimiza Halmashauri zote nchini na taasisi za umma na binafsi kutenga fedha kwa ajili ya kupanda miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitumie fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kushiriki katika upandaji miti na utunzaji wa miti. Aidha, ni matumaini yangu ya kuwa Waheshimiwa Wabunge watakuwa mstari wa mbele katika kushiriki na kuhamasisha wananchi kupanda na kutunza miti ili kuifanya Tanzania iwe ya kijani.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini naomba niweze kuuliza maswali yangu mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa amekiri kwamba wananchi wako tayari kupanda miti na kuna tatizo la vitalu vya miti, je, Serikali itaweka lini bajeti na utaalam ili kusudi vitalu vya miti viweze kuoteshwa katika kila Wilaya hapa nchini ili wananchi waweze kupanda miti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, miti mingi ambayo imekuwa inapandwa asili yake inatoka nje ya nchi siyo miti ya asili, je, ni lini sasa Serikali itaweka mkazo ili kusudi miti ambayo itaoteshwa kwenye vitalu ili wananchi waipande iwe ni miti ya asili ambayo ni rafiki wa mazingira na rafiki wa maji? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, suala la vitalu na Serikali kutenga bajeti, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya swali la msingi ni kwamba tayari tumeanza kutenga bajeti. Kwa mwaka huu kwa kuanzia tumetenga shilingi

bilioni mbili na tunataka katika miaka ijayo ya fedha tuwe na wastani wa kutenga zaidi ya shilingi bilioni 20 kila mwaka ili kuweza kupanda miti inayostahili Kitaifa.

Vilevile tumesema kwamba Halmashauri zote zina jukumu pia la kutenga fedha kwa ajili ya shughuli hii na hivyo sasa katika mpango wa upandaji miti tuliouandaa wa mwaka 2016-2020 unabainisha haya na kwamba Halmashauri zote zitawajibika kuhakikisha tunakuwa na vitalu katika ngazi ya kata mpaka vijiji na kwenye taasisi kama shule ili wananchi waweze kupata miche na mbegu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili amesema kwamba miti mingi inayopandwa ni ya kutoka nje, suala hapa siyo miti kutoka nje bali tunapanda miti yenye faida na wananchi tunawasisitiza wapande miti yenye faida. Kwa hiyo, wataalam wetu wanaohusika na misitu pamoja na hawa wa mazingira wamefanya upembuzi wa kujua kila eneo linafaa kupandwa miti ya aina gani, linafaa kupelekewa miti ya aina gani ambayo inaweza kustawi lakini vilevile yenye faida kwa wananchi kwa mfano, miti ya matunda, mbao, dawa kikubwa tumewaelekeza wataalam wetu wapeleke miti yenye faida.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Na.74

**Serikali Kutwaa Maeneo bila Kushirikisha Wananchi**

**MHE. SUSAN L. KIWANGA** aliuliza:-

Serikali imetwaa maeneo ya vijiji katika Kata za Idete, Namwala, Mofu, Mbinga, Igima, Mchombe, Mngeta, Kalengakelu, Mlimba, Kamwene, Chita na Utengule kwa madai kwamba ni maeneo ya hifadhi bila kuwashirikisha wananchi, jambo ambalo limefanya wananchi kushindwa kuendeleza shughuli zao za kilimo na ufugaji na hivyo kuendelea kuwa maskini.

Je, Serikali itakuwa tayari kushirikisha wananchi ili kuweka mipaka kati ya maeneo ya kilimo na ufugaji na yale ya Hifadhi ya Taifa ili kuondoa mgogoro wa ardhi uliopo hivi sasa kwa wananchi kukosa maeneo ya kilimo na malisho ya mifugo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu haijawahi kutwaa na haina utaratibu wa kutwaa maeneo ya vijiji na kuyafanya kuwa maeneo ya hifadhi bila ya kuwashirikisha wananchi. Aidha, sehemu ya maeneo ya vijiji vilivyoko ndani ya kata 12 zilizotajwa yamo ndani ya eneo la Hifadhi ya Ramsar ya Bonde la Kilombero iliyotambulika na kuorodheshwa mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Ramsar la Bonde la Kilombero ni muendelezo wa hifadhi ulioanza na Pori Tengefu la Kilombero lililoanzishwa kwa Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori, Sura ya 302 ya mwaka 1952 kupitia Tangazo la Serikali Namba107. Pori hili lilirithiwa na Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Namba12 ya mwaka 1974 na kuboreshwa na Sheria Namba 459 ya mwaka 1977 baada ya taratibu zote za kisheria kukamilika ikiwemo ushirikishaji wananchi. Aidha, eneo hili ambalo ni chanzo kikubwa cha maji na lenye uwepo wa viumbe adimu duniani lina ukubwa wa kilometa za mraba 7,967.35 sawa na hekta 795,735 sifa ambazo zinalifanya kuwa eneo la tatu kwa ukubwa lenye umuhimu wa Kimataifa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi iliyopo baina ya wananchi na vijiji katika kata zilizotajwa ambavyo vilianzishwa baada ya kuanzishwa kwa Pori Tengefu la Kilombero imetokana na hatua mbalimbali za ukiukaji wa sheria, kanuni na taratibu. Aidha, katika kutatua migogoro hiyo, Serikali inaendelea kutekeleza yafuatayo:-

(a)Kupitia Mradi wa *KILORWEMP* unaotekelzwa chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii; kupitia upya mipaka, kuweka alama, kuchora ramani na kutunza kumbukumbu kwa njia za kawaida na kielektroniki.

(b)Kupitia mpango wa upimaji ardhi za vijiji vya Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi unaosimamiwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; kukamilisha upimaji na urasimishaji wa ardhi ambapo mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji itaandaliwa na wananchi na watamilikishwa ardhi kisheria.

(c)Kupitia Kamati Maalum ya Kitaifa iliyoundwa kushughulikia migogoro ya rdhi nchini; kufika katika maeneo ya Ramsar na Pori Tengefu la Kilombero na kutekeleza majukumu yake katika kutatua migogoro kwa kuwashirikisha wananchi kama ilivyo kwa utekelezaji wa hatua zingine nilizozitaja hapo juu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Mimi nilifuata utaratibu nimeuliza swali fupi sana, lakini ukiona majibu marefu ujue hapa kuna udanganyifu. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza hili swali tangu nikiwa Mbunge wa Viti Maalum na Ofisi ya Wanyamapori wakati huo alikuwa Ndugu Sarakikya alinijibu kwamba walienda kupima na nikaenda Ofisi ya Ardhi Kilombero wakasema wananchi hawajashirikishwa. Baada ya kuwabana sana mkasema kwamba mnasubiri hela kutoka Ubelgiji na mmeshapata shilingi milioni 100 na sasa mnaaenda kushirikisha na mpaka kwenye Halmashauri yetu tunazo hizi taarifa, mnaenda mkashirikishe vijiji mkapime upya leo unaniletea majibu marefu. Nakuambia mradi wa ardhi hauendi kutatua migogoro unaenda kupima vipande vya ardhi ambavyo havina migogoro, Mheshimiwa Lukuvi huyu hapa. Sasa haya majibu yako mimi siyakubali, hiyo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa kuna barua ninayo hapa, Meneja wa Ramsar ametoa barua iko Kilombero anasema wataenda kutatua hiyo migogoro…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan nenda kwenye swali.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Sasa ni lini mtaenda kutatua ile migogoro na mmeruhusu wafugaji waende kule kwa wakulima, magomvi karibu yatatokea, ardhi mmeitwaa, mmeenda kufanya nini? Lini mtaenda kurekebisha ile mipaka? Ninachotaka ni safari ya kwenda Kilombero. Mimi nasemea Kilombero lakini kuna Wilaya tatu, Ulanga na Malinyi, kuna vijiji 126 mmechukua bila idhini yao. Nendeni mkafanye kazi, hilo ndilo swali langu, ndiyo, lini mtaenda Kilombero na barua mnayo? *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Susan. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunamjua Mheshimiwa Susan…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaomjua Mheshimiwa Susan ndiyo lugha yake, hatumshangai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo marefu ya Mheshimiwa Susan ni kweli kwamba tunayo migogoro mingi sana na Serikali tunajua

kwamba tunayo migogoro mingi. Iko migogoro inayoweza kutatuliwa na Wizara moja moja, lakini iko migogoro ambayo haiwezi kutatuliwa na Wizara moja moja. Juzi nimetoka Kilombero yale yanayonihusu mimi nimejaribu kuyatatua, lakini hayo mengine anayoyasema sisi Serikali tumeunda timu. Hivi sasa tumekutana mimi na mwenzangu Waziri wa Mifugo, Waziri wa Maliasili na TAMISEMI tumeunda timu ziko mtaani huko mikoani na huko Kilombero watafika na nimewaambia hata juzi kwamba haya anayoyasema hayo siyo yangu, kuna Madiwani wameniambia kama alivyoniambia Mheshimiwa Susan.

Kwa hiyo, nimewaambia hili si letu kwa sababu haiwezekani Lukuvi anayekwenda siku moja akatatua mgogoro. Kwa hiyo, tumeunda timu ya wataalam wa Wizara nne wanapitia kuangalia namna bora ya kutushauri sisi Mawaziri tuamue juu ya migogoro hiyo mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wanakumbuka wakati uliopita tuliwapa fomu fulani mkatupa ile migogoro iko, Mheshimiwa Susan ameandika kwenye kile kitabu. Kwa hiyo, kutokana na kile kitabu sasa tumeunda timu, nataka kukuhakikishia hata sisi kama Serikali tumejiwekea lengo katika miaka hii mitano lazima tuwe tumemaliza migogoro yote. Kwa hiyo, nataka tu kumueleza Mheshimiwa Susan kwamba migogoro ilikuwepo na itaendelea kuwepo lakini tumeamua kuikabili kisayansi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Jimbo la Mlimba na Jimbo la Kilolo ni majimbo yanayopakana. Kwa kuwa vijiji vingi ambavyo vinapakana na hifadhi huwa haviruhusiwi kufanya shughuli zozote za kibinadamu ndani ya hifadhi lakini tembo wamekuwa kero kwenye vijiji hivyo, kwa mfano, Kata ya Ruaha Mbuyuni, Mahenge na Nyanzo hivi ninavyozungumza uharibifu mkubwa wa mazao umefanyika. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kutoa tamko lolote leo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi muda wetu unakwenda sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la wanyama waharibifu kuvamia mashamba, ni kweli Serikali inazo taarifa kutoka katika vijiji mbalimbali vinavyopakana na hifadhi juu ya usumbufu wa wanyamapori wanaoharibu mazao ya wananchi. Siku za nyuma tulikuwa tukijikita zaidi katika kutumia vikosi vya Askari wa Wanyamapori kupambana na wanyama hao, lakini pale inapotokea wameshafanya uharibifu tulikuwa na ule utaratibu wa vifuta jasho.

Hata hivyo, Serikali imeshaona kwamba kutumia vikosi tu vya Askari wa Wanyamapori nguvu hiyo haitoshi lakini pia kusubiri mpaka wanyama wawe wameshafanya uharibifu ndipo tulipe vifuta jasho nao pia siyo mkakati mzuri kwa sababu siyo endelevu wakati mwingine gharama zinakuwa kubwa kuliko bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, kuanzia sasa Serikali imejipanga upya kubadilisha ulinzi ule wa kutegemea tu Askari wa Wanyamapori na kwenda kwenye ulinzi shirikishi au kufanya uhifadhi shirikishi. Vijiji vyote vinavyopakana na hifadhi kutapatikana askari ambao watawezeshwa kwa kupewa elimu na silaha kwa utaratibu ambao utaonekana unafaa ili ulinzi sasa ufanyike kwa njia ambayo ni pana zaidi ili kuweza kuzuia zaidi kuliko kusubiri kutibu baada ya kutoa vifuta jasho.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu hilo linawajibia Wabunge wote wanaovamiwa na wanyama, tunaendelea na Wizara ya Uvuvi.

Na. 75

**Mgogoro wa Kiwanda cha Igombola na Wananchi**

**MHE. JORAM I. HONGOLI** aliuliza:-

Uchumi wa wananchi wa Jimbo la Lupembe na Tarafa ya Lupembe unategemea biashara ya chai lakini kwa muda mrefu sasa wananchi wanataabika kupata soko la chai yao kwa sababu ya kufungwa kwa Kiwanda cha Chai cha Igombola - Lupembe mwaka 2009; na kwa kuwa kiwanda hicho kilikuwa cha wananchi lakini baadaye Serikali ikampata mwekezaji baada ya wananchi kushindwa kukiendesha lakini ukatokea mgogoro kati ya mwekezaji na wananchi ambao umesababisha hasara kubwa kwa wananchi, mwekazaji na Serikali pia.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua mgogoro huo ili Serikali iweze kunufaika na kiwanda hicho kupitia tozo ya kodi, ajira na kadhalika na wananchi waweze kuuza chai yao kwenye kiwanda hicho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji wa Kampuni ya *Dhow Mercantile East Africa Limited* alishinda kesi dhidi ya Muungano wa Vyama vya Ushirika

Lupembe (MUVYULU) iliyoamuliwa ilipe fidia inayokadiriwa kuwa shilingi bilioni 28 pamoja na gharama za kuendesha kesi hiyo. Hata hivyo, MUVYULU walikata rufaa na hivyo kesi hiyo bado ipo mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inasubiri maamuzi ya kesi iliyoko mahakamani kupitia uongozi wa Mkoa, Serikali iliomba *Mufindi Tea and Coffee Limited* kuangalia uwezekano wa kujenga Kiwanda cha Chai katika Tarafa ya Lupembe ili kuwezesha wakulima wa chai wa eneo hilo kuuza majani ya chai. *Mufindi Tea and Coffee Limited* ilitekeleza ombi hilo na kuunda Kampuni iitwayo *Ikanga Company Limited* na kujenga kiwanda katika eneo hilo na kilianza kufanyakazi mwezi Agosti, 2013 na kuzinduliwa rasmi mwezi Novemba 2013 na Rais Mstaafu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Kupitia kiwanda hicho sasa, wakulima wa Lupembe wanauza chai katika kiwanda hicho na kutoa ajira katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya Ikanga imeingia makubaliano na wakulima wa Lupembe kwa kuwapatia pembejeo na huduma za ugani ili kuweza kuzalisha chai yenye ubora mfumo ambao Serikali imekuwa ikiusisitiza katika kuendeleza uzalishaji wa mazo ya kilimo. Mwaka 2016 kampuni ya *Dhow Mercantile East Africa Limited* ilifanya ukarabati katika Kiwanda cha Lupembe ili kiweze kufanya kazi tena.

Hata hivyo, Serikali kupitia Bodi ya Chai imefanya ukaguzi na kugundua kasoro kuhusu hali ya kiwanda hivyo ilitoa leseni ya muda wa majaribio wa miezi mitatu kwa mwekezaji huyo ili kumpa muda wa kurekebisha kasoro zilizodhihirika. Baada ya mwekezaji kumaliza muda wa majaribio Bodi imemuongezea muda wa leseni kwa mwaka mmoja baada ya kujiridhisha na utendaji wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joram.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, nitoe shukrani kwa Serikali kwa jitihada ambazo imeendelea kuzichukua kwa ajili ya kunusuru uchumi wa Lupembe. Kwa namna ya pekee, nimpongeze Waziri wa kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kufanya ziara Lupembe na ni Waziri pekee aliyekuja Lupembe kwenye Jimbo langu kwa kutembelea hivi viwanda vyote viwili. Pamoja na shukrani hizo, nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mgogoro huu umedumu kwa muda mrefu sana na umekuwa ukienda mahakamani bila mafanikio au suluhu ya kudumu. Ni kwa nini sasa Serikali isichukue hatua ya kuwakutanisha wakulima pamoja na mwekezaji ili kuweza kupata suluhu ya kudumu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada anazofanya kurekebisha mgogoro ulioko pale Lupembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa mzozo ule wa Lupembe nadhani unakaribia mwisho kwa maana kwamba mwekezaji yule sasa yuko tayari kulegeza masharti aliyokuwa ameyaweka kwa kile chama cha MUVYULU na tumekwishazungumza naye. Kwa hiyo, nitoe wito tu pia kwa MUVYULU na wao kutong'ang'ania mambo ambayo mahakama imeamua siyo kwa kuwapa wao ushindi. Kwa hivyo, wakikubali kwamba watoe na kupokea *(give and take)* hili jambo litapata muafaka mara moja kwa sababu kimsingi wananchi hawana nia na huo mgogoro isipokuwa ni mmiliki na wale MUVYULU ndiyo wanaendesha mvutano na hivyo kuwafanya wananchi wapate hasara ya kutokuwa na viwanda viwili vinavyofanya kazi kwa mara moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na tatizo la soko la chai kuna tatizo kubwa sasa linaendelea katika Mkoa wangu wa Manyara kuhusu soko la mbaazi. Wafanyabiashara wamekataa kununua mbaazi kabisa katika Wilaya ya Babati na katika Wilaya zote za Mkoa wa Manyara na wakulima wamebaki na mbaazi zao kwa sababu India mwaka huu ambao walikuwa wanunuzi wakubwa wao wamelima, Uganda wamelima na Kenya wamelima.

Naomba nipate kauli ya Serikali juu ya wakulima hao wa mbaazi katika Mkoa wa Manyara ambao wameshindwa kuuza mbaazi zao kwa sababu wafanyabiashara wamegoma kabisa kununua mbaazi hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba bei ya mbaazi imetetereka katika miezi ya hivi karibuni na si jimboni kwake tu lakini Tanzania nzima. Soko la mbaazi limetikisika siyo nchini kwetu lakini ni duniani kote, wanunuzi wakubwa ambao wamekuwa wakinunua mbaazi yetu katika siku za hivi karibuni hawajaendelea na utaratibu ule wa kununua kwa bei ile kwa hiyo imepelekea mtikisiko utokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalifahamu hili, inajaribu kulifanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuangalia

uwezekano wa kupata wanunuzi mbadala. Nikubali tu kwamba ni kweli kabisa mbaazi imeshuka bei kwa baadhi ya maeneo kama Lindi na Mtwara imeshuka mpaka hata kufikia shilingi 500 kwa kilo ambayo ni tofauti kabisa na ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala hili tunalifahamu na tunalifanyia kazi na nimuahidi tu kwamba pale Serikali itakapopata suluhu tutamtaarifu kwa niaba ya wananchi wake wa Babati.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani.

Na. 76

**Utaratibu wa Kuimarisha Ulinzi Bungeni**

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH** aliuliza:-

Nchi inakuwa na amani pale ambapo kuna ulinzi imara.

Je, ni utaratibu upi mzuri wa kuimarisha ulinzi Bungeni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina utaratibu za kulinda maeneo yote tete kwa ustawi wa jamiii husika ikiwa ni pamoja na Bunge letu Tukufu. Kuna ulinzi wa kutumia vifaa vya kisasa na vinginevyo ambavyo ni *automated,* ulinzi unaoonekana na ule usioonekana ambao hufanywa na askari na ule unaofanywa na wanyama kama mbwa. Yote haya hufanyika kwa pamoja na tunakuwa na ulinzi imara katika maeneo yetu kwani huwezi kutegemea aina moja tu ya ulinzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Catherine.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi…

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Catherine, Mheshimiwa Rashid.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 145(a) na (b), yeyote ambaye anaingia katika maeneo ya Bunge au ukumbini ni lazima akaguliwe. Kwa utaratibu huo huo, magari ya Mawaziri na ya Wabunge wakati mwingine hukaguliwa kwa kutumia mbwa. Unapotumia mbwa kukagua magari wakati mwingine hudondosha mate na yale mate ni najisi tunaita *muhalladha* na najisi ile haiondoki mpaka uoshe mara saba na mara moja uhakikishe unatia mchanga. Je, hakuna utaratibu mwingine mzuri wa ku-*check* magari haya hasa kwa wale waislamu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Bunge lililopita tulishuhudia Mbunge mwenzetu akivamiwa katika maeneo anayoishi na kuharibiwa gari lake. Je, Bunge lina utaratibu gani kuhakikisha kwamba Wabunge hawa wanapata ulinzi au usalama wao unalindwaje kwenye maeneo yao wakiwa katika Bunge hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rashid Abdallah kwa *observation* yake ya msingi kabisa ambayo ni ya kiimani. Kwa kuwa ameuliza hakuna utaratibu mwingine na sisi kama Serikali pamoja na Bunge tuseme tumepokea ushauri ili tuli-*digest* jambo hilo huku tukiangalia maslahi mapana kwani imani inatuhusu na ulinzi unatuhusu. Kwa hiyo, ni jambo ambalo sote tutaliangalia tufikie muafaka mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili kuhusu Mbunge kuvamiwa, taarifa zake tunazo na tunachofanya ni kuimarisha ulinzi katika mazingira ya Wabunge wetu ili kuhakikisha kwamba wako katika maeneo salama. Niwahakikishie tu Wabunge kwamba wako mikono salama na kwa kuwa mnafanya kazi vizuri na sisi tunahakikisha kwamba wanakuwa salama. Niwatangazie tu Watanzania kwamba Wabunge hawa wanachapa kazi na jana wamechapa kazi mpaka saa sita usiku, wameunganisha kikao hiki. Kwa hiyo, wanapokutana nao huko uraiani watambue kwamba Wabunge hawa ni wachapakazi. Niwaambie vijana wangu kwamba hata wanapokuwa barabarani hawa Wabunge wakiona wako *speed* wawaambieni tu tunawahitaji lakini watambue ni kutokana na uchapakazi wao wanawahi mikutano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Catherine.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika suala zima la ulinzi tunategemea sana askari wetu, lakini tumekuwa tukishuhudia askari wetu

wakipoteza maisha wakiwa kazini wakati mwingine kwa kupambana na majambazi au wakipata ajali kwenye misafara mbalimbali. Nataka kufahamu Serikali ina utaratibu gani wa kuhudumia familia za askari hawa wanaopoteza maisha wakiwa kazini kama kusomesha watoto na huduma na huduma nyingine muhimu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Catherine kwa kulileta jambo hilo. Ni kweli kumekuwepo na matatizo hayo na sisi kama Wizara niliwaelekeza wataalam wangu kuangalia maeneo ambayo yanahusu sheria na yale yanayohusu sehemu ya bima kwa ajili ya askari wetu ili kuweza kusaidia askari kwanza akiwa bado yuko kazini, pale anapopata ajali kazini kuweza kuhudumiwa katika maumivu anayoyapata. Nilipozunguka nilipata taarifa kwamba kuna askari wanaumia kazini wanaambiwa bima haiingii kwenye baadhi ya vipimo ama katika baadhi ya dawa wanazotaka.

Kwa hiyo, hili la kuzihudumia familia wanapokuwa wamepata ajali tunaliangalia kwa mapana kisheria ili familia hizo zisiyumbe baada ya kuwa askari wetu amepata ajali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwijage, jiandae Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kabla sijauliza swali langu, naomba kuwashukuru wale wote ambao wanatoa misaada kwa Wilaya yangu ya Bukoba Mjini na naomba Watanzania wote na wasio Watanzania waangalie kwa jicho la huruma Bukoba Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kumuuuliza Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa Wizara yake inalinda raia na mali zao, hivi sasa Wilaya ya Bukoba Mjini watu wote wanalala nje na matatizo wanayoyapata ni kuibiwa mali zao na askari wanakwenda na kukamata wale watu ambao wanawasaidia wale wahanga. Je, Wizara yake imejipangaje kwenda kukabiliana na janga hili Bukuba Mjini kwa kuwalinda raia? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Nkamia anasema yeye basi. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Majibu.

**MWENYEKITI:** Aah *sorry*.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa jambo alilolileta ambalo liko muda huu. Niseme tu tangu tukio limetokea Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kushirikiana na Kamati za Ulinzi na Usalama Mkoa na Wilaya wameimarisha ulinzi katika maeneo husika. Kwa kuwa watu ni wengi inatokea katika kutafuta namna ya kujiridhisha kujua yupi anayeenda kwa ajili ya kutoa huduma na yupi anayeenda kwa ajili ya kukwapua ama kuchukua vile ambavyo vimezagaazagaa, kwa hiyo, ndiyo maana utaona kuna mwingiliano wa aina hiyo, lakini nia ya Wizara pamoja na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ni kuhakikisha kwamba watu hawa ambao wamepata matatizo wao pamoja na mali zao wanakuwa katika hali ya usalama.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Nkamia amesema yeye basi sasa tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 77

**Kuhamisha Mazoezi ya Kijeshi Chuo cha Polisi Moshi kwenye Maeneo ya Makazi**

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL** aliuliza:-

Mafunzo na mazoezi ya kijeshi yanayofanywa na Chuo cha Polisi *(CCP)* katika eneo la Kata ya Donyomorwa katika Wilaya ya Siha yamesababisha maafa makubwa kwa wananchi ikiwa ni pamoja na wananchi kuuawa kwa risasi na mabomu yanayotumika katika mazoezi hayo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamisha mafunzo hayo kutoka kwenye maeneo ya makazi ili kuepusha maafa yanayowapata wananchi wa maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina mpango wa kuhamisha mafunzo ya kijeshi katika eneo la Donyomorwa. Awali mafunzo hayo yalikuwa yakifanyika katika eneo la Kilelepori ambalo lilivamiwa na wananchi kwa kujenga nyumba na kufanya shughuli za kilimo ambapo Serikali iliamua kuhamisha mafunzo ya kijeshi katika eneo hili nililolitaja sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuepusha madhara yanayoweza kuwapata wananchi, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa jamii ya Kimasai kuacha kuchunga mifugo katika eneo hilo, kukata kuni na kuokota kitu chochote wasichokijua katika eneo hilo. Aidha, kabla ya Polisi kuanza mazoezi ya kijeshi huchukua tahadhari kama kutoa taarifa kwa Vijiji, Wilaya na Mkoa ikiwa ni pamoja na kuweka alama za tahadhari kuzunguka eneo lote kwa kuweka bendera nyekundu na kuwaweka askari katika vipenyo vya kuingia katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mollel.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ieleweke kuwa wananchi wa Siha siyo kwamba wanachukia polisi kuwepo katika eneo hilo lakini kilichoonekana ni kwamba watu wameongezeka sana katika eneo hili na ushahidi upo kwamba wameshakufa watoto wanne na tarehe 18/08/2016 kuna mtoto ambaye risasi ilimfuata nyumbani na mpaka sasa ana ulemavu. Maswali yangu mawili ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali isione ni busara sasa na ni wakati muafaka ikafuata ushauri wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Siha ya kwamba mazoezi ya polisi yapelekwe katika eneo la heka 500 ndani ya *NARCO* lakini hilo eneo likagawanywa katika sehemu tatu? Sehemu ya kwanza ni kutoa eneo ambalo litasaidia kupunguza ukata wa ardhi kwa wananchi wa Siha hasa walioko upande wa milimani, sehemu ya pili ikatolewa kwa ajili ya kufanya utalii wa kimila. Kama mnavyokumbuka mwaka huu Waziri wa Utamadumi alikuja pale na alifanya tukio kubwa ambalo linafanyika *East Africa* yote kwa ajili ya utalii. Kwa hiyo, Wizara ya Utamaduni na Idara ya Mambo ya Kale ikakabidhiwa chini ya Halmashauri eneo lingine kwa ajili ya kufanya utalii wa kimila. Eneo linalobaki tukajenga Chuo Kikuu cha Polisi badala ya kufanyia mazoezi yanayowaathiri wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Huwa sichanganyikiwi mkiongea sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, wananchi walioumia na huyu mtoto aliyepata ulemavu Serikali iko tayari kutoa fidia lakini vilevile Waziri kutembelea kuwaona waathirika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo alilopendekeza ametaja kwamba ni eneo la *NARCO* na *NARCO* iko chini ya Wizara nyingine na Wizara husika wana mpango wa matumizi wa eneo hilo. Ninachotambua ni kwamba ni kweli Wilaya ya Siha pamoja na Mkoa mzima wa Kilimanjaro una matatizo makubwa ya ardhi. Mkoa pamoja na Wilaya kwa kushirikisha Wizara ya Ardhi mara kwa mara wamekuwa wakiangalia mpango bora wa matumizi ya ardhi na sisi kama Wizara ya Mambo ya Ndani ni sehemu ya Serikali katika kuhakikisha wananchi wanapata eneo. Hata hivyo, kwa sasa yale niliyoyasema kwenye jibu la msingi yanasimama kwa maana tunatarajia kupima eneo lile ambalo linatumika kwa ajili ya mafunzo, kuweka alama na wananchi hawa waweze kutafutiwa maeneo mbadala ambapo mazungumzo yameendelea katika maeneo tofauti na Waziri wa Ardhi alishafika kule kuweza kuangalia njia bora ya kuwapatia vijana maeneo ya ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili ambalo amelisemea la kijana aliyeumia, kwa niaba ya Wizara na Serikali nitoe pole na tumepokea hayo ambayo ameyasema kama mapendekezo. Tutaongea na wataalam tuone ni kitu gani wamekuwa wakifanya punde yanapotokea mambo ya aina hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nkamia, jiandae Mheshimiwa Msabaha.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa suala la usalama ni jambo la msingi sana kwa raia wa Tanzania, kumekuwa na matukio mengi sana ya watu kupigwa na wengine kuuawa katika mpaka wa Kiteto na Chemba. Polisi wa eneo hili hasa wale wa Wilaya ya Chemba walioko Mrijo wanashindwa kufuatilia matukio haya kutokana na ukosefu wa vifaa ikiwemo magari, wengi wanaazima pikipiki na wakati mwingine baiskeli. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba vifaa vinapatikana katika maeneo ambayo kuna matatizo kama haya ili kunusuru wananchi na mali zao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Nkamia kwa kulisema jambo hili na niwahakikishie tu wananchi wa Chemba kwamba Mheshimiwa Nkamia amekuwa akifuatilia sana suala hili. Ameshakuja mara kadhaa ofisini na mimi nimemuahidi kwamba tutakapopata magari kwa ajili ya Wilaya mpya na Wilaya Chemba tutaipa kipaumbele zikiwepo na Wilaya nyingine kama Mkalama ambapo Mheshimiwa Allan Kiula naye amekuwa akisumbua mara kwa mara. *(Makofi)*

Kwa hiyo, napenda kumwambia Mheshimiwa Nkamia suala la magari pamoja na nyumba za askari katika Wilaya yake mpya tutalipa kipaumbele kwa kutambua mazingira tete ya eneo hilo ambapo pana changamoto za kugombania matumizi ya ardhi ambayo yanahitaji sana askari kuwepo katika maeneo hayo. Nitoe rai kwa wananchi wa maeneo husika watoe ushirikiano kwa Jeshi la Polisi punde mtu mmoja anapokuwa amekiuka sheria katika maeneo husika ili aweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Na mimi naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa zama hizi tumeona askari wakifanya mazoezi katika barabara wakiwa na silaha za moto na kwa mujibu wa sheria vikosi vyote vya ulinzi na usalama wana maeneo yao maalum ya kufanyia mazoezi. Je, Serikali haioni kwamba wanawapa maadui nafasi kuona udhaifu wa askari wetu na kuingiza maadui kupambana na vyombo vya ulinzi na usalama? Ni kwa nini vyombo hivi visibaki sehemu zao za kufanyia mazoezi huko huko vilikopangiwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu, mwambie Jeshi la Polisi halina udhaifu. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza vikosi vya ulinzi na usalama kufanya mazoezi ni sehemu ya maisha yao…

**MBUNGE FULANI:** Barabarani?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Na kila siku kwao ni mazoezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili alilosema kwamba kufanya mazoezi barabarani wanawafanya maadui wajue udhaifu wao, nimwambie tu mazoezi yale wanayofanyia barabarani ni ya viuongo na ni sehemu tu ndogo kati ya yale mazoezi makubwa wanayofanya ya kukabiliana na wahalifu. Na mimi niseme tu kwamba kwa mwananchi yeyote ambaye havunji sheria hana haja ya kushtuka anapoona askari wanafanya mazoezi. Wanafanya mazoezi hayo kwa ajili ya wahalifu, kwa hiyo, kama siyo mhalifu huna haja ya kuwa na mashaka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa barabarani ndiyo *theater of operation.* Waheshimiwa Wabunge na tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini. *(Kicheko)*

Na. 78

**Utafiti wa Mafuta na Gesi – Mafia**

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA (K.n.y. MHE. MBARAKA K. DAU)** aliuliza:-

Tafiti nyingi za mafuta na gesi zimefanywa na kampuni mbalimbali Kisiwani Mafia.

Je, ni nini matokeo ya tafiti hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni za *BP* na *Maurel Et Prome* kwa nyakati tofauti zilifanya tafiti katika eneo la Kisiwa cha Mafia kukusanya takwimu za mitetemo kwa eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 380 na 3D, lakini pia na katika Mkuza kwa kilometa 205 za 2D kuchimba visima viwili. Kati ya mwaka 1952 na 1956 kampuni ya *BP* ilichimba kisima cha Mafia -1 na kati ya mwaka 2006 hadi 2010 Kampuni ya *Maurel Et Prome* ilichimba kisima cha *Mafia Deep -1.* Baada ya tathmini ya takwimu hizo kufanyika matokeo yalionesha eneo hilo lina viashiria vya uwepo wa mafuta pamoja na gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa leseni ya kitalu hicho imekwisha muda wake hivyo eneo hilo liko wazi kwa kampuni yoyote kuomba na kuendelea kazi ya uchimbaji mafuta na gesi katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ulega.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa MWenyekiti, pamoja na majibu hayo mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jimbo langu la Mkuranga utafiti ulishafanyika na ikagundulika gesi asilia katika kijiji cha Kiparang'anda na kisima

kiko pale. Naomba sasa Serikali inieleze ina mpango gani wa kuhakikisha kisima kile cha gesi kilichopo pale Mkuranga kinatumika kwa manufaa ya Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha gesi hii inatumika ipasavyo katika kuzalisha umeme wa uhakika ili kikidhi haja ya viwanda na makazi yanayokuwa kwa kasi katika Jimbo hili la Mkuranga? Ahsante *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa makampuni ya utafiti yamefanya utafiti wa mafuta na gesi katika maeneo mbalimbali hasa katika maeneo ya Pwani ikiwepo eneo la Kiparang'anda. Nimhakikishie Mheshimiwa Ulega kwamba eneo la Kiparang'anda bado linafanyiwa utafiti na kazi inayofanyika sasa ni kuthibitisha kama kweli gesi na mafuta vipo. Mara baada ya kuthibitika hatua itakayofuata ni *appraisal* kuangalia kibiashara kama mafuta hayo bado yanaweza kuchimbika. Hatua itakayofuata baada ya hatua hiyo ni eneo la kufanya uendelezaji yaani *development* na baada ya hapo sasa hatua inayofuata ni uchimbijaji wa mafuta. Kwa hiyo, nimshukuru sana Mheshimiwa Ulega, kazi inaendelea kufanyika na hatua zikifikia mwisho Mheshimiwa Ulega na wananchi wake watafahamishwa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusiana na manufaa ya gesi kutumika kwa ajili ya umeme. Ni kweli kabisa kwani kwa sasa asilimia kubwa ya umeme tunaotumia hapa nchini ni kutokana na gesi asilia. Ni vyema niwahakikishie wananchi pamoja Waheshimiwa Wabunge kwamba sasa hivi megawati 743 za umeme zinatokana gesi na ni kiasi kikubwa sana cha gesi. Kwa hiyo, wananchi wa Mkuranga na maeneo mengine ya Pwani na siyo Pwani tu Mtwara pamoja na Lindi hata maeneo mengine ya Ukanda wa Kaskazini tutaendelea kutumia umeme wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Ulega vijiji vyake pamoja na vijiji vingine vya Rufiji, vijiji ambavyo ni 42 pamoja na 43 vya Mheshimiwa wa Rufiji pamoja na Kibiti vyote vitapata umeme kwa kutumia umeme wa gesi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo kwa swali linalofuata.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wandengereko wote duniani pamoja na Warufiji wa Kibiti na Rufiji, na

Wasukuma na Wamakonde wanaoishi kule, naomba swali langu namba 79 liweze kupatiwa majibu. *(Kicheko)*

Na. 79

**Kusuasua kwa Mradi wa REA - Rufiji**

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA** aliuliza:-

Mradi wa *REA* umekuwa ukisuasua katika maeneo ya vijiji vya Rufiji hususan Tarafa ya Mkongo, Kata za Mkongo, Ngorongo, Kipungila na Kata ya Mwaseni na Ngarambe.

Je, ni lini mradi huo utakamilika katika hatua inayofuata?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *REA* Awamu ya III ambao utafuata sasa na ambao unatekelezwa baada ya Mradi wa *REA* Awamu ya II katika Wilaya ya Rufiji unatekelezwa na Mkandarasi *MBH Power Ltd*. Wigo wa kazi katika Wilaya hii unahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 217.34; ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 04 yenye urefu wa kilometa 64.18; ufungaji wa transfoma 40 na kuwaunganishia umeme wateja wapatao 2,059.

Mradi umekamilika kwa asilimia 76 zikijumuisha ujenzi wa kilometa 201 za msongo wa kilovoti 33; ujenzi wa kilometa 23 za msongo wa kilovoti 0.4; kufunga transfoma 17 pamoja na kuwaunganishia umeme wateja 256. Mradi huu hadi kukamilika utagharimu shilingi bilioni 7.74.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata za Mkongo, Ngorongo, Kipungila, Mwaseni na Ngarambe ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 94 kutoka Ikwiriri hadi Mloka umekamilika kwa asilimia 90. Ujenzi wa njia ya usambazaji umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu kilomita 24.64 imekamilika kwa asilimia 45 na ufungaji wa transfoma 14 unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Septemba 2016. Kazi hizi zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2016. Kazi hii hadi kukamilika itagharimu shilingi bilioni 3.15.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli anasema kwamba msema kweli ndiyo mpenzi wa Mungu na mimi naomba niulize maswali ya kiukweli ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la umeme Rufiji ni takribani mwaka mmoja sasa tunapata umeme kwa saa nne tu kwa siku. Hali hii imesababisha vijana wa pale Ikwiriri kufunga viwanda vyao vidogo vya *furniture* kwa kuwa umeme wakati mwingine unakuja usiku. Naomba kufahamu kauli ya Serikali waliyoitoa kwamba nchi hii hakuna mgawo wa umeme, je, Rufiji siyo sehemu ya Tanzania? Hilo ni moja.

Swali la pili, wananchi hawa wa Rufiji hawana barabara hata robo kilometa, hawana maji, hawana hospitali hata *X-ray machine* hawana japokuwa wilaya hii ni ya zamani sana. Mchango wa Rufiji kwa Pato la Taifa ni asilimia 19 kutokana na hifadhi ya Taifa pamoja na misitu. Naomba kufahamu kwa nini Serikali inawachonganisha wananchi wa Jimbo la Rufiji na Chama chao cha Mapinduzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Mchengerwa kwa maswali yake mazuri, lakini kwa jinsi anavyowawakilisha wananchi wa Rufiji. Mheshimiwa Mchengerwa hongera sana na wananchi wako nadhani watapata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kwenye maswali mazuri ya nyongeza ya Mheshimiwa Mchengerwa. Suala la kukatikakatika kwa umeme, maeneo yanayopatiwa umeme kutoka Somanga Funga ambao ni mtambo unaosambaza umeme maeneo ya Rufiji pamoja na Kilwa, ni kweli kabisa kuna tatizo hilo. Kama nilivyowaeleza juzi mtambo wetu wa Somanga Funga ulikuwa na matatizo. Mtambo huu una vituo vitatu na mashine tatu za kuzalisha umeme, lakini mashine zilikuwa na matatizo ya uchakavu jambo ambalo tunalifanyia kazi na Serikali imetenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ukarabati. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mchengerwa pamoja na wananchi wa Rufiji mtambo huo utarekebika na kukatika umeme kutaisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata ule mtambo wa tatu ambao pia ulikuwa na hitilafu tunafunga sasa mtambo mwingine kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa umeme kwenye Mji wa Rufiji ambao unagharimu shilingi bilioni mbili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mchengerwa na wananchi wake watapata umeme wa uhakika hivi karibuni. Nimhakikishie vijiji vyake vyote vya Luwe,

Ngarambe, Ngombani, Kilimani A na B na Mashariki vyote vitapata umeme. Kwa hiyo, wananchi watapata umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri kwamba Rufiji ni sehemu ya Tanzania kama vijiji vingine. Sasa nijibu swali la pili kwa nini Serikali inawachonganisha wananchi wa Rufiji na maeneo mengine, sidhani na sina uhakika Mheshimiwa Mchengerwa. Nikiri kwamba Serikali haiwachonganishi wananchi wa Rufiji na maeneo mengine. Japo swali lako linahusiana na masuala ya barabara, maji, umeme lakini kwa vile Serikali ni moja nimhakikishie kwamba Serikali ya Awamu ya Tano haiwachonganishi wananchi na Rufiji na maeneo mengine. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MWENYEKITI:** Tuna maswali zaidi ya saba na muda umekwenda sana na kuanzia sasa hatutakuwa na maswali mengine ya nyongeza zaidi ya muuliza swali la msingi. Tunaendelea na swali la Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi.

Na. 80

**Ujenzi wa Barabara ya Bunda – Kisorya – Nansio**

**MHE. JOHN W. HECHE (K.n.y. MHE. JOSEPH M. MKUNDI)** aliuliza:-

Ni miaka mitatu sasa tangu barabara ya Bunda – Kisorya - Nansio iwekwe katika mpango wa ujenzi kwa kiwango cha lami lakini ujenzi huo unasuasua tu.

(a) Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utakamilika?

(b) Je, Serikali ina kauli gani juu ya ujenzi wa daraja kati ya Kisorya (Bunda) na Lugezi (Ukerewe)?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Nyamuswa (Bunda) - Kisorya - Nansio yenye urefu wa kilometa121.9 inaunganisha Mikoa ya Mara na Mwanza.

Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* imeanza kutekeleza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami katika awamu ya tatu; Nyamuswa - Bunda - Bulamba (kilometa 55); Bulamba – Kisorya (kilometa 51) na Kosorya - Nansio (kilometa 15.9) ikihusisha pia ujenzi wa daraja kubwa kati ya Kisorya na Lugezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara hii umekamilika isipokuwa sehemu ya Kisorya - Nansio (kilometa 15.9). Ujenzi wa kiwango cha lami umeanza kutekelezwa Disemba 2013 kwa sehemu ya Bulamba - Kisorya (kilometa 51) na unaendelea. Hadi sasa ujenzi wa sehemu hii ya barabara umekamilika kwa asilimia 14. Hata hivyo, ujenzi wake umekuwa ukisuasua kutokana na kucheleweshwa kwa malipo ya mkandarasi. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha ili kukamilisha ujenzi wa barabara hii.Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* imeanza mipango ya ujenzi wa daraja kati ya Kisorya na Lugezi linalounganisha Mikoa ya Mara na Mwanza ambayo imekamilisha upembuzi yakinifu na kwa sasa usanifu wa kina unaendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa majibu yaliyotolewa hapa na kwa niaba ya watu wa Ukerewe ambao Mbunge wao anaumwa ameniomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, barabara hii imeanza kujengwa mwaka 2013 mpaka leo ni zaidi ya miaka minne barabara iko asilimia 14 na Serikali inakiri hapa kwamba ujenzi unasuasua. Hii ni barabara inayounganisha Mkoa kwa Mkoa wala hata siyo Wilaya kwa Wilaya. Sasa ni lini au ni miaka mingapi, kwa sababu tukigawa hapa asilimia 85 iliyobaki ni miaka zaidi ya sita, ina maana mtoto azaliwe leo afikishe miaka sita aanze shule hamjamaliza barabara ambayo mmeanza kujenga miaka 13. Ni lini mnamaliza ujenzi wa barabara hii ambayo inaunganisha Mkoa kwa Mkoa msaidie watu wa Ukerewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili, mara nyingi tumeuliza hapa hilo swali Waziri, barabara ya kutoka Tarime Mjini - Nyamwaga - Nyamongo - Serengeti ambayo inapita kwenye Mgodi wa Nyamongo ambapo kila siku pale Serikali inapata pesa nyingi za wananchi wa Tarime. Ni lini mtaijenga barabara hii ili wale watu na wao wafurahie maisha kwamba ndiyo wanaotoa dhahabu inayochangia kwenye ujenzi wa miundombinu hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lini tunamaliza kujenga hiyo barabara siyo rahisi kumwambia lini, lakini anafahamu kwamba barabara hii ipo katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 - 2020. Ni ahadi yetu na Mheshimiwa Mbunge anafahamu Serikali hii ya Awamu ya Tano ikiahidi inatekeleza.Kwa hiyo, mimi namhakikishia barabara hii itakamilika katika kipindi hiki cha miaka mitatu na anafahamu fedha hizi zinatokana na kodi ambazo tunakusanya. Mheshimiwa Mbunge ajitahidi tukusanye kodi nyingi barabara hii tuikamilishe kwa muda ambao yeye na mimi tutakubaliana.

Swali la pili kuhusu barabara ya Tarime - Nyamwaga - Nyamongo - Serengeti nayo anafahamu ipo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020. Vilevile anafahamu kwamba tumeshaanza kazi, naomba aiamini Serikali hii, kazi hii tutaifanya. Sisi tuliopata dhamana ya kusimamia ujenzi wa barabara hii tunamhakikishia tutaijenga kwa kadri fedha tutakavyozipata.

**MWENYEKITI**: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 81

**Ujenzi wa Barabara ya Kibaha - Mapinga**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, ni lini Ujenzi wa barabara ya Kibaha - Mapinga, km 23 kwa kiwango cha lami utaanza na kukamilika kama ilivyoahidiwa kwenye Ilani ya CCM ya mwaka 2015?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kibaha *(TAMCO)* - Mapinga yenye urefu wa kilometa 23 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara kupitia Ofisi ya Meneja wa Mkoa wa Pwani. Ili barabara hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami, Serikali imefanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambao umekamilika. Pamoja na juhudi hizo hadi sasa tayari ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa moja kuanzia njia panda ya *TAMCO* umekamilika kwa kuwa eneo hilo halikuwa na tatizo la ulipaji wa fidia.

Eneo lote lililobaki katika barabara hii linahitaji kulipa fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa barabara hiyo. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha za kulipa fidia kabla ya kuendelea na ujenzi wa sehemu iliyobaki.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na naishukuru Serikali kwa ujenzi wa kilometa moja lakini pamoja na majiibu hayo ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kwa mujibu wa jibu la msingi kwamba kiwango cha kilometa 24 zilizobaki zinahitaji malipo ya fidia na kwa kuwa tarehe 7 Septemba, 2016 tulifanya kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa na taarifa ilitolewa kwamba takribani shilingi bilioni nane zitatakiwa kwa ajili ya fidia. Je, Serikali haioni kwa kuwa kiwango ni kikubwa kuongeza kama kilometa tano za ujenzi wa barabara hii kwenye eneo la viwanda kwenye maeneo hayo Kibaha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa ujenzi wa barabara hii ni ahadi ya Serikali ya Awamu ya Nne na kwa kuwa zipo ahadi mbalimbali za ujenzi wa miundombinu ambazo hazikukamilika kwa Awamu ya Nne, je, Wizara haioni imefika wakati sasa iunde timu ya tathmini ya ahadi zote ambazo hazikutekelezwa ili ziweze kutekelezwa awamu hii na hususani kuanzia mwaka ujao wa fedha na kuendelea? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Subira Mgalu kwa kufuatilia mambo mbalimbali ya Mkoa mzima wa Pwani, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo la viwanda la kilometa tano analoliongelea mimi namhakikishia ujenzi utaanza kama nilivyosema katika jibu langu la msingi mara tutakapopata zile fedha za fidia na kuwaondoa wale watu ambao wanatakiwa wafidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la tathmini ya ahadi ambazo hazijatekelezwa na viongozi wakuu, kwanza naomba nimhakikishie ahadi zote za viongozi wetu wakuu wa Serikali ya Awamu ya Nne na Serikali ya Awamu ya Tano orodha tunayo. Namhakikishia Serikali hii ya Awamu ya Tano kazi yake kubwa ni kuhakikisha kwamba ahadi zote za viongozi wakuu wa kuanzia Serikali za nyuma zinatekelezwa kikamilifu. Nitamshirikisha kumuonesha orodha kamili ya ahadi ambao zilitolewa na Awamu ya Tatu, Nne na Tano katika Mkoa wa Pwani

ili aelewe ninachokisema kwamba tuna dhamira ya dhati kuhakikisha ahadi za viongozi wetu zinatekelezwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa muda wetu umekwisha, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Na. 82

**Ongezeko la Fedha za Kujikimu kwa Wanafunzi wa Vyuo Vya Elimu ya Juu**

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA** aliuliza:-

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ilifanya ongezeko la fedha za kujikimu kwa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu kwa shilingi 1,000 kutoka shilingi 7,500 mpaka shilingi 8,500 katika mwaka wa fedha 2015/16 ongezeko ambalo haliendani na kasi ya mfumuko wa bei uliorekodiwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kutoka aslimia 4.2 Februari, 2015 mpaka kufikia asilimia 5.6 Februari, 2016:-

Je, Serikali iko tayari kuongeza fedha hizo kufikia shilingi 10,000 kwa siku ili kuendana na kupanda kwa gharama za maisha?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifanya utafiti juu ya gharama halisi za maisha ya wanafunzi ambazo hujumuisha gharama za chakula na malazi. Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilifanya utafiti katika vyuo vyote nchini ili kujua gharama halisi ya chakula na malazi. Utafiti huo ulionesha kuwa gharama hizo zilikuwa kati ya shilingi 8,000 mpaka 8,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa utafiti huo hufanyika kila baada ya miaka miwili, Wizara yangu itafanya utafiti mwingine, ili kubainisha gharama halisi za chakula na malazi. Matokeo ya utafiti huo yatatumika kupanga viwango vya fedha atakazolipwa mwanafunzi kwa kuzingatia gharama halisi pamoja na upatikanaji wa fedha.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na nitambue kazi kubwa inayofanywa na Wizara hii katika utekelezaji wa majukumu yake, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti mfumo wa uhakiki wa vigezo vinavyotumika kutoa mikopo kwa wanafunzi, ili kuhakikisha wanaopata mikopo ni wenye sifa na uhitaji na sio wale ambao wanafanya udanganyifu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mfumo huu wa utoaji mikopo utaendelea kuwa himilivu na endapo idadi ya wanafunzi itaendelea kuongezeka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu. Maswali yake ni mazuri mafupi na majibu yako yawe mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Bodi inatakiwa kuhakikisha kuwa kumbukumbu za wote wanaoomba mikopo zinakuwa kamilifu kwa kushirikiana na vyuo ambavyo vina wanafunzi wanaopewa mikopo hiyo. Kila chuo kinatakiwakuwa na dawati maalum ambalo linashughulikia mikopo, lakini pia katika kutoa mikopo ni lazima kuzingatia vigezo na sifa ambazo zimewekwa. Hivi karibuni Wizara imepitia vigezo hivyo na vigezo vinazingatia hasa uhitaji, uraia, lakini pia uombaji lazima upitie kwenye mtandao na vilevile kwa kuzingatia mahitaji ya nchi, yaani kipaumbele katika taaluma ambazo zinahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuona kwamba, mikopo hiyo inakuwa endelevu ni kwamba, Wizara baada ya kuangalia matatizo yaliyokuwa yakijitokeza katika ulipaji wa mikopo, imeangalia upya Sheria ya Bodi ya Mikopo na hivyo tuko katika kutaka kuileta Bungeni, ili kuona kwamba, inarekebishwa kuweka mikopo kuwa ni deni la kipaumbele kwa mwombaji ambaye ameshamaliza chuo. Lakini vilevile kuhakikisha kuwa waajiri wanahusika nao moja kwa moja katika kuhakikisha mikopo hiyo inalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika sambamba na hiyo tunaangalia namna ya kuboresha upya mifumo mizima ili kuona mfumo huo unaweza kuongea na taasisi nyingine zinazohudumia raia, ikiwemo ya Vitambulisho vya Taifa. Ahsante.

Na. 83

**Tafiti za Vyuo Vikuu Kusaidia Wananchi**

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI** aliuliza:-

Baadhi ya vyuo vikuu nchini vinaendelea kufanya tafiti mbalimbali zenye manufaa kwa wananchi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuviwezesha vyuo vikuu vyote hapa nchini, vikiwemo vya Tumaini na Mkwawa kufanya tafiti zitakazosaidia jamii kubwa ya wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali iliazimia na kuanza kutenga kiwango kikubwa cha fedha za utafiti ikilinganishwa na miaka ya nyuma ili kuhakikisha kuwa tafiti zinafanyika kulingana na vipaumbele vya kitaifa. Serikali imekuwa ikitenga fedha hizi kupitia Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (MTUSATE) unaoratibiwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* kulingana na Sheria Namba 7 ya mwaka 1986 iliyoanzisha Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za utafiti kutoka kwenye mfuko huu zimekuwa zikitumiwa na watafiti wa ndani ya nchi wakiwemo watafiti kutoka vyuo vikuu. Utaratibu ni kwamba miradi hii ya utafiti hufadhiliwa kwa misingi ya ushindani kupitia ubora wa maandiko ya miradi ya utafiti. Hivyo basi, vyuo vikuu vyote vikiwemo Vyuo Vikuu vya Tumaini na Mkwawa vinayo nafasi ya kupata fedha hizo iwapo vitaomba na kukidhi vigezo husika vya ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, vyuo vikuu vyote vinatakiwa kutenga fedha kupitia bajeti zao pamoja na kutafuta wafadhili, wadau wa maendeleo kwa ajili ya kuendeshea shughuli mbalimbali za maendeleo, ikiwemo kufanya utafiti.

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante ka kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa zipo tafiti nyingi muhimu zilizokwishafanyika, ikiwemo tafiti ya uyoga pori kwa matumizi ya chakula, je, Wizara imejipanga vipi kufikisha matokeo ya tafiti hizo kwa wananchi walio wengi, hasa ambao wako vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Waziri anaweza kuahidi nini kwa vyuo vikuu vilivyoko mkoani Iringa kuhusiana na ongezeko la bajeti yao ya tafiti katika mwaka ujao wa fedha? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru sana Mheshimiwa Mwamwindi kwa kuweka kipaumbele katika maeneo haya ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa tafiti inapofikia katika nafasi ya uendelezaji *(commercialization)* inakutana na changamoto kubwa ya kuendeleza kutokana na kutokuwa na fedha zinazoweza kuondoa utafiti huo katika awamu ya awali na kufikisha katika hatua ambayo sasa inaenda kwenye matumizi. Vilevile Wizara imeliona hilo, lakini pia, hata wanasayansi wengine wa nchi za *SADC* wameliona hilo na hivi jitihada iliyopo ni kuona kwamba katika kila nchi, fedha za utafiti angalau ziwe ni asilimia moja ya bajeti ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa Chuo cha Iringa kwanza niwapongeze kwa hatua mbalimbali wanazozifanya, lakini niwasisitize kuwa wanachotakiwa ni kuandika hayo maandiko mazuri, ili sasa Wizara iweze kutoa kipaumbele katika ku-*support* bajeti za utafiti za chuo hicho.

Na. 84

**Mpango wa Ujenzi wa Maabara ya Kupimia Ubora wa Asali Nchini**

**MHE. JOHN P. KADUTU (K.n.y. MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA)** aliuliza:-

Serikali ina mpango wa kujenga maabara ya kupima ubora na kiwango cha asali inayozalishwa hapa nchini.

Je, ni kwa nini Serikali isijenge maabara hiyo mkoani Tabora ambako ndipo kunazalishwa asali nyingi kuliko mkoa wowote nchini?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali namba 84, kwa ruhusa yako nilikuwa naomba uniruhusu niseme kidogo juu ya janga lililowapata wananchi wa Tanzania, hususan Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Kamati ya Uongozi ya Bunge na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa namna ambavyo kipekee mliguswa na tatizo la wananchi wenzetu wa Tanzania walioko mkoani Kagera. Lakini nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi na wadau ambao waliitikia wito wa Mheshimiwa Waziri Mkuu jana na kufika kumuunga mkono na kuweza kukusanya bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 1.369.

Nichukue fursa hii Waheshimiwa Wabunge, tusaidiane na Serikali kuhamasisha njia hii. Kiasi kilichokusanywa jana tulijiandaa kwa saa 30, tukijiandaa wote kwa pamoja tutatunisha Mfuko wa Maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nichukue fursa hii kuwapa pole wananchi wa Mkoa wa Kagera, hasa Wilaya za Muleba, Karagwe, Kyerwa, Bukoba Vijijini, Bukoba Mjini na Misenyi, watulie Serikali ipo na Serikali itahakikisha hali inarudi katika hali ya kawaida na kimsingi baada ya kujibu swali hili itabidi niondoke mwenyewe niende *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijibu swali namba 84. Upimaji wa ubora na viwango vya bidhaa aina ya asali unafuata kiwango chenye namba 851 cha mwaka 2006. Chini ya kiwango hiki maelezo na vigezo vimetolewa ambavyo mzalishaji, mtunzaji, muuzaji na mpimaji wanapaswa kuzingatia ili asali iwe katika ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wote kwa kufuata vigezo na maelezo katika kiwango namba 851 wanaweza kupima asali; hata hivyo, maabara kuu inayopaswa kutoa uthibitisho ipo *TBS* Dar es Salaam. *TBS* Makao Makuu ndio wanaopaswa kisheria kutoa hati ya ubora chini ya utaratibu maalum. Tunapoendelea kuhimiza ujenzi wa viwanda, ikiwemo viwanda vya asali, tutahakikisha viwanda hivyo vinakuwa na maabara zinazoweza kupima viwango vya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa maabara Tabora, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, wawekezaji ambao wanafuatilia ujenzi wa viwanda vya asali mkoani Tabora, Wizara yetu itahakikisha wanakuwa na maabara za kupima viwango vya msingi na kuiachia *TBS* kuweka Viwango vya Kitaifa na kudhibiti viwango hivyo.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza; kumekuwa na taarifa kwamba asali yetu ya Tabora ina chembechembe za sumu, lakini je, Serikali imewahi kufanya utafiti wa kisayansi na kuja na majibu ambayo yataleta ukweli wa jambo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali sasa iko tayari kuwasaidia wanaoshughulika na zao la asali kuwapatia masoko yenye uhakika, kwa sababu mara nyingi wanakuja watu kutoka nchi za Uarabuni na kununua asali katika njia za panya.

Je, sasa Serikali inao mkakati gani mahususi kuwasaidia wananchi hawa ili asali yao iweze kupata soko la uhakika bila kunyonywa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asali ya Tabora na asali ya Tanzania haina chembechembe yoyote ya sumu, ni asali safi na *world demand* (mahitaji ya dunia) kwa asali ya Tanzania ni tani 5,000 kwa wiki, tani 260,000 kwa mwaka, kiasi kinachoweza kuingiza trilioni nane kwa asali ni kwamba sisi tumebaki kuchangamka. Kwa hiyo, wanaosema ina sumu hawatutakii mema tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masoko ya uhakika kwa kushirikiana na *UNDP, TAN TRADE* na Wizara yangu tunaandaa mfumo wa soko na mfumo wa soko unaanza kwa kuchakata asali. Nilijibu swali la kwanza la msingi, kimsingi ni-*declare interest,* kuna mwenzetu tunahangaika kupeleka kiwanda cha kwanza cha asali Tabora. Kiwanda cha asali ni dola 50,000 kwa hiyo, wenzetu wanaotupiga madongo toka nchi jirani wamekuwa wakichukua ile *raw honey* ambayo haijachakatwa na kuchakata nchini kwao na ku-*pack* kupeleka. *TANTRADE* na Wizara yangu, tunalishughulikia na nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, tuelekezane, nunua viwanda, mtaweza kuona faida, faida iko kwenye asali. Trilioni nane ni mara mbili ya pesa tunazotumia kununua mafuta jamii ya petroli ambayo inatu-*cost* trilioni nne kwa mwaka.

Na. 85

**Viwanda Vilivyobinafsishwa Visivyofanya Kazi**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni aliahidi kuvirudisha Serikalini viwanda vyote vilivyobinafsishwa, lakini havifanyi kazi.

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa ahadi hiyo?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa agizo la Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, la kuhakikisha viwanda vilivyobinafsishwa vinafanya kazi, lilianza kutekelezwa mwezi Novemba, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kwanza ilikuwa ni Ofisi ya Msajili wa Hazina kuwataka wote waliopewa viwanda katika mtindo huo kutoa taarifa ya kina ya utendaji wa viwanda hivyo. Timu ya wataalam kutoka Wizara ya Viwanda na Ofisi ya Msajili wa Hazina walifuatilia na wanaendelea kutathmini

kwa kutembelea kiwanda baada ya kiwanda, ili kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayosababisha kiwanda kutokufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya taratibu hizo hapo juu, Wizara yangu inaendelea na zoezi la kuchambua mikataba ya mauzo kwa viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo ama havifanyi vizuri au vimesimama uzalishaji kabisa. Uchambuzi huo unafanyika kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina pamoja na Wizara za kisekta ambazo ni Maliasili na Utalii, Nishati na Madini, Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Uchambuzi huo unaangalia hali ya umiliki, wajibu wa mwekezaji, wajibu wa Serikali, utekelezaji wa mkataba wa mauzo, hali ya sasa ya kiwanda na hivyo kutoa mapendekezo ya hatua stahiki. Zoezi hili linaenda sambamba na ulinganishaji wa taarifa za uwekezaji katika viwanda vilivyobinafsishwa zilizowasilishwa kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina na wamiliki wa viwanda hivyo kama nilivyoeleza hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tathmini ya hali ya viwanda nayo inaendelea kufanyika kwa ushirikiano wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ambapo viwanda 45 tayari vimefanyiwa tathmini. Kati ya viwanda hivyo, viwanda vinne vimeonesha dalili kuwa wawekezaji wa sasa hawana uwezo wa kuvifufua hivyo, kuwa na uwezekano wa Serikali kutafuta wawekezaji wengine. Taarifa ya tathmini itakapokamilika itawasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupata maoni ya kisheria katika njia muafaka ya kutwaa viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine ambayo tumeichukua katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ni Serikali kukitwaa kiwanda cha chai Mponde *(Mponde Tea Estate Limited)* kilichopo Lushoto – Tanga, ambacho mwekezaji amekiuka makubaliano ya kimkataba. Kiwanda hicho kilitwaliwa tarehe 29 Januari, 2016 na tayari mazungumzo kati ya Serikali na Mfuko ya Hifadhi ya Jamii wa *Local Authority Provident Fund – LAPF* yanaendelea. Mazungumzo hayo ni matokeo ya maagizo ya Mheshimiwa Rais kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza katika sekta ya viwanda.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida pamoja na Mkoa wa Dodoma ni miongoni mwa mikoa masikini ambayo inahitaji usaidizi wa Serikali. Sasa Mheshimiwa Waziri yuko tayari kusaidia wananchi wa mikoa hii ya Dodoma na Singida kwa ushawishi wake mkubwa na weledi wake kufanya basi angalau kiwanda kimoja kiwekezwe katika Mkoa wa Singida, hususan katika Jimbo la Manyoni Magharibi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kutembelea wananchi wa Itigi ili kujionea fursa zilizopo ili kushawishi wawekezaji waweke kiwanda katika eneo la Itigi? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kama niko tiyari kuwekeza Singida na Dodoma? Niko tiyari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili ni kutembelea Itigi.Ninapaswa kutembelea Singida kwenye Jimbo la Mheshimiwa Kingu, kuna mradi wa maziwa, tutapanga twende wote.

Lakini nichukue fursa hii kuwaeleza kwamba ukanda huu una fursa ya maziwa, una fursa ya viwanda vya mafuta jamiii ya alizeti na una fursa ya sekta ya ngozi. Hapa Dodoma Wizara yangu imetengewa ekari 200 na ninayo pesa tayari ya kutengeneza *cluster* ya ngozi.

Kwa hiyo, hii ni sehemu ambayo ni *potential* na kwa kutumia ngozi tutatoka; mnajua idadi ya ng'ombe tulio nao. Kwa hiyo, Dodoma tunaweza kutengeneza viatu tukavika Afrika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yote yamekwisha na sasa ni kipindi cha matangazo. Lakini nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa sana walioifanya baada ya tukio la janga la tetemeko la ardhi ambayo nchi yetu imepata siku nne/tano zilizopita.

Waheshimiwa Wabunge, Uchina mwaka 1988 kulikuwa na tetemeko la ardhi, walikufa watu 80,000 na dunia yote ikahamia Uchina kupeleka misaada. Kwa hiyo, kazi iliyofanywa jana na Waziri Mkuu imeonesha mshikamano wa Kimataifa na mshikamano wa Kitanzania. *(Makofi)*

Nawashukuru Wabunge wote kwa hoja aliyoitoa Mheshimiwa Shangazi ya tukatwe posho yetu ya siku moja. Kwa hiyo, utaratibu wa Kibunge utafanywa, Mheshimiwa Waziri Mkuu natumaini Spika utawasiliana naye ili na mchango wetu uje. Wabunge wote wamechangia, nawapongeza na kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuweka *rapid deployment team* ndicho kilichotakiwa kufanywa. Inapotokea tatizo una-*deploy* wataalam haraka sana kwenye eneo lililohusika, ndio namna Serikali ilivyofanya kazi. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na viongozi wote na Mawaziri wote ambao walihusika na zoezi hili. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, waliopo Jukwaa la Spika; wageni 11 ambao Waheshimiwa Wabunge saba na maafisa wanne kutoka Bunge la Kenya waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ambao watakutana na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge wakiongozwa na Dkt. James Murgor - kiongozi wa msafara, karibuni Tanzania, karibuni Dodoma.

Wageni 13 wa Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni viongozi mbalimbali waliokuja kushiriki katika uzinduzi wa miongozo, anuani za makazi, sheria ndogo na *post card. (Makofi)*

Pia kuna wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Katiba na Sheria wanatokea Jimboni kwake Kyela Mkoani Mbeya, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Kuna wageni 27 wa Mheshimiwa Freeman Mbowe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wanaotoka Jimboni kwake Hai, wakiongozwa na Diwani wa Kata ya KIA Mheshimiwa Yohana T. Laizer, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Mboni Mhita ambao ni wanakwaya kutoka Mtakatifu Francis iliyopo Handeni Vijijini Mkoani Tanga.

Aidha, kuna mgeni mmoja wa Mheshimiwa Halima Mohamed ambaye ni mtoto wake kutoka Mkoa wa Kusini Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Raisa Abdallah Mussa ambao ni watoto wake na wajukuu zake kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud A. Khamis ambao ni watoto wake na shemeji zake kutoka Mkoa wa Magharibi Zanzibar, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni wanafamilia yake kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia kuna wageni tisa wa Mheshimiwa Oran Njeza ambao ni wadau wa zao la pareto kutoka Mkoa wa Mbeya. Aidha, kuna wageni watatu wa Mheshimiwa Alex Gashaza kutoka Redio Kwizera iliyopo Ngara Mkoani Kagera, karibuni.*(Makofi)*

Kuna mgeni mmoja wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambaye ni kaka yake anayetokea Karagwe Mkoani Kagera na wageni wanne wa Mheshimiwa Venance Mwamoto wanaotokea Kilolo, Mkoani Iringa. *(Makofi)*

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 47 na walimu watano kutoka *Mother Kelvin English Medium School* iliyopo Wilaya ya Same, Mkoani Kilimanjaro, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Pia kuna wanafunzi 68 na walimu watano kutoka shule ya msingi *Maria De Mathias* kutoka Mkoani Dodoma, karibuni sana na muwakumbushe wenyeji wenu kuna chai pale kantini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kukumbushwa kwamba leo tarehe 14 Septemba, 2016 kutakuwa na uzinduzi wa miongozo ya mfumo wa anuani ya makazi za post kadi ambayo itafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa 7.00 mchana. Mgeni rasmi katika uzinduzi huo atakuwa ni Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria.

Tangazo la msiba, nasikitika kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Mheshimiwa Vedatus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini amefiwa na mama yake mzazi jana tarehe 13 Septemba, 2016 katika Hospitali ya Agha Khan Dar es Salaam alipokuwa akipatiwa matibabu. Mwili wa marehemu utasafirishwa kesho tarehe 15 Septemba, 2016 kwenda Musoma kwa ajili ya mazishi. Mungu ailaze roho yake marehemu mahali pema peponi, Amina.

Katibu!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mwongozo Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Waitara…

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Haonga.

**MWENYEKITI:** Haonga?

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Eeh!

**MWENYEKITI:** Haya tunaanza na Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ninaomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) na ninaomba ili kuokoa muda nisiisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Bunge lako tukufu limetuhumiwa kwa rushwa. Gazeti la Nipashe ukurasa wa kwanza katika kichwa kikubwa kabisa cha habari kuna habari inayosema kwamba Mbunge wa CCM atoboa

Wabunge wanavyohongwa. Ukipitia ndani ya gazeti hili na ninaomba uniruhusu ninukuu kidogo anasema; "kuna wakati mwingine unaweza kuletewa taarifa za udanganyifu na wewe ukafanya maamuzi kupitia taarifa hizo, mwisho wa siku unapotoka na kupotosha Taifa. Niliamua kusema vile kwa sababu suala hilo linatetewa na baadhi ya Wabunge wa CCM na hata Wabunge wa Upinzani walikuwa hawajui chochote kinachoendelea."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu jambo hili likiachwa, linaingilia haki, kinga, maadili na madaraka ya Bunge. Ninakuomba kwa mamlaka uliyonayo kwa sababu hii ni *generalization,* ni kana kwamba Wabunge wote wamehusishwa mpaka Mbunge wa Ruangwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, maana yake hakuna majina yaliyotajwa humu ndani.

Ninakuomba kwa mamlaka uliyonayo Mbunge anaehusika na kwa mujibu wa gazeti hili ametajwa Mbunge wa Jimbo la Manonga, Mheshimiwa Seif Gulamali aombwe ili aweze kulieleza Bunge hili, Wabunge wanaohusika katika kushawishi rushwa au kushawishiwa kutoa rushwa ili kulirejeshea Bunge lako heshima miongoni mwa wananchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninaomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) na naomba kwa kuokoa muda nisiisome.

Muda mfupi uliopita ulipongeza viongozi mbalimbali akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye tunajua alienda Kagera, Bukoba na wengine waliohusika lakini hukumtaja kiongozi wa Upinzani Bungeni ambaye baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoka pale alienda na sisi Wabunge wa Upinzani kabla hata ya azimio la jana tulishakubaliana kuchangishana fedha na zilishakabidhiwa kwa Kiongozi wa Upinzani akabidhi kwa ajili ya kusaidia wenzetu ambao wamepata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba Mwongozo wako hao viongozi tunapokuwa tunapeana nafasi za kupongezana na wewe hutaji kiongozi mkubwa namna hiyo katika upinzani na kwa mujibu wa Kanuni anatajwa nadhani sio jambo jema.

Kwa hiyo, naomba Mwongozo wako lakini izingatiwe pia kwamba tumekuwa na malalamiko kwamba matukio mbalimbali ya Kitaifa viongozi wetu wanaenda Mameya, Wabunge hawatambulishwi na haya yametajwa. Kwa hiyo, naomba Mwongozo wako ili tuweze kwenda sawasawa, vinginevyo naunga mkono wote ambao wanaendelea kusaidia janga hili na wanaoendelea kutoa michango na wanoendelea kuguswa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo alioomba ndugu yangu Waitara kwa hiyo Kanuni ya 68(7) na mimi nilitaka niombe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa ni mfululizo wanatajwa viongozi mbalimbali ambao wameenda kwenye lile tukio lakini kiongozi wetu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haguswi, hatajwi utafikiri hajashiriki wakati tangu siku ya kwanza yupo pale.

Kwa hiyo, dharau hii naona tu kwamba ni vizuri tusijaribu kuonesha dharau, huyu ni kiongozi mkubwa sana. Kwa hiyo, kwa sababu mwenzangu ameshatangulia basi naomba tu niungane naye kwa sababu ameshaomba huo mwongozo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asanteni sana.

Kuhusu Mwongozo wa Mheshimiwa Selasini kuhusu rushwa ambayo ameona kwenye vyombo vya habari. Bunge hili halifanyi kazi na vyombo vya habari ndio Mwongozo wangu na kama kutakuwa na jambo lolote la ziada mamlaka zinazohusika zitalifanyia kazi taarifa hizo.

Waheshimiwa Wabunge,nikishasema ndio nishasema nataka niwape mfano mdogo tu ili muelewe kanuni na *rules* tulizojiwekea hata mpirani *referee* akishasema ndio kasema, ukibisha kidogo utakwenda nje. *(Makofi/Kicheko)*

Kuhusu suala la Mwongozo wa Mheshimiwa Waitara, kwa nini Kiongozi wa Upinzani hakutajwa katika pongezi. Nikubali sikumtaja na nimuombe radhi, sababu na yeye alihusika na hili suala lisitugawe, litufanye tuwe kitu kimoja. Nafikiri hii nimekujibu vilevile Mheshimiwa Haonga. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Na ule wa kwanza ule kuhusu tuhuma.

**MWENYEKITI:** Wewe kaa chini. Katibu!*(Kicheko)*

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo wa mwaka 2016 *[The Tanzania Agricultural Research Institute Bill, 2016]***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano walioutoa kwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika kuboresha Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania ya mwaka 2016. Muswada huu umezingatia maoni ya wadau yaliyotolewa kwa Kamati ya Bunge tarehe 24 hadi tarehe 25 Agosti, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la muswada huu ni maamuzi ya Baraza la Mawaziri kupitia waraka namba 2 wa mwaka 2014/2015 kuhusu mapendekezo ya Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania mwaka 2016. Kupitia kikao chake cha tarehe 4 Novemba, 2014 Baraza la Mawaziri liliridhia na kuelekeza kutungwa kwa sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania. Muswada unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti ya Kilimo Tanzania, 2016. Sheria inayopendekezwa inakusudia kuweka mfumo wa utafiti unaolenga kuimarisha shughuli za utafiti wa kilimo kwa ujumla kulingana na mahitaji ya sasa ili kuongeza upatikani na usambazaji wa teknolojia sahihi kwa ajili ya kuendeleza kilimo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, utasaidia kuimarika kwa matumizi sahihi ya rasilimali za utafiti yaani *cost effectiveness* kwa kulenga katika vipaumbele vya sekta na kuondoa hali ambayo taasisi zaidi ya moja hurudia kufanya miradi ya utafiti inayofanana, *overlaps and duplications*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu yafuatayo yamezingatiwa katika sheria inayopendekeza kutungwa:-

(a) Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo kwa ajili ya kufanya utafiti, kusimamia na kuratibu shughuli zote za utafiti wa kilimo unaofanyika hapa nchini.

(b) Kubainisha majukumu ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na mahusiano yake na wadau wengine wa utafiti ikiwemo mashirika ya umma, taasisi na asasi nyingine za umma na binafsi.

(c) Kuanzisha Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, mamlaka na majukumu ya Bodi ya Wakurugenzi, Mkurugenzi Mkuu, vituo vya utafiti wa kilimo na watendaji wake.

(d) Kuvitambua kisheria vituo vyote vya utafiti wa kilimo *(Agricultural Research Centers)* vitakavyosimamiwa na *TARI* ikiwa ni pamoja na majukumu yake. Vituo ambavyo kwa sasa vipo chini ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ambavyo vitawekwa chini ya *TARI* ni pamoja na Dakawa, Hombolo, Ifakara, Ilonga, Kibaha, Kifyulio, Makutupora, Maluku, Mikocheni, Mlingano, Naliendele, Seriani, Tengeru, Tumbi, Ukiliguru na Uyole.

Aidha, Waziri baada ya kushauriana na Bodi anaweza kuunganisha au kuongeza idadi ya vituo kwa jinsi itavyoonekana inafaa ili kuongeza ufanisi na kufikia malengo ya *TARI*

(e) Kuweka utaratibu wa ushirikishwaji wa wadau wa tasnia ya utafiti wa kilimo kupitia Jukwaa la Taifa la Ushauri wa Utafiti wa Kilimo *(National Agricultural Research Consultative Forum)*. Jukwaa litatoa fursa kwa wadau kujadili changamoto za utafiti na kupendekeza namna ya kukabiliana na changamoto hizo na kupeana taarifa mbalimbali zinazohusu utafiti na kushauri masuala mbalimbali ya utafiti nchini. Aidha, jukwaa litakuwa na wajumbe kutoka katika taasisi, asasi na wadau mbalimbali wanohusika katika uendelezaji wa utafiti wa kilimo.

(f) Kuainisha muundo wa utafiti ambao ni endelevu na kuwiana na miundo ya utafiti hapa nchini na nje ya nchi ili kuwezesha ugunduzi, upatikanaji na usambazaji wa teknolojia sahihi za kilimo nchini.

Pia muswada unaweka utaratibu wa kuanzisha na kuimarisha miundombinu ya utafiti kwa viwango vinavyokubalika kimataifa.

(g) Sheria itaweka vipaumbele vitakavyosimamia masuala ya fedha *(financial provisions)* ili kuhakikisha kuwepo kwa matumizi sahihi ya fedha na vifaa vya taasisi.

(h) Kuainisha wigo wa vyanzo vya fedha kwa ajili ya utafiti na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania.

(i) Kuanzisha Mfuko wa Kuendeleza Utafiti *(Agricultural Research Fund)* ambao utasaidia katika kuhakikisha upatikanaji wa fedha za utafiti kwa manufaa ya TARI na wadau wengine.

(j) Sheria itaweka mfumo utakaovutia watafiti kujiunga na kubaki kwenye sekta ya umma tofauti na hivi sasa ambapo watafiti wenye ujuzi huondoka

kufuata maslahi bora ndani au nje ya nchi. Utaratibu kama utoaji wa motisha kwa watafiti kupitia sehemu ya faida ya mbegu zitakazo gunduliwa utatumika.

(k) Kuweka taratibu za kuwezesha sheria kuzingatiwa na kutekelezwa *enforcement mechanism* kwa kuwaweka Wakurugenzi katika vituo vya utafiti chini ya *TARI.*

(l) Kuweka utaratibu wa kufanya na kusimamia utafiti na watoa huduma za utafiti.

(m) Kuainisha vipengele vya makosa na adhabu.

(n) Sheria itaweka kipengele kitakacho muwezesha Waziri mwenye dhamana kuandaa kanuni za utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya sheria inayopendekezwa kutungwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongezeka kwa ugunduzi, upatikanaji na matumizi ya teknolojia sahihi za kuendeleza kilimo kulingana na mahitaji ya soko.

(ii) Kuongezeka kwa ufanisi wa shughuli za utafiti wa kilimo hapa nchini.

(iii) Kuimarika kwa matumizi sahihi ya rasilimali za utafiti kwa kulenga vipaumbele vya sekta na kuondoa hali ambayo taasisi zaidi ya moja kurudia kufanya miradi ya utafiti inayofanana.

(iv) Kuweka mfumo madhubuti wa kusimamia shughuli za utafiti wa kilimo nchini ikilinganishwa na mfumo uliopo sasa.

(v) Kuimarika kwa ushirikiano kati ya taasisi, mashirika na wadau wengine wanaoshughulika na utafiti wa kilimo ndani na nje ya nchi; na

(vi) Kuimarika kwa mnyororo wa thamani kutokana na utafiti utakaofanywa kulingana na mahitaji ya kila zao ili kuongeza tija na kipato cha wakulima na hivyo kuongeza mchango wa sekta ya kilimo katika uchumi na usalama wa chakula na lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu sita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza inahusu masuala ya utangulizi kama vile jina la sheria inayopendekezwa na tarehe ya kuanza

kutumika, ibara ya pili ya sehemu hii inahusu utafsiri na misamiati mbalimbali kama ilivyotumika katika sheria inayopendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili inahusu masharti ya uanzishwaji na uendeshwaji wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania. Sehemu hii inapendekeza kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania na taasisi hii itakuwa ndicho chombo pekee chenye mamlaka kisheria kusimamia shughuli za utafiti wa kilimo Tanzania Bara. Kwa mujibu wa masharti ya sehemu hii, taasisi itakuwa chini ya Bodi ambayo inaundwa na jumla ya wajumbe tisa watakaoteuliwa na Waziri kutoka katika taasisi mbalimbali. Taasisi itaongozwa na Mwenyekiti wa Bodi atakayeteuliwa na Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 11 ya Muswada inatambua na kuweka chini ya usimamizi wa taasisi vituo mbalimbali vya utafiti ambavyo kwa sasa vipo chini ya Idara ya Utafiti wa Kilimo iliyopo Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili sehemu ndogo (c) inaanzisha Jukwaa la Taifa la Ushauri wa Utafiti wa Kilimo. Jukwaa hili litakuwa ndiyo jukwaa la mijadala mbalimbali kuhusu utafiti wa kilimo na matokeo ya mijadala hii itasaidia taasisi za Serikali kwa ujumla katika kusimamia masuala ya utafiti wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu inapendekeza masharti kuhusu uendeshaji wa taasisi. Pamoja na mambo mengine, sehemu hii ya utafiti inaipa mamlaka bodi ya taasisi kuweka miongozo mbalimbali ya kuratibu utafiti wa kilimo hapa nchini. Sehemu hii pia inaweka masharti ya usimamizi na udhibiti wa utafiti unaofanywa Tanzania au kwa manufaa ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne inahusu usajili wa miradi ya utafiti wa kilimo na usajili wa watoa huduma za utafiti. Pamoja na mambo mengine, sehemu hii inaweka masharti yanayomtaka mtu yeyote anayetoa huduma kuhusu utafiti wa kilimo kupata usajili kabla ya kufanya hivyo. Aidha, kwa mujibu wa masharti ya sehemu hii, mtu yeyote hataruhusiwa kuendesha mradi wa utafiti mpaka mradi huo uwe umesajiliwa. Hivyo kwa msingi huo taasisi itaanzisha na kutunza rejista kwa ajili ya usajili wa huduma za utafiti na miradi ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano inahusu masharti ya fedha. Sehemu hii inaainisha masharti mbalimbali kuhusu vyanzo vya fedha za taasisi, udhibiti wa fedha hizo, ukaguzi wa fedha za taasisi na uwasilishaji wa taarifa za fedha katika ngazi mbalimbali za maamuzi kama vile ngazi ya Bodi, Wizara au Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita ya muswada inahusu masuala ya jumla ambayo ni pamoja na masharti ya adhabu kwa makosa ambayo adhabu zake hazijaainishwa ndani ya sheria, mamlaka ya Waziri kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba muswada huu uingie pamoja na marekebisho yake. Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, mwakilishi. Karibu Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niungane na wenzangu wote kwa kuwapa pole wananchi wa Bukoba waliopatwa na matatizo ya maafa ya tetemeko na niishukuru Serikali kwa kuchukua hatua za haraka na madhubuti ili kuwafariji watu wa Bukoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo mafupi kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Mwaka, 2016 *(The Tanzania Agricultural Research Institute Bill, 2016)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kupokea Muswada wa Sheria, Kamati ilitoa mwaliko kwa wadau mbalimbali kupitia vyombo vya habari, kwa kuwatumia barua na nakala ya muswada kwa njia ya posta na kuwatumia barua pepe. Wajibu huu ulitekelezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Mwaliko uliotolewa ulikusudia kuwapa wadau fursa ya kutoa maoni yao kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya sheria inayokusudiwa kutungwa na hatimaye kuisaidia Kamati kufanya uchambuzi wa kina wa muswada tajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi wa muswada watendaji wakuu wa vituo 16 vya utafiti wa kilimo, taasisi mbalimbali za Serikali na mashirika yasiyo ya Serikali ambayo muswada wa Sheria inayopendekezwa unawagusa walihudhuria vikao vya kamati ili kutoa michango yao kwa njia ya majadiliano na kwa maandishi. Aidha, Chama cha Wanasheria Tanganyika *(Tanyanyika Law Society)* na Muungano wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) walifika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 23 Agosti, 2016 Kamati ilikutana na Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika Ukumbi wa *Mount Meru* ulioko Jengo la *Hazina Square*, Dodoma kwa lengo la kupokea maelezo ya Serikali kuhusu

muswada husika. Aidha, terehe 01 Septemba, 2016 Kamati ilifanya kikao cha mashauriano na Wizara kuhusu marekebisho ya muswada husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kukutana na kupata maoni ya wadau mbalimbali, iliendelea kukutana na watendaji wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, wawakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wawakilishi wa Mshauri wa Sheria kutoka Ofisi ya Bunge kwa lengo la kubadilishana mawazo na kupata uelewa mpana kuhusu maudhui ya muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yake, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi aliieleza Kamati kuwa Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo wa mwaka 2016 unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la sheria inayopedekezwa kutungwa ni kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ambayo pamoja na mambo mengine, itakuwa na jukumu la kufanya na kusimamia tafiti zote za kilimo Tanzania Bara.

Aidha, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa muswada huu una sehemu sita na jumla ya vifungu 38 na kwa ukamilifu unasomeka kuwa ni Muswada wa Sheria wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo wa mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; baada ya utangulizi huo, sasa ninaomba niwasilishe maoni na ushauri wa Kamati kuhusu muswada huu. Maoni haya kwa kiasi kikubwa yametokana na uchambuzi wa Kamati na maoni ya wadau mbalimbali pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Serikali. Hata hivyo, kabla ya kuanza kuwasilisha maoni ya Kamati ninapenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Jedwali la Marekebisho mlilopewa ni matokeo ya uchambuzi wa muswada uliofanywa na Kamati kutokana na muswada wenyewe na maoni ya wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zote zilizoibuliwa na Kamati kuhusu marekebisho ya muswada huu zilikubaliwa na Serikali na kuhitimishwa kama zinavyoonekana kwenye kiambatanisho ambacho ni Jedwali la Uchambuzi wa Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya ambayo muktadha wake unapatikana katika sehemu ya muswada ijulikanayo kama madhumuni na sababu yanalenga kuwezesha yafuatayo kutokea:-

(i) Kuongezeka kwa uzalishaji, upatikanaji na matumizi ya teknolojia sahihi za kuendeleza kilimo kulingana na mahitaji ya soko.

(ii) Kuongezeka kwa ufanisi wa shughuli za utafiti wa kilimo hapa nchini.

(iii) Kuimarika kwa matumizi sahihi ya rasilimali za utafiti kwa kulenga katika vipaumbele vya sekta na kuondoa hali ambayo taasisi zaidi ya moja kurudia kufanya utafiti uliokwishafanywa.

(iv) Kuwepo mfumo madhubuti wa kusimamia shughuli za utafiti wa kilimo nchini ikilinganishwa na mfumo uliopo sasa.

(v) Kuimarika kwa ushirikiano kati ya taasisi, mashirika na wadau wengine wanaoshughulika na utafiti wa kilimo ndani na nje ya nchi; na

(vi) Kuimarika kwa mnyororo wa thamani kutokana na utafiti utakaofanywa kulingana na mahitaji ya kila zao ili kuongeza tija na kipato cha wakulima na hivyo kuongeza mchango wa Sekta ya Kilimo katika uchumi na usalama wa chakula na lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono madhumuni na sababu ya Serikali kuhusu muswada huu kwani yanalenga kuweka mfumo mahsusi wa utafiti utakaowezesha uzalishaji, upatikanaji na usambazaji wa teknolojia sahihi za mazao nchini na kujenga uwezo wa wataalam na miundombinu ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na madhumuni na sababu ya Serikali kuleta muswada huu Bungeni, Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013 imeelekeza kuanzishwa kwa chombo cha kuratibu na kusimamia utafiti nchini. Kwa mujibu wa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, kutokuwepo kwa chombo hiki chenye mamlaka ya kisheria cha kuratibu na kusimamia utafiti wa kilimo kumesababisha kutokuwepo uratibu na usimamizi mzuri wa utafiti na rasilimali zake. Vilevile kutokuwepo na mfumo wa kufanya maamuzi kwa wakati muafaka na athari zake ni pamoja na kutokuwepo ufanisi na utafiti endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata nafasi ya kutathimini uzoefu wa taasisi za nchi nyingine kama *Kenya Agricultural Research Institute, National Agricultural Research Organization* ya Uganda, *Rwanda Agricultural Board, Ethiopian Institute of Agricultural Research, Brazilian Agricultural Research Corporation* (*EMBRAPA*) na *India Agricultural Research Council* na kubaini kuwa miundo ya taasisi hizo imeziwezesha kuwa na utaratibu mzuri na wenye ufanisi, na kwamba miundo hiyo imewezesha kuwepo utaratibu mzuri wa kufikisha matokeo ya utafiti kwa walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huu, Kamati inaona ni wakati muafaka sasa kwa nchi yetu kuwa na sheria hii ambayo itawezesha kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ambayo itakuwa chombo huru cha kusimamia na kuratibu utafiti wa kilimo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kamati kuunga mkono mapendekezo ya sheria inayokusudiwa kutungwa, yapo mambo kadhaa ambayo yaliibua wasiwasi kwa Wajumbe wa Kamati wakati wa uchambuzi wa muswada na hivyo kuhitaji ufafanuzi wa kina kutoka kwa Serikali. Mambo hayo ni pamoja na:-

(i) Sheria Namba 7 ya mwaka 1986 iliyoanzisha Tume ya Sayansi na Teknolojia ambayo imeweka sharti la kuelekeza fedha zote za tafiti katika Mfuko wa Tume ya Sayansi na Teknolojia. Wajumbe walitaka kufahamu kama fedha za tafiti katika Sekta ya Kilimo zitaelekezwa katika mfuko huo, na nini athari zake katika ufanisi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo.

(ii) Wajumbe walitaka kufahamu utaratibu utakaotumika kwa taasisi nyingine za elimu ya juu zinazofanya tafiti za Muswada wa Kilimo.

(iii) Kwa kawaida mahala pengi duniani sekta ya kilimo inajumuisha mazao yatokanayo na kilimo, mifugo na uvuvi, kwa muktadha huu, Wajumbe walitaka kufahamu kwa nini Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo inayokusudiwa kutungwa haijajumuisha sekta za mifugo na uvuvi.

(iv) Wajumbe walitaka kufahamu utaratibu utakaotumika kuhakikisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya tafiti za kilimo.

(v) Wajumbe walitaka kujiridhisha endapo sheria inayoanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania haitaongeza ukiritimba katika utafiti. Wasiwasi wa Wajumbe ulitokana na baadhi ya majukumu yaliyotajwa kwenye sheria yanatekelezwa pia na taasisi nyingine za utafiti kwa mfano, Tume ya Sayansi na Teknolojia ina jukumu la kuratibu shughuli zote za utafiti nchini ikiwa ni pamoja na kilimo. Lakini pia Taasisi ya Tathmini za Rasilimali ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(Institute of Resource Assessment)* inafanya tafiti zilizoainishwa kwenye Jedwali la Tatu Kipengele 6(a),(b) na (c).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, Kamati ilifanya kikao cha majumuisho na Wizara ya Kilimo, Mifugo Uvuvi ambapo Waziri alitoa ufafanuzi wa hoja zote zilizoibuliwa na kufikia muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa muswada; sehemu ya kwanza ya muswada inayohusu masharti ya utangulizi. Katika sehemu hii ya kwanza, Kamati ilitoa maoni na mapendekezo kwenye maeneo kadhaa yaliyohusu:-

(i) Mipaka ya sheria inayokusudiwa kutungwa;

(ii) Kuongeza na kufuta baadhi ya maneno ambayo tafsiri ya maneno hayo ilileta mkanganyiko;

(iii) Kuongezwa kwa vifungu vipya; na mwisho

(iv) Kusahihisha makosa ya kiuchapaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya muswada inahusu uanzishwaji na usimamizi wa taasisi. Katika sehemu hii Kamati ilipendekeza kuongezwa kwa kifungu kipya kitakachobainisha Mamlaka ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, kubadilisha baadhi ya maneno ambayo tafsiri yake ilileta mkanganyiko na kurekebisha baadhi ya makosa ya kiuchapaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu hii pia kulikuwa na marekebisho yaliyotaka uwakilishi wa Makamu Mkuu wa Chuo kikuu cha Kilimo kwenye muundo wa bodi ya taasisi uzingatie weledi wa chuo husika na sio kama ilivyopendekezwa kwenye muswada katika kifungu cha 5(2)(ii) kwamba Makamu Mkuu wa Chuo atakayeteuliwa kutoka katika moja ya vyuo vikuu vya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipendekeza pia katika kifungu cha 5(2)(vii) ambacho kinatoa nafasi ya mkulima mmoja kuwakilisha wakulima wote kwenye wajumbe wa bodi ya taasisi. Kamati imependekeza idadi ya wakulima watakaowakilisha kwenye Bodi iongezwe na kufikia wakulima wawili kwa sababu Bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, pamoja na kazi nyingine, ina jukumu la kumshauri Waziri kuhusu uanzishwaji wa vituo vya utafiti au vituo vidogo vya utafiti ambavyo vitaongeza tija katika kilimo na kupunguza umaskini kwa Watanzania ambao wengi wao ni wakulima, hivyo uwakilishi wa kutosha ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, ni muhimu suala la idadi ya uwakilishi wa wakulima kwenye bodi ya taasisi likazingatiwa kwa uzito unaostahili kwa sababu muswada ulipendekeza uwakilishi wa mkulima mmoja ambapo Kamati inaamini uwakilishi wa mkulima mmoja haukidhi kuwakilisha wakulima wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 5(3) muswada unamtaka Waziri kuteua Wajumbe wa Bodi kwa kuzingatia taaluma, uzoefu na jinsia. Katika kifungu hiki, Kamati imependekeza sheria imtake Waziri kwa upande wa jinsia kuteuwa Wajumbe wa Bodi kwa kuzingatia uwiano wa jinsia. Kwa mfano, ikiwa bodi itakuwa na wajumbe 10, basi itamlazimu Waziri kuteua wajumbe wasiopungua wanne kutoka jinsia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 8 kinachohusu usimamizi wa taasisi ambapo kifungu cha 8(5) kinamtaka Mkurugenzi Mkuu kutekeleza

majukumu yake kwa kuzingatia maelekezo ya bodi yatakayotolewa mara kwa mara na kuzingatia Sheria ya Taasisi ya Utafiti Tanzania.

Kamati imependekeza muswada uongeze maneno yatakakayomtaka Mkurugenzi Mkuu pamoja na kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maelekezo ya Bodi na Sheria ya Taasisi ya Utafiti, lakini pia iongozwe sheria nyingine za nchi zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu ya pili kipengele (c) muswada unapendekeza kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Ushauri wa Utafiti wa Kilimo. Kipengele hiki kinamtaka Waziri kuteua wajumbe kutoka asasi zinazounda Mfumo wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo, ambapo katika kifungu cha 12(2)(b)(vi) kinataka mwakilishi mmoja kutoka vyama vya wakulima kuwawakilisha wakulima mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza la Taifa la Ushauri wa Utafiti wa kilimo halina idadi maalum ya wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa sheria na kwa kuwa baraza ndiyo chombo chenye nafasi na uwezo wa kuibua, kujadili na kushauri kuhusu changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo na namna ya kutatua changamoto hizo, Kamati imependekeza idadi ya wajumbe wanaowakilisha vyama vya wakulima nchini iongezwe kutoka mkulima mmoja hadi wakulima kumi. Ongezeko linalopendekezwa litasaidia kupunguza idadi ya watawala na kuongeza idadi ya watafiti na hivyo kuongeza tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 12(2)(b)(vii) kinahusu mwakilishi mmoja kutoka vyama vya wafanyabiashara wa mazao ya kilimo. Kamati imependekeza idadi ya wawakilishi wa vyama vya wafanyabiashara iongezwe kutoka mwakilishi mmoja hadi wawili kwa sababu mazao ya kilimo ni mengi na ni muhimu katika kuchangia ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano inahusu masharti ya fedha, Kamati imependekeza kiongezwe kifungu kipya katika sehemu hii kitakachotamka kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo.

Kamati imefikia uamuzi huu kutokana na ukweli kwamba shughuli za utafiti zinahitaji fedha nyingi ambazo uzoefu unaonyesha kuwa fedha zinazopatikana mara nyingi ni fedha za wadau wa maendeleo ambapo fedha hizo hutolewa kulingana na masharti yanayoendana na vipaumbele vyao ambavyo si vipaumbele vya Taifa. Mathalani, sekta ya kilimo inaweza isiwe kipaumbele cha mipango ya fedha za nchi wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine iliyoifanya Kamati kupendekeza sheria iweke hitaji la kuwa na mfuko maalum wa tafiti za kilimo ni kutokana na kutotekelezwa kwa azimio la Serikali la kutenga asilimia moja ya

pato ghafi la Taifa kila mwaka kwa ajili ya kugharamia tafiti, kwani hadi hivi sasa Serikali imeweza kuchangia chini ya asilimia 0.5 ya pato ghafi la Taifa kwenye tafiti. Aidha, fedha kidogo zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya tafiti mbalimbali huelekezwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ambayo hutolewa kwa vigezo vya ushindani ambavyo si lazima vilenge sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu inayohusu majedwali - Jedwali la Tatu. Katika sehemu hii, aya ya (6) kipengele (b) kinachohusu utafiti unaolenga kupunguza upotevu wa bioanuai, Kamati imependekeza maneno "*commercial over exploitation*" yaondolewe kwani kupotea au uharibifu wa *bioanuai* kunatokana na sababu mbalimbali kama vile mfumo wa kilimo unaotumika nchini na shughuli za kilimo katika maeneo ya milimani na kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu hii, Kamati pia imependekeza kuongezeka kipengele (g) kinachohusu tafiti za mabadiliko ya tabia nchi na namna zinavyoathiri sekta ya kilimo na uzalishaji mazao. Kwani kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya mabadiliko ya tabia ya nchi na shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumpongeza Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi Mheshimiwa William Olenasha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa George Masaju, pamoja na Wataalamu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wataalamu kutota Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi na Vituo 16 vya Utafiti ambavyo vinaguswa na sheria inayokusudiwa kutungwa.

Aidha, nachukua fursa hii pia kuwashukuru wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao. Kipekee nawashukuru Ofisi ya Bunge kupitia Kitengo cha Sheria, Chama cha Wanasheria cha Tanganyika, Jumuiko la Vikundi vya Wakulima Tanzania, Baraza la Kilimo Tanzania, Taasisi ya Utafiti ya viuatilifu vya Kitropiki, Taasisi ya Utafiti ya Kahawa, Taasisi ya Utafiti ya Chai na Taasisi ya Utafiti ya Tumbaku ambao michango yao ya kitaalam imeisaidia Kamati kuboresha muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kuchambua kikamilifu maoni yaliyowasilishwa na wadau na hivyo kuwawezesha kuchambua muswada kwa kina na hatimaye kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini sio kwa umuhimu,napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah pamoja na Makatibu wa Kamati Ndugu Virgil Mtui, Ndugu Martha Chassama na Ndugu Rachel

Nyega na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hii na kuandaa kikamilifu taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii na kukushukuru wewe Mwenyekiti, ahsanteni sana Bunge zima. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO YA MWAKA, 2016(*THE TANZANIA AGRICULTURAL RESEARCH INSTITUTE BILL*, 2016)**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Mwaka, 2016 (*The Tanzania Agricultural Research Institute Bill*, 2016).

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kupokea Muswada wa Sheria, Kamati ilitoa mwaliko kwa wadau mbalimbali kupitia vyombo vya habari, kwa kuwatumia barua na nakala ya Muswada kwa njia ya posta na kwa kutumia barua pepe. Wajibu huu ulitekelezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Mwaliko uliotolewa ulikusudia kuwapa wadau fursa ya kutoa maoni yao kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya sheria inayokusudiwa kutungwa na hatimaye kuisaidia Kamati kufanya uchambuzi wa kina wa muswada tajwa.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa muswada watendaji wakuu wa Vituo kumi na sita (16) vya utafiti wa kilimo, taasisi mbalimbali za Serikali na mashirika yasiyo ya Serikali ambayo Muswada wa Sheria inayopendekezwa unawagusa walihudhuria vikao vya Kamati ili kutoa michango yao kwa njia ya majadiliano na kwa maandishi. Aidha, Chama cha Wanasheria Tanganyika (*Tanyanyika Law Society*) na Muungano wa vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) walifika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao.

**Mheshimiwa Spika**, mnano tarehe 23 Agosti, 2016, Kamati ilikutana na Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi katika Ukumbi wa *Mount Meru* ulioko jengo la Hazina *Square*, Dodoma kwa lengo la kupokea maelezo ya Serikali kuhusu Muswada husika. Aidha, terehe 01 Septemba, 2016 Kamati ilifanya kikao cha mashauriano na Wizara kuhusu marekebisho ya Muswada husika.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kukutana na kupata maoni ya wadau mbalimbali, iliendelea kukutana na Watendaji wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi, wawakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na

wawakilishi wa Mshauri wa Sheria kutoka Ofisi ya Bunge kwa lengo la kubadilishana mawazo na kupata uelewa mpana kuhusu maudhui ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** katika maelezo yake, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi aliieleza Kamati kuwa Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo wa Mwaka, 2016 (*The Tanzania Agricultural Research Institute Bill*, 2016) unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, 2016 (*Tanzania Agricultural Research Institute Act*, 2016).

**Mheshimiwa Spika,** lengo la Sheria inayopedekezwa kutungwa ni kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa kilimo ambayo, pamoja na mambo mengine, itakuwa na jukumu la kufanya na kusimamia tafiti zote za kilimo Tanzania bara. Aidha, katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa Muswada huu una sehemu sita (6) na jumla ya vifungu thelathini na nane (38) na kwa ukamilifu unasomeka kuwa ni Muswada wa Sheria wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo wa Mwaka, 2016.

## 2.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo, sasa ninaomba niwasilishe maoni na ushauri wa Kamati kuhusu muswada huu. Maoni haya kwa kiasi kikubwa yametokana na uchambuzi wa Kamati na maoni ya wadau mbalimbali pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Serikali. Hata hivyo, kabla ya kuanza kuwasilisha maoni ya Kamati ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, jedwali la marekebisho mlilopewa, ni matokeo ya Uchambuzi wa Muswada iliyofanywa na Kamati kutokana na Muswada wenyewe na maoni ya wadau.

**Mheshimiwa Spika**, hoja zote zilizoibuliwa na Kamati kuhusu marekebisho ya muswada huu zilikubaliwa na Serikali na kuhitimishwa kama zinavyoonekana kwenye kiambatanisho ambacho ni Jedwali la Uchambuzi wa Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo haya ambayo muktadha wake unapatikana katika sehemu ya Muswada ijulikanayo kama madhumuni na sababu *(objects and reasons) yanalenga* kuwezesha yafuatayo kutokea:-

(i) Kuongezeka kwa uzalishaji, upatikanaji na matumizi ya teknolojia sahihi za kuendeleza kilimo kulingana na mahitaji ya soko;

(ii) Kuongezeka kwa ufanisi wa shughuli za utafiti wa kilimo hapa nchini;

(iii) Kuimarika kwa matumizi sahihi ya rasilimali za utafiti kwa kulenga katika vipaumbele vya sekta na kuondoa hali ambayo taasisi zaidi ya moja kurudia kufanya utafiti uliokwishafanywa;

(iv) Kuwepo mfumo madhubuti wa kusimamia shughuli za utafiti wa kilimo nchini ikilinganishwa na mfumo uliopo sasa;

(v) Kuimarika kwa ushirikiano kati ya taasisi, mashirika na wadau wengine wanaoshughulika na utafiti wa kilimo ndani na nje ya nchi; na

(vi) Kuimarika kwa mnyororo wa thamani kutokana na utafiti utakaofanywa kulingana na mahitaji ya kila zao ili kuongeza tija na kipato cha wakulima na hivyo kuongeza mchango wa sekta ya kilimo katika uchumi na usalama wa chakula na lishe

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono madhumuni na sababu (*objects and reasons*) ya Serikali kuhusu muswada huu kwani yanalenga kuweka mfumo mahsusi wa utafiti utakaowezesha uzalishaji, upatikanaji na usambazaji wa teknolojia sahihi za mazao nchini na kujenga uwezo wa wataalam na miundombinu ya utafiti.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na madhumuni na sababu ya Serikali kuleta Muswada huu Bungeni, Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013 imeelekeza kuanzishwa kwa Chombo cha kuratibu na kusimamia utafiti nchini. Kwa mujibu wa Waziri wa Kilimo, Mifugo na maendeleo ya Uvuvi kutokuwepo kwa Chombo hiki chenye mamlaka ya kisheria cha kuratibu na kusimamia utafiti wa kilimo kumesababisha kutokuwepo uratibu na usimamizi mzuri wa utafiti na rasilimali zake. Vilevile kutokuwepo na mfumo wa kufanya maamuzi kwa wakati muafaka na athari zake ni pamoja na kutokuwepo ufanisi na utafiti endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata nafasi ya kutathimini uzoefu wa taasisi za nchi zingine kama *Kenya Agricultural Research Institute* (*KARI*), National *Agricultural Research Organization* (*NARO*) ya Uganda, Rwanda *Agricultural Board* (*RAB*), *Ethiopian Institute of Agricultural Research* (*EIAR*), *Brazilian Agricultural Research Corporation* (*EMBRAPA*) na *Indian Agricultural Research Council* (*IARC*) na kubaini kuwa miundo ya Taasisi hizo imeziwezesha kuwa na utaratibu mzuri na wenye ufanisi. Na kwamba, miundo hiyo imewezesha kuwepo utaratibu mzuri wa kufikisha matokeo ya utafiti kwa walengwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muktadha huu, Kamati inaona ni wakati muafaka sasa kwa nchi yetu kuwa na sheria hii ambayo itawezesha kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Taasisi ambayo itakuwa chombo huru cha kusimamia na kuratibu utafiti wa kilimo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kuunga mkono mapendekezo ya Sheria inayokusudiwa kutungwa, yapo mambo kadhaa ambayo yaliibua wasiwasi kwa Wajumbe wa Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada na hivyo kuhitaji ufafanuzi wa kina kutoka kwa Serikali. Mambo hayo ni pamoja na:-

Sheria Na 7 ya mwaka 1986 iliyoanzisha Tume ya Sayansi na Teknolojia, ambayo imeweka sharti la kuelekeza fedha zote za tafiti katika mfuko wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH). Wajumbe walitaka kufahamu kama fedha za tafiti katika sekta ya kilimo zitaelekezwa katika mfuko huo, na nini athari zake katika ufanisi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI).

Wajumbe walitaka kufahamu utaratibu utakaotumika kwa Taasisi zingine za Elimu ya Juu zinazofanya tafiti za maswala ya Kilimo.

Kwa kawaida mahala pengi duniani sekta ya kilimo inajumuisha mazao yatokanayo na kilimo, mifugo na uvuvi, kwa muktadha huo, Wajumbe walitaka kufahamu kwanini Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo inayokusudiwa kutungwa haijajumuisha sekta za mifugo na uvuvi.

Wajumbe walitaka kufahamu utaratibu utakaotumika kuhakikisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya tafiti za kilimo.

Wajumbe walitaka kujiridhisha endapo sheria inayoanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania haitaongeza ukiritimba katika utafiti? Wasiwasi wa Wajumbe ulitokana na baadhi ya majukumu yaliyotajwa kwenye sheria yanatekelezwa pia na Taasisi zingine za utafiti kwa mfano; Tume ya Sayansi na Teknolojia ina jukumu la kuratibu shughuli zote za utafiti nchini ikiwa ni pamoja na kilimo. Lakini pia Taasisi ya Tathmini za Rasilimali ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam (*Institute of Resource Assessment* -IRA) inafanya tafiti zilizoainishwa kwenye Jedwali la Tatu Kipengele 6 (a, b, na c).

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, Kamati ilifanya kikao cha majumuhisho na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi ambapo Waziri alitoa ufafanuzi wa hoja zote zilizoibuliwa na kufikia mhafaka.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 3.1 SEHEMU YA KWANZA YA MUSWADA INAYOHUSU MASHARTI YA UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** katika sehemu hii ya kwanza, Kamati ilitoa maoni na mapendekezo kwenye maeneo kadhaa yaliyohusu:-

Mipaka ya Sheria inayokusudiwa kutungwa;

Kuongeza na kufuta baadhi ya maneno ambayo tafsiri ya maneno hayo ilileta mkanganyiko;

Kuongezwa kwa vifungu vipya na

Kusahihisha makosa ya kiuchapaji.

## 3.2 SEHEMU YA PILI YA MUSWADA INAHUSU UANZISHWAJI NA USIMAMIZI WA TAASISI

**Mheshimiwa Spika,** katika sehemu hii Kamati ilipendekeza kuongezwa kwa kifungu kipya kitakachobainisha ukuu/ mamlaka ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, kubadilisha baadhi ya maneno ambayo tafsiri yake ilileta mkanganyiko na kurekebisha baadhi ya makosa ya kiuchapaji**.**

**Mheshimiwa Spika,** katika sehemu hii pia kulikuwa na marekebisho yaliyotaka uwakilishi wa Makamu Mkuu wa Chuo kikuu cha kilimo kwenye muundo wa Bodi ya Taasisi uzingatie weledi wa chuo husika na sio kama ilivyopendekezwa kwenye Muswada katika kifungu cha 5(2)(ii) kwamba Makamu Mkuu wa Chuo atakayeteuliwa kutoka katika moja ya vyuo vikuu vya kilimo**.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imetoa mapendekezo katika kifungu cha 5(2) (vii) ambacho kinatoa nafasi ya mkulima mmoja kuwakilisha wakulima wote kwenye wajumbe wa Bodi ya Taasisi. Kamati imependekeza idadi ya namba ya wakulima watakaowakilisha kwenye Bodi iongezwe na kufikia wakulima wawili kwa sababu Bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania pamoja na kazi zingine, ina jukumu la kumshauri Waziri kuhusu uanzishwaji wa vituo vya utafiti au vituo vidogo vya utafiti ambavyo vitaongeza tija katika kilimo na kupunguza umaskini kwa watanzania ambao wengi wao ni wakulima, hivyo uwakilishi wa kutosha ni muhimu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo, ni muhimu suala la idadi ya uwakilishi wa wakulima kwenye Bodi ya Taasisi likazingatiwa kwa uzito unaostahili kwa sababu Muswada ulipendekeza uwakilishi wa mkulima mmoja ambapo Kamati inaamini uwakilishi wa mkulima mmoja haukidhi kuwakilisha wakulima wengi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kifungu cha 5(3) Muswada unamtaka Waziri kuteua wajumbe wa Bodi kwa kuzingatia taaluma, uzoefu na jinsia. Katika kifungu hiki, Kamati imependekeza Sheria imtake Waziri kwa upande wa jinsia kuteuwa Wajumbe wa Bodi kwa kuzingatia uwiano wa jinsia. Kwa mfano, ikiwa Bodi itakuwa na Wajumbe 10, basi itamlazimu Waziri kuteua Wajumbe wasiopungua wanne kutoka jinsia moja.

**Mheshimiwa Spika,** katika kifungu cha (8) kinachohusu Usimamizi wa Taasisi, ambapo kifungu cha 8(5) kinamtaka Mkurugenzi Mkuu kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maelekezo ya Bodi yatakayotolewa mara kwa mara na kuzingatia Sheria ya Taasisi ya Utafiti Tanzania. Kamati imependekeza Muswada uongeze maneno yatakakayo mtaka Mkurugenzi Mkuu pamoja na kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maelekezo ya Bodi na Sheria ya Taasisi ya Utafiti lakini pia iongozwe na Sheria zingine za nchi zilizopo.

**Mheshimiwa Spika**, katika sehemu ya pili kipengele "c" Muswada unapendekeza kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Ushauri wa Utafiti wa Kilimo. Kipengele hiki kinamtaka Waziri kuteua Wajumbe kutoka asasi zinazounda Mfumo wa Taifa wa utafiti wa kilimo, ambapo katika kifungu cha 12(2) (b) (vi) kinataka mwakilishi mmoja kutoka vyama vya wakulima kuwakilisha wakulima mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Baraza la Taifa la ushauri wa utafiti wa kilimo halina idadi maalum ya Wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa sheria na kwa kuwa baraza ndio chombo chenye nafasi na uwezo wa kuibua, kujadili na kushauri changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo na namna ya kutatua changamoto hizo, Kamati imependekeza idadi ya wajumbe wanaowakilisha vyama vya wakulima nchini iongezwe kutoka mkulima mmoja (1) hadi wakulima kumi (10). Ongezeko linalopendekezwa litasaidia kupunguza idadi ya watawala na kuongeza idadi ya watafiti na hivyo kuongeza tija.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu 12 (2) (b) (vii) kinahusu mwakilishi mmoja kutoka vyama vya wafanyabiashara wa mazao ya kilimo. Kamati imependekeza idadi ya wawakilishi wa vyama vya wafanyabiashara iongezwe kutoka mwakilishi mmoja (1) hadi wawili (2) kwa sababu mazao ya kilimo ni mengi na ni muhimu katika kuchangia ukuaji wa uchumi.

### 3.3 SEHEMU YA TANO INAHUSU MASHARTI YA FEDHA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imependekeza kiongezwe kifungu kipya katika sehemu hii kitakachoeleza kuanzishwa kwa mfuko wa Taifa wa utafiti wa kilimo. Kamati imefikia uamuzi huu kutokana na ukweli kwamba shughuli za utafiti zinahitaji fedha nyingi ambazo uzoefu unaonyesha kuwa, fedha zinazopatikana mara nyingi ni fedha za wadau wa maendeleo ambapo fedha hizo hutolewa kulingana na masharti yanayoendana na vipaumbele vyao ambavyo si vipaumbele vya Taifa. Mathalani, sekta ya kilimo inaweza isiwe kipaumbele cha mipango ya fedha za nchi wahisani.

**Mheshimiwa Spika,** sababu nyingine iliyoifanya Kamati kupendekeza sheria iweke hitaji la kuwa na mfuko maalum wa tafiti za kilimo ni kutokana na kutotekelezwa kwa azimio la Serikali la kutenga **asilimia 1%** ya pato ghafi la Taifa kila mwaka kwa ajili ya kugharamia tafiti, kwani hadi hivi sasa Serikali imeweza kuchangia chini ya **asilimia 0.5** ya pato ghafi la Taifa kwenye tafiti. Aidha, fedha kidogo zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya tafiti mbalimbali huelekezwa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ambayo hutolewa kwa vigezo vya ushindani ambavyo si lazima vilenge sekta ya kilimo.

## 3.4 SEHEMU INAYOHUSU MAJEDWALI - JEDWALI LA TATU

**Mheshimiwa Spika,** katika sehemu hii, aya ya sita (6) kipengele (b) kinachohusu utafiti unaolenga kupunguza upotevu wa bioanuai, Kamati imependekeza maneno "***commercial over exploitation***" yaondolewe kwani kupotea au uharibifu wa bioanuai kunatokana na sababu mbalimbali kama vile mfumo wa kilimo unaotumika nchini na shughuli za kilimo katika maeneo ya milimani na kwenye vyanzo vya maji**.**

**Mheshimiwa Spika,** katika sehemu hii, Kamati pia imependekeza kuongeza kipengele (g) kinachohusu tafiti za mabadiliko ya tabia nchi na namna zinavyoathiri sekta ya kilimo na uzalishaji mazao. Kwani kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya mabadiliko ya tabia ya nchi na shughuli za kilimo.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumpongeza Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi Mhe. Dkt. Charles Tizeba (Mb), Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi Mhe. William T. Olenasha (Mb), Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. George W. Masaju (Mb), pamoja na wataalamu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wataalamu kutota Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi na Vituo 16 vya Utafiti ambavyo wanaguswa na sheria inayokusudiwa kutungwa.

Aidha, nachukua fursa hii pia kuwashukuru wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao. Kipekee nawashukuru Ofisi ya Bunge kupitia kitengo cha Sheria, Chama cha Wanasheria cha Tanganyika (TLS), Jumuiko la Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), Baraza la Kilimo Tanzania (ACT), Taasisi ya Utafiti ya Viuatilifu vya Kitropiki (TPRI), Taasisi ya Utafiti ya Kahawa (TaCRI), Taasisi ya Utafiti ya Chai (TRIT) na Taasisi ya Utafiti ya Tumbaku (TORITA) ambao michango yao ya kitaalam imeisaidia Kamati kuboresha Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kuchambua kikamilifu maoni yaliyowasilishwa na wadau na hivyo kuwawezesha kuchambua Muswada kwa kina na hatimaye kukamilisha taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na taadhima, naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt.Mary Michael Nagu, Mb -Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb – M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Emmanuel P. John, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Philipo A. Mulugo, Mb "

| | |
|---|---|
| 5. Mhe. Dkt. Immaculate S. Semesi, Mb | " |
| 6. Mhe. Mahmoud H. Mgimwa, Mb | " |
| 7. Mhe. Salum M. Rehani | " |
| 8. Mhe. Khadija H. Aboud, Mb | " |
| 9. Mhe. Kunti Y. Majala, Mb | " |
| 10. Mhe. Marwa R. Chacha, Mb | " |
| 11. Mhe. Mashimba M. Ndaki, Mb | " |
| 12. Mhe. Oliver D. Semuguruka, Mb | " |
| 13. Mhe. John J. Mnyika, Mb | " |
| 14. Mhe. Hamidu H. Bobali, Mb | " |
| 15. Mhe. James K. Millya, Mb | " |
| 16. Mhe. Njalu D. Silanga, Mb | " |
| 17. Mhe. Pascal Y. Haonga, Mb | " |
| 18. Mhe. Salim M. Bawazir, Mb | " |
| 19. Mhe. Deo K. Sanga, Mb | " |
| 20. Mhe. Abdallah H. Ulega, Mb | " |
| 21. Mhe. Daniel N. Nsazugwako, Mb | " |
| 22. Mhe. Upendo F. Peneza, Mb | " |
| 23. Mhe. Haji A. Haji, Mb | " |

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu,napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah pamoja na makatibu wa Kamati Ndg. Virgil Mtui, Ndg. Martha Chassama na Ndg. Rachel Nyega na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Mary M. Nagu (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**
14 Septemba, 2016

**MWENYEKITI:** Ahsante, sasa namuita Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI – NAIBU MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Msemaji wa Kambi rasmi ya Upinzai, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, napenda kuwasilisha maoni kuhusu Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania kwa mwaka 2016 chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni ya Kudumu za Bunge 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na unyenyekevu naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili na kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, juu ya Muswada tajwa ulio mbele yetu.

Aidha, nitoe shukrani zangu kwa ushirikiano wa hali ya juu wa Kiongozi wa Upinzani Bungeni pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote ambao kwa njia moja ama nyingine wamekuwa ni sehemu ya maoni haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki kama nitashindwa kutambua mchango mkubwa wa Sekretarieti ya Kambi Rasmi ya Upinzani katika maandalizi na uchambuzi uliomo katika wasilisho hili la Kambi. Mwisho lakini sio kwa umuhimu ni kwa Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi juu ya uchambuzi wake kwa kifungu cha 3(3), 3(4) na 3(5) kama ambavyo kimenakiliwa kilivyo kutoka kwenye Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya muswada, muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti ya Kilimo Tanzania, lengo la sheria inayopendekezwa kutungwa ni kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ambayo pamoja na mambo mengine itakuwa na jukumu la kufanya na kusimamia tafiti zote za kilimo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 3(2) kinachosema kuwa; "Taasisi itakuwa ni taasisi hodhi na itakuwa na (b) jina lake la biashara na uwezo wa kushtaki na kushtakiwa." Kwa maana halisi ya kifungu cha 3(2)(b) ni kwamba kama chombo au mtu yeyote mwenye kuona kuwa hakutendewa haki na taasisi hii au taasisi yoyote binafsi itaona kuwa haikutendewa haki na chombo chochote inaweza kushtakiwa na kushtaki ili haki ipatikane kwa njia ya mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu vidogo vya 3(3), 3(4) na 3(5) kimaudhui vinamtaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia kati katika hatua yoyote ya shauri linalolihusu taasisi, iwe imeshtaki au imeshtakiwa na pia masharti ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri dhidi ya Serikali katika Sura ya Tano itatumika kama vile suala hilo limefunguliwa na Serikali au dhidi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge ambao hawakuwepo katika Bunge la Kumi, naomba kunukuu sehemu ya taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Katiba na Sheria aliyoiwasilishwa Bungeni wakati Bunge linapitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za mwaka 2014 kwani maudhui ya kifungu cha 3(3), 3(4) na 3(5) vimenukuliwa kama vilivyo kutoka kwenye sheria

iliyopitishwa mwaka 2014. Ninanukuu baadhi ya kilichotajwa awali; "Mwanasheria Mkuu ana uwezo kisheria wa kupata taarifa yoyote ile kutoka kwa afisa yeyote yule wa umma kuhusu shauri au jambo lolote lile lililopo katika mahakama yoyote ile au linalohitaji ushauri wowote ule wa kisheria."

Swali la wazi linalohitaji kuulizwa na kujibiwa kwa ukweli na ufasaha ni je, kwa nini muswada huu umeletwa mbele ya Bunge lako Tukufu? Je, lengo hasa la mapendekezo haya ni lipi? Na je, kupitishwa kwa muswada huu kama Bunge lako Tukufu linavyoombwa kufanya kutakuwa na athari gani kwa nchi yetu na kwa wananchi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la jumla la maswali yote haya ni kwamba Serikali hii ya CCM inataka kusiwe na uwezekano wowote ule wa mtu yeyote yule, ama Shirika, Taasisi au Kampuni yoyote ile binafsi ya kupata haki endapo Serikali au Taasisi na Mashirika yake yote yaliyotajwa kwenye muswada huu yatashitakiwa mahakamani na kushindwa kesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuthibitisha ukweli wa kauli hii ni muhimu kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kuelewa maana halisi ya maneno yaliyoko kwenye aya mbalimbali za muswada huu kwamba pale ambapo Mwanasheria Mkuu anaingilia jambo lolote basi masharti ya sheria ya Mshauri wa Serikali yatatumika kuhusiana na mashauri au jambo hilo kana kwamba yamefunguliwa na au dhidi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema ikaeleweka vizuri kuwa mtu wa leo sio wa kesho kutokana na anavyo-*approach issues*, hivyo kama sheria zilizotungwa miaka ya 1990 zilikosewa au mazingira ya wakati huo ilikuwa sahihi, lakini sheria hizo hizo kwa miaka hii sio sahihi ni kwa nini mfumo wa uandishi wa sheria zetu ubaki kuwa ule ule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema hivyo kutokana na ukweli kwamba sheria inayotungwa au karne hii ya sayansi na teknolojia hakuna ulazima wowote Wenyeviti wa Bodi au Watendaji Wakuu kuteuliwa na Rais, ni dhahiri kuendelea kukumbatia dhana hiyo ya uteuzi kuwa ni mamlaka ya Rais ni kuwafanya watendaji kukosa ubunifu na badala yake kuendelea kucheza ngoma inayopigwa na Rais. *(Makofi)*

Kwa muktadha huo Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa kifungu cha 5(a) cha uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi iwe Mwenyekiti wa Bodi atateuliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Bodi na nafasi ya Mtendaji Mkuu wa Taasisi ishindaniwe kwa sifa zilizoainishwa na kifungu cha 8(2) na ikilazimu vigezo viongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 5(2)(b) kinahusu Wajumbe tisa wa Bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania watakaoteuliwa na Waziri. Kwa kuwa taasisi hii ya utafiti wa kilimo pamoja na mambo mengine itakuwa na jukumu la kusimamia tafiti zote za kilimo Tanzania bila ya kubagua kuwa zinafanywa na watafiti toka taasisi binafsi au wa taasisi za Serikali. Lakini kati ya wateule tisa wa Waziri, Wajumbe sita ni watendaji wa Serikali na mmoja inasema ni Mtendaji Mkuu atakayewakilishwa kutoka taasisi binafsi za utafiti wa kilimo. Kwa maana hiyo Wajumbe zaidi ya wale waajiriwa wa Serikali ni wawili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa utafiti kwenye kilimo unaweza kuwa ni sehemu ya kilimo cha kibiashara kwa wakulima wakubwa kama ambao wanasemwa kwenye Mpango wa *SAGCOT* kuwa na vituo vya vya utafiti kwa kadri ya mahitaji yao ni jambo la kawaida kabisa. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa, badala ya kuwajaza Watendaji wa Serikali kwenye bodi ni bora tuangalie ni upande upi utakaoleta tija zaidi kwa maendeleo ya Taifa letu. Hivyo basi, kuwa na wajumbe toka sekta binafsi ni suala la muhimu sana. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupewa tafsiri ya kifungu kidogo cha 5(2)(b)(iii). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 7 kinachohusu posho kwa Wajumbe wa Bodi, kifungu kinapendekeza Wajumbe walipwe posho zitakazoainishwa na Waziri mara baada ya kupendekezwa na Bodi. Kama ambavyo Kambi Rasmi imekuwa ikishauri kwamba posho za Wajumbe wa Bodi pendekezo lisitoke kwa wajumbe wenyewe bali viwango vya posho kwa Wajumbe wa Bodi zipangwe na ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Ofisi inayohusika na utumishi wa umma. Kambi Rasmi inasema hili kutokana na uzoefu wa bodi za taasisi kadhaa ambapo Wajumbe wa Bodi wanajilipa posho za vikao ambayo kwa hali halisi ya Tanzania haiwezekani na bodi inapanga vikao vyake vifanyike sehemu ambazo ni ghali sana wakati huo posho zao za vikao ziko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa lengo la sheria ni ujenzi wa taasisi za kiutendaji kuwa imara katika mfumo mzima wa uendeshaji wa nchi, hivyo basi, kifungu cha 8(1) kinachosema kuwa Mtendaji Mkuu wa Taasisi atateuliwa na Rais baada ya kupata ushauri wa Waziri kutoka miongoni mwa watu wenye sifa na uzoefu. Aidha, kifungu cha 8(2) kimeorodhesha sifa zinazohitajika kwa kazi hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikisemea utaratibu huu wa uteuzi ambao unawafanya wateuliwa kuwa ni hisani ya waliowateua badala ya kuona kwamba wanastahili kazi hizo na jambo hilo limepelekea wateuliwa kutokufanyakazi kwa mujibu wa taaluma zao na matakwa ya kazi zao na badala yake wamekuwa wanatekeleza matakwa ya mamlaka za uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuwa ili utumishi wa umma uwe imara yaani *strong civil service* ni lazima ajira za

utendaji zipitie kwenye mfumo ambao hautakuwa na ushawishi wa mtu yeyote wala upendeleo wa aina yoyote. Vinginevyo thamani ya taaluma itaendelea kudharauliwa kutokana na ushauri wao wa kitaaluma kutoheshimika mbele za watawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 9 cha muswada kinaipa bodi uwezo wa kuanzisha idadi yoyote ya Idara na Vitengo chini ya taasisi kwa kuzingatia muundo wa Taasisi ilioidhinishwa, naomba ninukuu kifungu husika. Nanukuu kama ifuatavyo; "9(1) *for the proper discharge of the functions of the Institute under this Act, the Board shall establish such number of departments and units under the Institute in accordance with the approved organizational structure.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kujua huo muundo utaidhinishwa na nani? Wakati huo hapo awali Bodi imepewa nguvu ya kuanzisha Idara na Vitengo kwa kadri itakavyoona inafaa. Kwa kutoa mwanya huu katika sheria, kuna uwezekano mkubwa kwa idara hata ambazo hazitokuwa na mahitaji zikaanzishwa kwa lengo la kutoa ajira kwa watu wa aina fulani. Hii ni hatari kwa sheria kuacha mwanya huu bila kuzibwa, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini Idara Kuu ya Utumishi ndio chombo mwafaka cha kuangalia miundo ya Idara na Vitengo vinavyohitajika kwa taasisi na wakala mbalimbali wa Serikali, vinginevyo ni kwa maelekezo maalum toka kwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 10(1) kinahusu ajira za watumishi wa taasisi, na kifungu kinasema kwamba na nanukuu; *"The Institute shall, with approval of the Board, appoint or recruit on competitive basis such other staff."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaliona hili jambo la Taasisi kupewa uwezo wa kuteua watumishi ama wafanyakazi baada ya bodi kuwa tayari imeunda Idara na vitengo sio busara na hapa ndipo mambo ya *nepotism* yatakapojitokeza. Pia hakuna kitu kama uteuzi wa ushindani, hivyo basi Kambi inashauri maneno "*appoint or*" yafutwe ili sheria iwe chombo cha kutenda haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 10(2) kinasema kuhusiana na kipindi cha utendaji kazi kwa waajiriwa wa taasisi kuwa itakuwa ni bodi kuamua ni muda gani watendaji hao wafanye kazi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona itakuwa vyema kama ambavyo sheria imeweka muda wa Bodi kuhudumu na muda wa Mtendaji Mkuu kuhudmu, vivyo hivyo muda wa watendaji kuhudumu ungewekwa wazi ili kuondoa tabia iliyopo ya watendaji kuzeekea kwenye viti jambo ambalo lilionekana kuwa ofisi ni mali binafsi za watendaji na jambo hili linawanyima fursa watu wengine kufanyakazi katika taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 11(2) kinasema kuwa, na-*quote; "the research centres shall be headed by a director who shall be appointed by the Board."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina wataalam wengi sana katika fani ya kilimo na wengine bado wanaendelea kufuzu kutoka vyuo vya ndani na vya nje. Kambi Rasmi ya Upinzani inapingana na dhana ya uteuzi kwani inaua kabisa dhana ya ushindani wa wazi, jambo hili linazidisha kile kinachoitwa kuwajibika kwa mtu badala ya kuwajibika kwa majukumu ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ili kuleta ushindani kwa wale wote wenye sifa ni vyema kuendesha mchakato wa wazi wa watu kuomba na kufanyiwa usahili kwa kazi husika, badala ya uteuzi ambapo watu wale wale wamekuwa wanazunguka kutoka kituo kimoja kwenda kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 35(3) cha muswada kinahusu rufaa kwa kusema kuwa, na-quote; *"The decision by the Minister shall be final."* Kifungu hiki kwa mantiki yake kinapingana na kifungu cha 3(2)(b), 3(3), 3(4) na 3(5). Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, kama vifungu hivyo vinatoa nafasi kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia mashauri yoyote ambayo taasisi itakuwa imeshtaki au kushtakiwa, inakuwaje kifungu cha 35(3) kinasema kuwa uamuzi wa Waziri utakuwa ni wa mwisho? Na haioneshi kuwa utaratibu wa kimahakama unapewa nafasi yoyote ili wahusika wapate haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi huo wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye vifungu ambavyo nimevionesha hapo awali naomba kuwasilisha, ahsante. *(Makofi)*

**MAONI YA MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI MHESHIMIWA MAGDALENA HAMISI SAKAYA (MB), KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA, WA MWAKA 2016 (Tanzania Agricultural Research Institute Act, 2016) KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016)*

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa heshima kubwa na unyenyekevu naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili na kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, juu ya muswada tajwa ulio mbele yetu. Aidha, nitoe shukrani zangu kwa ushirikiano wa hali ya juu wa Kiongozi wa Upinzani Bungeni pamoja na waheshimiwa wabunge wote ambao

kwa njia moja ama nyingine wamekuwa ni sehemu ya maoni haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

**Mheshimiwa Spika,**
Nitakuwa sijatenda haki kama nitashindwa kutambua mchango mkubwa wa Sekretariet ya Kambi Rasmi ya Upinzani katika maandalizi na uchambuzi uliomo katika wasilisho hili la Kambi. Mwisho lakini sio kwa umuhimu ni kwa Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi juu ya uchambuzi wake kwa kifungu cha 3(3), 3(4) na 3(5) kama ambavyo kimenakiliwa kilivyo **(copy and paste)** kutoka kwenye sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali ya mwaka 2014.

## 2. MAPITIO YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,**
Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti ya Kilimo Tanzania, lengo la sheria inayopendekezwa kutungwa ni ya kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ambayo, pamoja na mambo mengine itakuwa na jukumu la kufanya na kusimamia tafiti zote za kilimo Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,**
Kifungu cha 3(2) kinachosema kuwa ***"Taasisi itakuwa ni taasisi hodhi na itakuwa na,(b) jina lake la biashara na uwezo wa kushtaki na kushtakiwa";***

Kwa maana halisi ya kifungu cha 3(2)(b) ni kwamba kama chombo au mtu yeyote mwenye kuona kuwa hakutendewa haki na taasisi hii au taasisi yoyote binafsi itaona kuwa haikutendewa haki na chombo chochote inaweza kushtakiwa na kushtaki ili haki ipatikane kwa njia ya Mahakama.

**Mheshimiwa Spika,**
Vifungu vidogo vya 3(3), 3(4) na 3(5) kimaudhui vinamtaka Mwanasheria mkuu wa Serikali kuingilia kati katika hatua yoyote ya shauri linaloihusu taasisi, iwe imeshtaki au imeshtakiwa, na pia masharti ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri dhidi ya Serikali (Sura ya 5) itatumika kama vile suala hilo limefunguliwa na Serikali au dhidi ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa faida ya waheshimiwa wabunge ambao hawakuwepo katika Bunge la 10, naomba kunukuu sehemu ya taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Wizara ya Katiba na Sheria aliyoiwasilisha Bungeni wakati Bunge linapitisha Muswada wa sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali wa mwaka 2014. Kwani mahudhui ya kifungu cha 3(3), 3(4) na 3(5) vimenukuliwa kama vilivyo kutoka kwenye sheria iliyopitishwa mwaka 2014;

Ninanukuu

"Mheshimiwa Spika,
Katika hotuba yake ya awali ya kuwasilisha Muswada huu, na ambayo nakala yake aliigawia wajumbe wa Kamati, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu alisema kwamba marekebisho haya "*yanalenga kulinda maslahi ya Serikali kwenye mashauri yanayofunguliwa na au dhidi ya mashirika na taasisi za umma kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kushiriki kwenye shauri husika katika hatua za awali.*" Aidha, inaelezwa - katika 'Madhumuni na Sababu' za Muswada huu - kuwa maudhui ya marekebisho yaliyokuwa yanapendekezwa "*... ni kuweka masharti yanayomuwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia kati, katika hatua yoyote, shauri lolote lililopo mahakamani dhidi ya shirika au taasisi yoyote iliyoanzishwa na sheria.*"

**Mheshimiwa Spika,**
Hizi hazikuwa sababu sahihi au za kweli za kuhalalisha Muswada huu kuletwa kwenye Bunge lako tukufu sio. Kwanza, tayari – kwa sheria zilizopo sasa hivi – Mwanasheria Mkuu anayo mamlaka kamili ya kuingilia kati, katika hatua yoyote, shauri lolote lililopo mahakamani linaloihusu serikali, idara zake, mashirika au taasisi zake au linalohusu watu binafsi kabisa.

Kwa mujibu wa kifungu cha 6(a) cha *Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya 2005*, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa ibara ya 59(3) ya *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977*, Mwanasheria Mkuu atakuwa na atatekeleza mamlaka ya "*... kuingilia kati katika hatua yoyote ya mashauri yoyote, rufaa yoyote, kukaza hukumu yoyote au katika mashauri yanayohusiana nayo katika mahakama yoyote au baraza lolote ambapo haki ya Mwanasheria Mkuu kusikilizwa imezuiliwa na sheria.*"
'*Incidental proceedings*' zilizotajwa katika kifungu hiki ni pamoja na maombi (*applications*), marejeo (*revisions*), mapitio (*review*), rejea (*reference*) au mashauri ya gharama za mashauri (*taxation proceedings*) yanayotokana na mashauri, rufaa au taratibu za kukaza hukumu katika mashauri mbali mbali yanayoihusu au yasiyoihusu Serikali katika mahakama zetu zote na mabaraza mbali mbali yenye hadhi ya kimahakama. Kwa maana hiyo, Mwanasheria Mkuu ana mamlaka - kwa Sheria ya sasa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yake – kufanya mambo yote ambayo Bunge lako tukufu linaombwa kumpatia kwa kupitisha Muswada huu.

Cha zaidi, Mheshimiwa Spika, ni kwamba Mwanasheria Mkuu amekuwa na mamlaka hayo tangu mwaka 2005 na - kwa ushahidi uliotolewa mbele ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge lako tukufu na wadau mbali mbali – hajawahi kuyatumia katika kesi au mashauri yanayohusu mashirika au taasisi za umma zilizotajwa katika Muswada huu. Kila mwakilishi wa mashirika au taasisi za umma tajwa aliyetoa maelezo yake mbele ya Kamati aliiambia

Kamati kwamba, licha ya kuwa na mamlaka hayo kwa mujibu wa Sheria inayofafanua utaratibu wa utekelezaji wa mamlaka yake kikatiba, Mwanasheria Mkuu hajawahi kuingilia kati mashauri yoyote katika hatua yoyote yanayofunguliwa na au dhidi ya mashirika au taasisi husika.

Kwa maana nyingine, Mheshimiwa Spika, Bunge lako tukufu lilikuwa linaombwa kupitisha Muswada utakaompatia Mwanasheria Mkuu mamlaka ambayo tayari anayo kwa zaidi ya miaka tisa sasa na hajawahi kuyatumia. Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inashukuru uamuzi wa kuyaondoa mapendekezo haya kwa sababu yangeleta mjadala usiokuwa na tija yoyote na kupoteza bure muda wa Bunge lako tukufu na fedha za walipa kodi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,**
Kama inavyoelezwa katika Madhumuni na Sababu za Muswada huu, endapo Sehemu hizo zisingeondolewa na Bunge lako tukufu likakubali kuupitisha kama ulivyokuwa, mashirika na taasisi za Serikali yangekuwa "... *na wajibu wa kumtaarifu Mwanasheria Mkuu wa Serikali juu ya kufunguliwa au kusudio la kufunguliwa kwa shauri lolote dhidi ya shirika au taasisi husika.*" Taarifa hii, kwa mujibu wa maelezo ya Mwanasheria Mkuu, ingemuwezesha Mwanasheria Mkuu "... *kuangalia kama kuna haja ya kuingilia kati au la.*" Hapa pia, hakukuwa na sababu yoyote ya kuleta mapendekezo haya kwani tayari Mwanasheria Mkuu anayo mamlaka hayo kwa mujibu wa sheria ya sasa.

Kwa mujibu wa kifungu cha 6(c) cha *Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu*, Mwanasheria Mkuu ana mamlaka ya kumtaka ofisa yeyote wa umma "*kutoa taarifa yoyote kuhusiana na jambo lolote ambalo linahitaji ushauri wa kisheria.*" Aidha, kwa mujibu wa aya ya (d) ya kifungu hicho, Mwanasheria Mkuu ana mamlaka ya "*kumwita ofisa yeyote kwenye utumishi wa umma kueleza jambo lolote ambalo linahusu mashauri ya au dhidi ya Serikali.*"

Kwa maana hiyo, kama Mwanasheria Mkuu anataka kupata taarifa kuhusu kesi yoyote inayohusu Serikali, taasisi au mashirika yake, tayari anayo mamlaka ya kupata taarifa hizo na amekuwa na mamlaka hayo kwa zaidi ya miaka tisa! Hata hivyo, kama ilivyokuwa kwa mamlaka yake ya kuingilia mashauri mbali mbali, Kamati ilielezwa na wawakilishi wa mashirika na taasisi husika za umma kwamba Mwanasheria Mkuu hajawahi kuyatumia mamlaka yake chini ya kifungu cha 6(c) na (d) kuhusiana na mashauri mbali mbali ya mashirika na taasisi hizo!

**Mheshimiwa Spika,**
Sio tu kwamba Mwanasheria Mkuu ana mamlaka kamili na makubwa ya kuingilia kesi yoyote ile, iwe inaihusu Serikali na mashirika au taasisi zake au la, katika hatua yoyote ile ilikofikia, bali pia Mwanasheria Mkuu ana mamlaka ya

kuhamisha kesi hizo kutoka mahakama moja kwenda mahakama nyingine. Kwa mujibu wa kifungu cha 6(b) cha *Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu*, pale ambapo shauri, rufaa au kukaza hukumu imefunguliwa katika Mahakama ya Mwanzo, Mwanasheria Mkuu au 'Ofisa wa Sheria' au Wakili wa Serikali ana uwezo wa kuwasilisha hati katika Mahakama hiyo kuitaka ihamishie jambo hilo kwenye Mahakama ya Wilaya iliyo na mamlaka kwa ajili ya maelekezo ya ziada.

Ni wazi, kwa hiyo, kwamba Mwanasheria Mkuu ana mamlaka kamili na makubwa kwa mujibu wa sheria za sasa ya kufanya mambo ambayo Bunge lako tukufu lilikuwa linaombwa kumpatia kwa kupitisha Muswada huu. Ndiyo maana ni jambo jema kwamba Mwanasheria Mkuu amekubali ushauri wa Kamati wa kuondoa mapendekezo haya kwenye Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,**
Kama mapendekezo ya marekebisho yaliyoko kwenye Sehemu za II hadi XXVIII yangebaki katika Muswada huu, basi kusingekuwa na uwezekano wowote ule wa mtu yeyote yule, au shirika, taasisi au kampuni yoyote ile binafsi wa kupata haki, endapo Serikali au taasisi na mashirika yake yote yaliyotajwa kwenye Muswada huu yatashtakiwa mahakamani na kushindwa kesi. Ili kuthibitisha ukweli wa kauli hii ni muhimu kwa Waheshimiwa Wabunge kuelewa maana halisi ya maneno yaliyoko kwenye aya mbali mbali za Muswada huu kwamba "*pale ambapo Mwanasheria Mkuu anaingilia jambo lolote, basi masharti ya Sheria ya Mashauri ya Serikali yatatumika kuhusiana na mashauri au jambo hilo kana kwamba yamefunguliwa na, au dhidi ya, Serikali.*"

**Mheshimiwa Spika,**
Ni nini hasa maana ya mashauri yaliyoko mahakamani kugeuzwa kuwa 'mashauri ya Serikali'? Majibu ya swali hili yanapatikana katika Sheria tajwa, yaani *Sheria ya Mashauri ya Serikali, Sura ya 5 ya Sheria za Tanzania*. Ijapokuwa ni kweli, kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria hiyo, kwamba Serikali na watumishi wake mbali mbali wanaweza kushtakiwa kwa makosa mbali mbali wanayoyatenda wakati wakitimiza majukumu yao kama watumishi wa Serikali, masharti yaliyopo katika Sheria hiyo yamefanya utekelezaji wa haki ya kuishtaki Serikali au watumishi wake kuwa ndoto.

Kwanza, kwa mujibu wa kifungu cha 6(2), mtu yeyote anayekusudia kufungua mashauri dhidi ya Serikali lazima kwanza awasilishe kusudio hilo kwa Waziri wa Serikali, Idara au ofisa anayehusika kwa notisi ya muda usiopungua siku tisini. Kifungu hicho kinamlazimu mdai huyo kuelezea msingi wa madai yake dhidi ya Serikali na lazima apeleke nakala ya notisi hiyo kwa Mwanasheria Mkuu. Bila kutimiza masharti haya, kifungu cha 6(2) kinasema wazi kwamba "*hakuna shauri litakalofunguliwa dhidi ya Serikali na kusikilizwa....*" Mawakili na wadaawa wengi waliokumbana na makali ya masharti haya wanafahamu jinsi

ambavyo kesi nyingi dhidi ya Serikali hutupiliwa mbali na mahakama zetu kila mwaka– na hivyo wananchi wengi walioumizwa na Serikali hii au na watendaji na watumishi wake kukosa haki zao - kwa sababu tu ya kutotimizwa kwa masharti ya kifungu cha 6(2) cha Sheria hiyo.

Pili, kwa mujibu wa kifungu cha 6(4) cha Sheria ya Mashauri ya Serikali, "*mashauri yote dhidi ya Serikali yatafunguliwa katika Mahakama Kuu....*" Msimamo huu unatiliwa nguvu zaidi na kifungu cha 7 kinachosema: "*Bila kujali sheria nyingine yoyote, hakuna mashauri ya madai dhidi ya Serikali yatakayofunguliwa katika mahakama nyingine yoyote isipokuwa Mahakama Kuu.*" Mwanasheria Mkuu alidai katika maelezo yake mbele ya Kamati kwamba hili sio tatizo kwani "... *Serikali imejitahidi kujenga ofisi za Mikoa za Mahakama Kuu katika kila Mkoa ambazo wananchi huzitumia kufungua mashauri.*"

Kauli hii ya Mwanasheria Mkuu inahitaji kulinganishwa na hali halisi ya nchi yetu ambapo, kwa sasa, mikoa ya Singida, Lindi, Pwani, Morogoro, Njombe, Katavi na Kigoma haina masjala za Mahakama Kuu. Mikoa mingine ambayo haina masjala za Mahakama Kuu ni Mara, Manyara, Simiyu, Geita na Mkoa wa Shinyanga ambao masjala yake ya Mahakama Kuu haijafunguliwa bado kwa sababu majengo yake hayajakamilika. Kwa maana hiyo, kati ya mikoa ishirini na sita ya Tanzania Bara, mikoa kumi na mbili haina masjala za Mahakama Kuu na wananchi wa mikoa hiyo wanalazimika kutumia gharama kubwa kwenda mikoa ya jirani yenye masjala za Mahakama Kuu ili kufungua na kuendesha mashauri mbali mbali.

**Mheshimiwa Spika,**
Kama ni kweli – na Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inaamini ni kweli - kwamba Mwanasheria Mkuu tayari ana mamlaka kamili na makubwa ya kuingilia kesi yoyote ile, katika hatua yoyote ile, wakati wowote ule anapotaka; kama ni kweli – na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inajua ni kweli – kwamba **Mwanasheria Mkuu ana uwezo kisheria wa kupata taarifa yoyote ile kutoka kwa ofisa yeyote yule wa umma kuhusu shauri au jambo lolote lile lililopo katika mahakama yoyote ile au linalohitaji ushauri wowote ule wa kisheria, swali la wazi linalohitaji kuulizwa na kujibiwa kwa ukweli na ufasaha ni je, kwa nini Muswada huu umeletwa mbele ya Bunge lako tukufu? Je, lengo hasa la mapendekezo haya ni lipi? Na je, kupitishwa kwa Muswada huu, kama Bunge lako tukufu linavyoombwa kufanya, kutakuwa na athari gani kwa nchi yetu na kwa wananchi wetu?**

**Jibu la jumla la maswali yote haya ni kwamba Serikali hii ya CCM inataka kusiwe na uwezekano wowote ule wa mtu yeyote yule, au shirika, taasisi au kampuni yoyote ile binafsi wa kupata haki, endapo Serikali au taasisi na mashirika yake yote yaliyotajwa kwenye Muswada huu yatashtakiwa mahakamani na kushindwa kesi. Ili kuthibitisha ukweli wa kauli hii ni muhimu**

**kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kuelewa maana halisi ya maneno yaliyoko kwenye aya mbali mbali za Muswada huu kwamba "*pale ambapo Mwanasheria Mkuu anaingilia jambo lolote, basi masharti ya Sheria ya Mashauri ya Serikali yatatumika kuhusiana na mashauri au jambo hilo kana kwamba yamefunguliwa na, au dhidi ya, Serikali.*"**

**Mheshimiwa Spika,**
Ni vyema ikaeleweka vizuri kuwa mtu wa leo sio wa kesho kutokana na anavyo-approach issues, hivyo kama sheria zilizotungwa miaka ya 90 zilikosewa au mazingira ya wakati huo ilikuwa sahihi lakini sheria hizo hizo kwa miaka hii sio sahihi ni kwanini mfumo wa uandishi wa sheria zetu ubaki kuwa ule ule?

**Mheshimiwa Spika,**
Kambi Rasmi ya Upinzani inasema hivyo kutokana na ukweli kwamba sheria *inayotungwa* au karne hii ya sayansi na Teknolojia hakuna ulazima wowote Wenyeviti wa Bodi au Watendaji wakuu kuteuliwa na Rais, ni dhahiri kuendelea kukumbatia dhana hiyo ya uteuzi kuwa ni mamlaka ya Rais ni kuwafanya watendaji kukosa ubunifu na badala yake kuendelea kucheza ngoma inayopigwa na Rais. Kwa muktadha huo Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa kifungu cha 5(2)(a) cha uteuzi wa Mwenyekiti wa bodi iwe Mwenyekiti wa Bodi atateuliwe kutoka miongoni mwa wajumbe wa bodi na nafasi ya Mtendaji Mkuu wa Taasisi ishindaniwe kwa sifa zilizoainishwa na kifungu cha 8(2) na ikilazimu vigezo viongezwe.

**Mheshimiwa Spika,**
Kifungu cha 5(2) (b) kinahusu wajumbe tisa wa bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania watakaoteuliwa na Waziri. Kwa kuwa taasisi hii ya Utafiti wa kilimo,pamoja na mambo mengine itakuwa na jukumu la kusimamia tafiti zote za kilimo Tanzania, bila ya kubagua kuwa zinafanywa na watafiti toka taasisi binafsi au wa taasisi za Serikali. Lakini kati ya wateule 9 wa Waziri wajumbe 6 ni watendaji wa Serikali na 1 inasema ni Mtendaji Mkuu atakayewakilishwa kutoka taasisi binafsi za utafiti wa Kilimo. Kwa maana hiyo wajumbe zaidi ya wale waajiriwa wa Serikali ni 2 tu

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa kuwa utafiti kwenye kilimo unaweza kuwa ni sehemu ya kilimo cha kibiashara, kwa wakulima wakubwa kama ambao wanasemwa kwenye mpango wa SACGOT kuwa na vituo vya vya utafiti kwa kadri ya mahitaji yao ni jambo la kawaida kabisa. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa; badala ya kuwajaza watendaji wa Serikali kwenye bodi ni bora tuangalie ni upande upi utakaoleta tija zaidi kwa maendeleo ya Taifa letu. Hivyo basi, kuwa na wajumbe toka sekta binafsi ni suala la muhimu sana.

Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupewa tafsiri ya kifungu kidogo cha 5 (2)(b)(iii).

**Mheshimiwa Spika,**
Kifungu cha 7 kinachohusu posho kwa wajumbe wa bodi, kifungu kinapendekeza wajumbe walipwe posho zitakazoainishwa na Waziri mara baada ya kupendekezwa na bodi. Kama ambavyo Kambi Rasmi imekuwa ikishauri kwamba posho za wajumbe wa bodi pendekezo lisitoke kwa wajumbe wenyewe bali viwango vya posho kwa wajumbe wa bodi zipangwe na ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Ofisi inayohusika na utumishi wa umma. Kambi Rasmi inasema hili kutokana na uzoefu wa bodi za taasisi kadhaa mbapo wajumbe wa bodi wanajilipa posho za vikao ambayo kwa hali halisi ya Tanzani haiwezekani na bodi inapanga vikao vyake vifanyike sehemu ambazo ni ghali sana wakati huo posho zao za vikao ziko pale pale.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa kuwa lengo la sheria ni ujenzi wa taasisi za kiutendaji kuwa imara katika mfumo mzima wa uendeshaji wa nchi. Hivyo basi, kifungu cha 8(1) kinachosema kuwa Mtendaji Mkuu wa Taasisi atateuliwa na Rais baada ya kupata ushauri wa Waziri kutoka miongoni mwa watu wenye sifa na uzoefu. Aidha, kifungu cha 8(2) kimeorodhesha sifa zinazohitajika kwa kazi hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikisemea utaratibu huu wa uteuzi ambao unawafanya wateuliwa kuwa ni hisani ya waliowateua badala ya kuona kwamba wanastahili kazi hizo na jambo hilo limepelekea wateuliwa kutokufanyakazi kwa mujibu wa taaluma zao na matakwa ya kazi zao na badala yake wamekuwa wanatekeleza matakwa ya mamlaka za uteuzi.

**Mheshimiwa Spika,**
Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuwa,ili utumishi wa umma uwe imara ***(strong civil service)*** ni lazima ajira za utendaji zipitie kwenye mfumo ambao hautakuwa na ushawishi wa mtu yeyote wala upendeleo wa aina yoyote. Vinginevyo thamani ya taaluma itaendelea kudharauliwa kutokana na ushauri wao wa kitaaluma kutoheshimika mbele ya watawala.

**Mheshimiwa Spika,**
Kifungu cha 9 cha muswada kinaipa bodi uwezo wa kuanzisha idadi yoyote ya Idara na Vitengo chini ya taasisi kwa kuzingatia muundo wa Taasisi ulioidhinishwa, naomba ninukuu kifungu husika; ***"9(1) for the proper discharge of the functions of the Institute under this Act, the Board <u>shall establish such</u> number of departments and units under the Institute in accordance with <u>the approved</u> organizational structure".***
Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kujua huo muundo utaidhinishwa na nani? Wakati huo hapo awali Bodi imepewa nguvu ya kuanzisha idara na vitengo kwa kadri itakavyoona inafaa. Kwa s kutoa mwanya huu katika sheria, kuna

uwezekano mkubwa kwa idara hata ambazo hazitokuwa na mahitaji zikaanzishwa kwa lengo la kutoa ajira kwa watu wa aina fulani. Hii ni hatari kwa sheria kuacha mwanya huu bila kuzibwa, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini Idara kuu ya Utumishi ndio chombo mwafaka cha kuangalia miundo ya Idara na vitengo vinavyohitaji kwa taasisi na wakala mbalimbali wa Serikali, vinginevyo iwe ni kwa maelekezo maalum toka kwa Rais.

**Mheshimiwa Spika,**
Kifungu cha 10(1) kinahusu ajira za watumishi wa Taasisi, na kifungu kinasema kwamba, ***"The Institute shall, with approval of the Board, appoint or recruit on competitive basis such other staff………..."***

Kambi Rasmi ya Upinzani inaliona hili jambo la Taasisi kupewa uwezo wa kuteua watumishi/wafanyakazi baada ya bodi kuwa tayari imeunda Idara na vitengo sio busara na hapa ndipo mambo ya "nepotism" yatakapojitokeza. Pia hakuna kitu kama **uteuzi wa ushindani**, hivyo basi Kambi inashauri maneno ***"appoint or"*** yafutwe ili sheria iwe chombo cha kutenda haki.

**Mheshimiwa Spika,**
Kifungu cha 10(2) kinasema kuhusiana na kipindi cha utendaji kazi kwa waajiriwa wa Taasisi kuwa itakuwa ni bodi kuamua ni muda gani watendaji hao wafanye kazi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona itakuwa vyema kama ambavyo sheria imeweka muda wa bodi kuhudumu na muda wa Mtendaji Mkuu kuhudmu, vivyo hivyo muda wa watendaji kuhudumu ungewekwa wazi ili kuondoa tabia iliyopo ya watendaji kuzeekea kwenye viti jambo ambalo lilionekana kuwa ofisi ni mali binafsi za watendaji na jambo hili linawanyima fursa watu wengine kufanyakazi katika taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika,**
Kifungu cha 11(2) kinasema kuwa, **"the research centres shall be headed by a director <u>who shall be appointed</u> by the Board".**

Tanzania ina wataalam wengi sana katika fani ya kilimo na wengine bado wanaendelea kufuzu kutoka vyuo vya ndani na vya nje. Kambi Rasmi ya Upinzani inapingana na dhana ya Uteuzi kwani inaua kabisa dhana ya ushindani wa wazi, jambo hili linazidisha kile kinachoitwa kuwajibika kwa mtu badala ya kuwajibika kwa majukumu ya kazi. Hivyo basi ili kuleta ushindani kwa wale wote wenye sifa ni vyema kuendesha mchakato wa wazi wa watu kuomba na kufanyiwa usahili kwa kazi husika, badala ya uteuzi ambapo watu wale wale wamekuwa wanazunguka kutoka kituo kimoja kwenda kingine.

**Mheshimiwa Spika,**
Kifungu cha 35(3) cha muswada kinahusu rufaa kwa kusema kuwa, **"The decision by the Minister shall be final".** Kifungu hiki kwa mantiki yake

kinapingana na kifungu cha 3(2) (b), 3 (3), 3(4) na 3 (5). Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, kama vifungu hivyo vinatoa nafasi kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia mashauri yoyote ambayo Taasisi itakuwa imeshtaki au kushtakiwa, inakuwaje kifungu cha 35(3) kinasema kuwa uamuzi wa Waziri utakuwa ni wa mwisho? Na haioneshi kuwa utaratibu wa kimahakama unapewa nafasi yoyote ili wahusika wapate haki zaidi.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa uchambuzi huo wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye vifungu ambavyo nimevionesha hapo awali, naomba kuwasilisha.

**…………………………..**
**Dr. Sware Semesi (Mb)**
**K.n.y Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-**
**Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi.**
**14 September, 2016**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge ninaomba wachangiaji wa vyama vyote walete, yafike mapema mezani. Nawashukuru.

Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa mwaka 2016**
***(The Fisheries Research Institute Bill, 2016)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mtoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii tena kwa mara nyingine kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano walioutoa kwa Wizara yangu katika kuboresha Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi ya mwaka 2016 yaani *The Tanzania Fisheries Reserch Institute Bill, 2016.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umezingatia maoni ya wadau yaliyotolewa kwa Kamati ya Bunge tarehe 29 Agosti 2016 hadi tarehe 2 Septemba, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la muswada huu ni maamuzi ya Baraza la Mawaziri kupitia Waraka wake wa mwaka 2014/2015 kuhusu mapendekezo ya kutunga Sheria ya Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi Tanzania. Kupitia kikao chake cha tarehe 20 Januari, 2015 Baraza la Mawaziri liliridhia na kuelekeza kutungwa kwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za utafiti wa uvuvi zilikuwa zinafanyika chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyojumuisha nchi za Kenya, Tanzania na Uganda. Baada ya kuvunjika kwa Jumuiya mwaka 1977 shughuli hizi zilihamishiwa Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya Idara ya Uvivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1980 Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(TAFIRI)* ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 6 ya mwezi Februari, 1980 *(The Tanzania Fisheries Research Institute Act No. 6 of 1980)*. Hadi sasa *TAFIRI* imeendelea kufanya utafiti wa uvuvi hapa nchini kupitia vituo vyake vya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Kyela na kituo kidogo cha Sota, Mkoani Mara. Makao Makuu ya Taasisi yako Kunduchi, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti Tanzania *(The Tanzania Fisheries Research Institute Bill, 2016)* unakusudia kuleta mapendekezo ya sheria mpya itakayosimamia utafiti wa uvuvi na ukuzaji wa viumbe kwenye maji. Aidha, muswada huu utafuta Sheria iliyopo ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Namba 6 ya mwaka 1980 *(The Tanzania Fisheries Research Institute Act No. 6 of 1980)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu yafuatayo yamezingatiwa katika sheria inayopendekezwa kutungwa:-

(i) Kuipa taasisi mamlaka ya kushughulikia utafiti wa ufugaji wa viumbe kwenye maji.

(ii) Kuzingatia mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

(iii) Kuweka utaratibu wa kufuatilia tafiti zinazofanyika nje na ndani ya nchi kwa kutumia rasilimali za uvuvi za Tanzania.

(iv) Kutambua uwepo wa vituo vya utafiti wa uvuvi vya Dar es Salaam, Kigoma, Kyela na Mwanza vitakavyoanzishwa.

(v) Kuanzisha utaratibu wa kutoa tuzo za ugunduzi katika utafiti wa uvuvi ambazo zinatambuliwa na *COSTECH*.

(vi) Kuipa taasisi mamlaka ya kumiliki aina zote za ugunduzi.

(vii) Kutambua hakimiliki za watafiti na wagunduzi.

(viii) Kuainisha shughuli za utafiti wa uvuvi na ufugaji wa viumbe kwenye maji.

(ix) Kuainisha shughuli za watafiti wa ndani na nje ya nchi.

(x) Kuweka utaratibu wa kumbana mtafiti anaposhindwa kuwasilisha taarifa ya mwisho ya utafiti.

(xi) Kuweka utaratibu wa kusitisha shughuli za utafiti pale mtafiti anaposhindwa kutekeleza wajibu wake.

(xii) Kuanzisha cheo cha Naibu Mkurugenzi Mkuu.

(xiii) Kuweka utaratibu wa uteuzi wa watumishi wa taasisi wa kada mbalimbali utakao simamiwa na Bodi.

(xiv) Kuweka kanuni zitakazohusu masuala ya fedha na watumishi wa taasisi.

(xv) Kuweka utaratibu wa kusimamia nidhamu ya Watumishi kuanzia Mtendaji Mkuu na watumishi wa chini yake.

(xvi) Kuruhusu ushiriki wa sekta binafsi katika utafiti na tuzo za ugunduzi.

(xvii) Kumarisha uhusiano wa utafiti wa kikanda na kimataifa.

(xviii) Kuweka viwango stahiki vya adhabu kwa makosa mbalimbali kwa watafiti wa nje ya ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria mpya inatarajia kuwa na matokeo yafuatayo:-

(i) Kuwepo na utaratibu wa kufuata kwenye tafiti zinazofanyikia nje ya nchi kwa kutumia rasilimali za uvuvi kutoka Tanzania Bara.

(ii) Kuongezeka kwa tija katika ugunduzi kwenye tasnia ya uvuvi.

(iii) Kufutwa kwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Namba 6 ya mwaka 1980.

(iv) Taasisi kuwa na hatimiliki ya aina zote za ugunduzi ilioufanya au uliofanywa kwa niaba yake.

(v) Kuwepo kwa vituo vya utafiti vitakavyotambulika rasmi na vitakavyoanzishwa kisheria chini ya taasisi.

(vi) Kupanuka kwa matumizi ya sayansi na teknolojia.

(vii) Kupanuka kwa wigo wa upatikanaji wa matokeo ya tafiti za uvuvi.

(viii) Kukuza ufugaji wa viumbe kwenye maji *(aquaculture)*.

(ix) Kupungua kwa makosa yatokanayo na ukiukwaji wa sheria.

(x) Taasisi kuweza kufuatilia watafiti wa ndani na wa nje ya nchi.

(xi) Kuongezeka uwajibikaji wa watafiti.

(xii) Kuwepo kwa ushuriki wa watafiti binafsi katika utafiti wa uvuvi.

(xiii) Kuwianisha sheria na sheria zingine za uvuvi zilizopo pamoja na sheria mbalimbali zinazogusa sekta ya uvuvi. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003, Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Sura 388, Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Namba 29 ya mwaka 1994 *(The Territorial Sea and Exclusive Economic Zone Act. 1989),* Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 20 ya mwaka 20014, Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Namba 7 ya mwaka 1986, Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Namba11 ya mwaka 2009, Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999.

(xiv) Taasisi itakuwa na mfumo mzuri wa utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpangilio wa muswada huu ni kuwa umegawanyika katika sehemu siya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza inahusu mambo ya utangulizi, jina la Muswada na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria; ufafanuzi wa maeneo yaliyotumika na madhumuni ya sheria inayopendekezwa kutungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili inaelezea uanzishwaji wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania na majukumu yake. Aidha, sehemu hii pia inaainisha utaratibu wa kuanzisha taasisi, vituo vya taasisi, kazi za taasisi, uundwaji na uendeshwaji wa vikao vya bodi na mamlaka ya Waziri kuhusiana na bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu inahusu vifungu vinavyohusu utafiti wa uvuvi na ufugaji viumbe kwenye maji. Shughuli za utafiti wa uvuvi na ufugaji viumbe kwenye maji, hitaji la kuwasilisha taarifa za utafiti kwenye taasisi, taasisi kuhitaji taarifa za utafiti wa uvuvi na viumbe kwenye maji unaofanywa na mtafiti wa ndani ya nchi, watafiti kutoka nje ya nchi na kushindwa kuwasilisha taarifa ya mwisho ya utafiti, usitishwaji wa utafiti, utaratibu wa utafiti unaofanywa nje ya Tanzania Bara, masharti yanayohusu Uvumbuzi, Mamlaka ya Mkurugenzi wa Uvuvi au Mkurugenzi wa Ukuzaji wa Viumbe Kwenye Maji kuhusiana na utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne inahusu uteuzi, kazi na mamlaka ya Mkurugenzi Mkuu. Uteuzi wa Naibu Mkurugenzi Mkuu, uteuzi wa wakurugenzi wa vituo, wakuu wa wdara na vitengo, wafanyakazi wengine wa taasisi, utaratibu wa uteuzi, bodi kukasimu madaraka, utoaji wa amri na maelekezo, marupurupu ya wajumbe wa bodi na kinga dhidi ya mashtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano inahusu masuala ya fedha na ina Ibara zinazohusu mafao ya uzeeni, fedha za taasisi, mamlaka ya bodi kutoza tozo, uwekezaji wa fedha, mamlaka ya kukopa, bajeti ya mwaka na bajeti ya nyongeza, hesabu na ukaguzi wa hesabu, taarifa ya fedha ya mwaka na uwasilishwaji wa taarifa hizo Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita inahusu masharti ya jumla kama vile kubainisha makosa na adhabu chini ya sheria inayopendekezwa na mamlaka ya Waziri ya kutunga kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano ya mwisho muswada huu unapendekeza majedwali mawili *(schedules)* kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hii. Jedwali la kwanza linaelezea vituo vya taasisi ambavyo viko vinne ambavyo ni vituo vya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma na Kyela. Jedwali la pili linahusu Bodi ya Wakurugenzi, muundo na namna ya uendeshaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muswada huu uingie pamoja na Majedwali ya Marekebisho. Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namuita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Maji, au mwakilishi wake.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA (MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi ya mwaka, 2016 *(The Tanzanian Fisheries Research Institute Bill, 2016).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kupokea Muswada wa Sheria, Kamati ilitoa mwaliko kwa wadau mbalimbali kupitia vyombo vya habari, kwa kuwatumia barua na nakala ya muswada kwa njia ya posta na kwa kutumia barua pepe. Wajibu huu ulitekelezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaliko uliotolewa ulikusudia kuwapa wadau fursa ya kutoa maoni yao kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya sheria inayokusudiwa kutungwa na hatimaye kuisaidia Kamati kufanya uchambuzi wa kina wa muswada tajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi wa muswada watendaji wakuu na wawakilishi wa Taasisi za Utafiti wa uvuvi taasisi mbalimbali za Serikali na mashirika yasiyo ya Serikali ambayo muswada wa sheria inayopendekezwa unawagusa walihudhuria vikao vya Kamati ili kutoa michango yao kwa njia ya majadiliano na kwa maandishi. Aidha, Chama cha Wavuvi wa Kati Tanzania Bara (CHAWAKATA) walifika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 29 Agosti, 2016 Kamati ilikutana na Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi katika ukumbi wa *Mount Meru* ulioko Jengo la *Hazina Square*, Dodoma kwa lengo la kupokea maelezo ya Serikali kuhusu muswada husika. Aidha, terehe 2 Septemba, 2016 Kamati ilifanya kikao cha mashauriano na Wizara kuhusu marekebisho ya muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kukutana na kupata maoni ya wadau mbalimbali, iliendelea kukutana na Watendaji wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi, wawakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wawakilishi wa Mshauri wa Sheria kutoka Ofisi ya Bunge kwa lengo la kubadilishana mawazo na kupata uelewa mpana kuhusu maudhui ya muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yake, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi aliieleza Kamati kuwa Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa mwaka 2016 yaani *The Tanzania Fisheries Research Institute Bill, 2016* unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, 2016 *(Tanzania Agricultural Research Institute Act, 2016)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania unakusudia kufuta Sheria iliyopo ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Na.6 ya mwaka 1980 *(The Tanzania Fisheries Research Institute Act No.6 of 1980)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu unakusudia kuleta mapendekezo ya Sheria mpya ambayo pamoja na mambo mengine itasimamia utafiti wa uvuvi na ukuzaji wa viumbe kwenye maji. Aidha, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa Muswada huu una sehemu sita na jumla ya vifungu thelathini na tisa na kwa ukamilifu unasomeka kuwa ni Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa ninaomba niwasilishe maoni na ushauri wa Kamati kuhusu muswada huu. Maoni haya kwa kiasi kikubwa yametokana na uchambuzi wa Kamati na maoni ya wadau mbalimbali pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Serikali. Hata hivyo, kabla ya kuanza kuwasilisha maoni ya Kamati ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Jedwali la Marekebisho mlilopewa, ni matokeo ya Uchambuzi wa muswada uliyofanywa na Kamati kutokana na muswada wenyewe na maoni ya wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zote zilizoibuliwa na Kamati kuhusu marekebisho ya muswada huu zilikubaliwa na Serikali na kuhitimishwa kama zilivyoonekana kwenye kiambatisho ambacho ni Jedwali la Uchambuzi wa muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya ambayo muktadha wake unapatikana katika sehemu ya muswada ijulikanayo kama madhumuni na sababu yanalenga kuwezesha yafuatayo kutokea:-

(i) Kuwepo kwa utaratibu wa kufuata kwenye tafiti zinazofanyika nje ya nchi kwa kutumia rasilimali za uvuvi kutoka Tanzania Bara.

(ii) Kuongezeka kwa tija katika ugunduzi kwenye tasnia ya uvuvi.

(iii) Kufutwa kwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Namba 6 ya mwaka 1980.

(iv) Taasisi kuwa na hatimiliki ya aina zote za ugunduzi uliofanya au uliofanywa kwa niaba yake.

(v) Kuwepo kwa vituo vya utafiti vitakavyotambulika rasmi na vitakavyoanzishwa kisheria chini ya taasisi.

(vi) Kupanuka kwa matumizi ya sayansi na teknolojia.

(vii) Kupanuka kwa wigo wa upatikanaji wa matokeo ya tafiti za uvuvi.

(viii) Kukuza ufugaji wa viumbe kwenye maji yaani *aqua culture*.

(ix) Kupungua kwa makosa yatokanyo na ukiukwaji wa sheria.

(x) Taasisi kuweza kufuatilia watafiti wa ndani na je ya nchi.

(xi) Kuongeza uwajibikaji wa watafiti.

(xii) Kuwepo kwa ushiriki wa watafiti binafsi katika utafiti wa uvuvi.

(xiii) Taasisi kuwa na mfumo mzuri wa utendaji kazi.

(xiv) Kuwianisha sheria zingine za uvuvi zilizopo pamoja na sheria mbalimbali zinazogusa sekta ya uvuvi. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003; Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Sura 388; Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Namba 29 ya mwaka 1994; *The Territorial Sea and Exclusive Economic Zone Act, 1989*; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 20 ya mwaka 2014; Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Namba 7 ya mwaka 1986; Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Namba 11 ya mwaka 2009, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono madhumuni na sababu ya Serikali kuhusu muswada huu kwani yanalenga kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania na kuainisha kazi za Mamlaka ya Taasisi kuhusiana na uendeshaji wa utafiti wa uvuvi na utafiti wa ukuzaji viumbe kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na madhumuni na sababu ya Serikali kuleta muswada huu Bungeni, napenda ieleweke wazi Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 6 ya mwaka 1980 ambayo imekuwa ikisimamia utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya taasisi hii. Hata hivyo, kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia na ukweli kwamba sheria iliyopo imefanya kazi kwa takribani miaka 36 upungufu mwingi ya kisheria yamejitokeza na kukwamisha baadhi ya shughuli za taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wanaweza kujiuliza kwanini sheria iliyopo isingeliletwa Bungeni kwa utaratibu wa *miscellaneous amendments,* utaratibu ambao umekuwa ukitumika kufanya marekebisho kwenye sheria mbalimbali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako kuwa Kamati imejiridhisha kuwa marekebisho yanayohitajika kwenye sheria iliyopo ni mengi kiasi kwamba haiwezekani kuifanyia marekebisho sheria iliyopo. Aidha, kwa mujibu wa taratibu za uandishi wa sheria, sheria ikihitaji marekebisho zaidi ya nusu ya sheria yenyewe hakuna budi kuifuta sheria hiyo na kuiandika upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo Kamati imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa ili kuwezesha nchi kuwa na sheria mpya ambayo itafuta Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Namba 6 ya mwaka 1980 na kuanzisha sheria mpya ambayo itawezesha kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi *(Tanzania Fisheries Research Institute -TAFIRI),* taasisi ambayo itakuwa chombo huru cha kisheria cha kusimamia na kuratibu utafiti wa uvuvi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kamati kuunga mkono mapendekezo ya sheria inayokusudiwa kutungwa, yapo mambo kadhaa ambayo yaliibua wasiwasi kwa Wajumbe wa Kamati wakati wa uchambuzi wa muswada na hivyo kuhitaji ufafanuzi wa kina kutoka kwa Serikali. Mambo hayo ni pamoja na:-

(i) Kwa kuwa Chuo Kikuu cha Sokoine, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Tume ya Sayansi na Teknolojia ni taasisi za Serikali zilizoanzishwa kisheria na zina mamlaka ya kutoa vibali vya tafiti vya uvuvi, je, sheria inayopendekezwa ni kwa kiasi gani imezingatia kutokuwepo kwa muingiliano wa majukumu?

(ii) Wajumbe walitaka kufahamu sababu za msingi zilizopelekea Serikali kuleta muswada Bungeni unaotunga jina la sheria iliyopo.

Kamati ilitaka kufahamu kwa nini marekebisho yanayopendekezwa yasirekebishwa kupitia utaratibu wa *miscellaneous ammendment*? Wajumbe walitaka kufahamu utaratibu utakaotumika kuhakikisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya tafiti za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, Kamati ilifanya kikao cha majumuhisho na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi ambapo Waziri alitoa ufafanuzi wa hoja zote zilizoibuliwa na kufikia mwafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa muswada; sehemu ya kwanza ya muswada inayohusu masharti ya utangulizi. Katika sehemu hii ya kwanza Kamati ilitoa maoni na mapendekezo kwenye maeneo kadhaa yaliyohusu:-

(i) Kuongeza na kufuta baadhi ya maneno ambayo tafsiri ya maneno hayo ilileta mkanganyiko;

(ii) Kuongezwa kwa vifungu vipya; na

(iii) Kusahihisha makosa ya kiuchapaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya muswada inahusu uanzishwaji wa taasisi na majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu hii Kamati ilipendekeza kuondoa kifungu cha 5(5) ambacho maelezo yake yameshaelezwa kwenye kifungu cha (4)(1)(c). Kurekebisha kifungu 6(1)(d) kwa kuondoa maneno *carried out within Mainland Tanzania* ambayo yamejirudia. Pia kurekebisha kifungu cha 6(3) kwa kuondoa neno *shall* ambalo matumizi yake yanalazimisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(TAFIRI)* kushirikiana na taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa wakati wa kutekeleza majukumu yake; badala yake Kamati inapendekeza kuweka neno *may* ambalo litaiwezesha *TAFIRI* kutekeleza majukumu yake bila kushurutishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu hii pia kifungu cha 6(3) kipengele (g) hakijaweka uhakika wa kushirikisha taasisi za elimu ya juu zinazojihusisha na tafiti katika uvuvi. Kamati imependekeza kuongezwa kwa kipengele kipya ambacho kitakuwa (h) ambacho kinalenga kuhusisha Chuo Kikuu kinachotambulika nchini kwa kufanya tafiti za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipendekeza pia katika kifungu cha 6(3) (a) mpaka (f) Kamati imependekeza sheria sita zinazotajwa kwenye maelezo ya pembeni haziwiani na maudhui ya maelezo yaliyotolewa. Hivyo, Kamati imependekeza ili kuleta mantiki sheria zinazotajwa zipangwe kwa kufuatana na kifungu kilichotolewa maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 7 kinaelezea muundo wa taasisi ambapo taasisi inaweza kuanzisha kurugenzi, idara, kamati za ufundi au vitengo kulingana na majukumu yaliyoanishwa kama Bodi itakavyoamua.

Kamati imependekeza kwa kuzingatia muundo wa uendeshaji wa shughuli za taasisi, mpangilio wa taasisi yoyote uanaelezwa kwa kufuata utaratibu ufuatao; kurugenzi, idara, vitengo na sehemu. Kwa muktadha huo, Kamati inapendekeza kuongezwa kwa neno *units* baada ya neno *department*. Aidha, Kamati pia imependekeza maneno *techinical committee* yaondolewe na badala yake yayaelezwe kwenye kanuni zitakazotungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti sehemu ya tatu inahusu utawala wa taasisi. Sehemu hii inaelezea muundo na utaratibu wa Bodi kutekeleza majukumu yake, ambapo kwa kawaida inakuwa na kifungu kinachoelezea kuanzishwa na muundo wa bodi ya taasisi. Kwa sababu maelezo hayo yameelezwa kwenye Jedwali la Pili yenye kichwa cha habari kinachosomeka Masharti kuhusu Bodi ya Wakurugenzi, Kamati imependekeza maelezo ya maneno hayo yahamishiwe kwenye kifungu kipya cha 8(3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifugu cha 12(2) kilikuwa na makosa ya kiuchapaji tu, ambapo Kamati imeshauri kosa hilo lisahihishwe kwa kuondoa herufi "*n*" kwenye neno *Tanzanian* na neno hilo sasa litasomeka Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 12(b) kinaelezea Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na watendaji wengine wa taasisi. Kipengele cha 6 kinaeleza Mkurugenzi Mkuu atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Kamati inapendekeza maneno *for another term of five years* yaondolewe kwa kuwa yanajirudia na badala yake yawekwe maneno *for one more term* ili kuzingatia kanuni za kiuandishi na kuongeza ladha ya usomaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu hii pia, kifungu cha 14(i) kinaelezea uteuzi wa Wakurungezi na wafanyakazi wengine wa taasisi. Kwa kawaida mpangilio wa muundo wa taasisi unakuwa na idara, vitengo na sehemu. Neno *units* limesahaulika. Kamati imependekeza liongezwe neno *units* mara baada ya maneno *Heads of Departments* na kabla ya maneno *and Sections.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 14(3) kina makosa ya kiuchapaji ambapo alama ya mkato (,) imesahaulika baada ya neno *basis*. Hivyo, Kamati imependekeza kuweka alama ya mkato (,) kati ya maneno *basis* na *professional.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 14(4) kina makosa ya mpangilio ambapo rejea iliyofanywa kwenye kifungu kidogo cha (1) hailengi watumishi waliotajwa kwenye kifungu kidogo (2), hivyo Kamati imependekeza kifungu hicho kisahihishwe kwa kufanya rejea kwenye kifungu kidogo cha (2) ili kuleta maana iliyokusudiwa na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne inahusu mamlaka na uendeshaji wa taasisi. Kifungu cha 20(2) kinaeleza sharti la taasisi kuzingatia mtafiti toka nje ya nchi kufanya utafiti kwa kushirikiana na mtafiti toka ndani ya nchi; wakati kifungu cha 20(3) kinataka rejea ifanywe kwenye kifungu cha 20(2) ambacho hakijamaanisha mahitaji ya tafiti. Kamati imependekeza rejea ifanywe kwenye kifungu 19(2) ambacho kimeorodhesha mapendekezo ya kuzingatia wakati wa kufanya utafiti wa viumbe kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 22 kwenye maelezo ya pembeni kinaelezea usitishwaji wa utafiti, ambapo sehemu ya 22(b) inaeleza:-

"22. Endapo mtafiti atashindwa kuwasilisha:

(b) anashindwa wasilisha taarifa ambayo inayoridhisha, taasisi inaweza kusitisha utafiti huo na kumtaka mtafiti arudishe fedha zote alizopewa kwa madhumuni ya utafiti huo endapo hautakuwa wa kuridhisha."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imependekeza neno *satisfactory* liondolewe baada ya neno *is* badala yake liwekwe neno *prescribed.* Aidha, kanuni zitakazotungwa zieleze vigezo vya kutambua taarifa ya utafiti unaoridhisha. Vilevile Kamati imependekeza hitaji la kumtaka mtafiti kurudisha fedha zote alizopewa kufanya utafiti liondolewe na badala yake Kamati imependekeza kanuni zieleze kutakuwa na kamati ya ufundi ambayo pamoja na majukumu mengine itafanya kazi ya kufuatilia hatua mbalimbali za utafiti ili kuweza kubaini makosa kabla ya taarifa ya utafiti kufika mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 25 kwenye maelezo ya pembeni kina makosa ya kiuchapaji katika neno *directors.* Kamati inapendekeza neno "*s*" liondolewe ili kuandika lugha ya kiingereza kwa ufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti sehemu ya tano inahusu masuala ya fedha. Kamati inapendekeza kiongezwe kifungu kipya katika sehemu hii kitakachoeleza kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Utafiti wa Uvuvi. Kamati imefikia uamuzi huu kutokana na ukweli kwamba shughuli za utafiti zinahitaji fedha nyingi ambazo uzoefu unaonyesha kuwa fedha zinazopatikana mara nyingi ni fedha za wadau wa maendeleo ambapo fedha hizo hutolewa kulingana na masharti yanayoendana na vipaumbele vyao ambavyo si vipaumbele vya Taifa. Mathalani, sekta ya uvuvi inaweza isiwe kipaumbele cha mipango ya fedha za nchi wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine iliyoifanya Kamati kupendekeza sheria iweke hitaji la kuwa na mfuko maalum wa tafiti za uvuvi ni kutokana na kutotekelezwa kwa azimio la Serikali la kutenga asilimia moja ya Pato Ghafi la Taifa kila mwaka kwa ajili ya kugharamia tafiti, kwani hadi hivi sasa Serikali imeweza kuchangia chini ya asilimia 0.5 ya Pato Ghafi la Taifa kwenye tafiti. Aidha, fedha kidogo zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya tafiti mbalimbali huelekezwa Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* ambayo hutolewa kwa vigezo vya ushindani ambavyo si lazima vilenge sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 28 kinachoelezea uwekezaji kwenye maelezo ya pembeni kinapendekeza kuwa Bodi inaweza, kwa kibali cha Waziri kuwekeza sehemu yoyote ya fedha zilizopo kwenye mfuko wowote wa taasisi katika uwekezaji kama itakavyoidhinishwa na madhumuni kuhusu uwekezaji wa fedha kwenye Sheria ya Uwekezaji wa Wadhamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa kifungu cha 28 hakijazingatia hitaji la kumhusisha Msajili wa Hazina kama Sheria ya Msajili wa Hazina inavyohitaji. Sheria ya Msajili wa Hazina Sura Namba 370 ya mwaka 2002 na kama ilivyorekebishwa mwaka 2010 inaipa majukumu Ofisi ya Msajili wa Hazina kusimamia uwekezaji unaofanywa na taasisi, mashirika ya umma na makampuni yote ambayo Serikali ina hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa kifungu hiki kunamkosesha Msajili wa Hazina nguvu ya kufuatilia miradi ya uwekezaji kuanzia ngazi ya awali ya ubunifu wa mradi hadi katika hatua ya utekelezaji na utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi zote zilizo chini ya Msajili wa Hazina zinatakiwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kupata idhini ya Msajili wa Hazina juu ya posho zinazolipwa na taasisi kwa bodi na watumishi;

(ii) Kupata kibali cha Msajili wa Hazina cha Sera ya Uwekezaji;

(iii) Mpango wa uwekezaji wa taasisi uidhinishwe na Msajili wa Hazina;

(iv) Kama Taasisi imechukua mkopo kwa ajili ya uwekezaji kwa kutumia dhamana ya mali za taasisi inatakiwa ipate idhini ya Msajili wa Hazina; na

(v) Taasisi inatakiwa kuwasilisha Mpango wa Biashara *(Business Plan)* kwa Msajili wa Hazina kwa uchambuzi na idhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, Kamati imependekeza kiongezwe kifungu kipya kitakachoweka sharti la kumuhusisha Msajili wa Hazina katika uwekezaji utakaofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti sehemu ya sita inahusu masharti ya ujumla. Kifungu cha 37(2) kina kosa la kiuchapaji ambapo neno *Minster* limeandikwa kimakosa. Kamati imependekeza neno hilo lirekebishwe kwa kuongeza herufi “i” kati ya herufi “n” na herufi “s”, na neno hilo liandikwe kwa ufasaha na kusomeka *Minister*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 38 kinaelezea masharti ya ajira kwa wafanyakazi waliokuwepo kwenye taasisi ambapo wafanyakazi wote wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi watahamishiwa na kuajiriwa kwenye taasisi hii kuanzia mwaka wa kuanza kutumika kwa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki, Kamati imefanya marekebisho kwa kuondoa maneno *be transferred to and be employed by the institute* na badala yake kuweka maneno *continued to be employees of the institute;* hii ni kwa sababu taasisi hii haijaanzishwa upya, kilichofanyika ni kuboresha sheria iliyopo kwa kuiandika upya ili kukidhi mahitaji halisi ya uendeshaji na usimamizi wa sekta ya uvuvi nchini na hivyo watumishi walipo wataendelea kuhudumu katika nyadhifa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu inayohusu majedwali, jedwali la pili, kipengele cha 1(1) kinazungumzia masharti kuhusu Bodi ya Wakurugenzi na Muundo wa Bodi. Hata hivyo, hakuna kifungu kinachozungumzia muda maalum wa Mwenyekiti wa Bodi kukaa madarakani. Hivyo, Kamati imependekeza kuongezwa kwa kifungu kipya kinachoeleza Mwenyekiti wa Bodi atashika madaraka yake kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu kuanzia tarehe ya kuchaguliwa kwake na anaweza kustahili kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine kisichozidi miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ndogo ya pili inaeleza Mkurugenzi Mkuu au Afisa yeyote wa taasisi atakayeteuliwa na Mkurugenzi Mkuu atakuwa Katibu wa Bodi. Kamati inapendekeza maneno *or any employee of the Institute appointed by him* na badala yake yawekwe maneno *the Director General shall be the Secretary of the Board.* Kamati imependekeza hivyo kwa sababu Mkurugenzi Mkuu ndiye Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi na ndiye atakayewajibika na kutekeleza maamuzi yaliyofikiwa na Bodi.

Aya ya pili inaelezea utaratibu wa kumpata Makamu Mwenyekiti wa Bodi na muda wa kushika madaraka ambapo muswada unaeleza Makamu Mwenyekiti wa Bodi atashika ofisi kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe ya kuchaguliwa kwake na anaweza kustahili kuchaguliwa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba maneno yote yaingie kwenye *Hansard.*

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi Mheshimiwa William Olenasha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Basi ahsante. Wapelee message za shukrani hao.

## MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI YA MWAKA, 2016(*THE TANZANIA FISHERIES RESEARCH INSTITUTE BILL*, 2016) KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi ya Mwaka, 2016 (*The Tanzania Fisheries Research Institute Bill*, 2016).

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kupokea Muswada wa Sheria, Kamati ilitoa mwaliko kwa wadau mbalimbali kupitia vyombo vya habari, kwa kuwatumia barua na nakala ya Muswada kwa njia ya posta na kwa kutumia barua pepe. Wajibu huu ulitekelezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** mwaliko uliotolewa ulikusudia kuwapa wadau fursa ya kutoa maoni yao kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya sheria inayokusudiwa kutungwa na hatimaye kuisaidia Kamati kufanya uchambuzi wa kina wa muswada tajwa.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa muswada watendaji wakuu ama wawakilishi wa taasisi za utafiti wa uvuvi, taasisi mbalimbali za Serikali na mashirika yasiyo ya Serikali ambayo Muswada wa sheria inayopendekezwa unawagusa, walihudhuria vikao vya Kamati ili kutoa michango yao kwa njia ya majadiliano na kwa maandishi. Aidha, Chama cha Wavuvi wa Kati Tazania Bara (CHAWAKATA) walifika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao.

**Mheshimiwa Spika**, mnano tarehe 29 Agosti, 2016, Kamati ilikutana na Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi katika Ukumbi wa *Mount Meru* ulioko jengo la Hazina *Square*, Dodoma kwa lengo la kupokea maelezo ya Serikali kuhusu Muswada husika. Aidha, terehe 02 Septemba, 2016 Kamati ilifanya kikao cha mashauriano na Wizara kuhusu marekebisho ya Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kukutana na kupata maoni ya wadau mbalimbali, iliendelea kukutana na Watendaji wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi, wawakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wawakilishi wa Mshauri wa Sheria kutoka Ofisi ya Bunge kwa lengo la kubadilishana mawazo na kupata uelewa mpana kuhusu maudhui ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** katika maelezo yake, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi aliieleza Kamati kuwa Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa Mwaka, 2016 (*The Tanzania Fisheries Research Institute Bill*, 2016) unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, 2016 (*Tanzania Fisheries Research Institute Act*, 2016).

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (Tanzania *Fisheries Institute Bill*) unakusudia kufuta Sheria iliyopo ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Na. 6 ya Mwaka 1980 (The *Tanzania Fisheries Research Institute Act No. 6 of 1980*).

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unakusudia kuleta mapendekezo ya Sheria mpya ambayo pamoja na mambo mengine itasimamia utafiti wa uvuvi na ukuzaji wa viumbe kwenye maji. Aidha, katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa Muswada huu una sehemu sita (6) na jumla ya vifungu thelathini na tisa (39) na kwa ukamilifu unasomeka kuwa ni Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa Mwaka, 2016.

## 2.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo, sasa ninaomba niwasilishe maoni na ushauri wa Kamati kuhusu muswada huu. Maoni haya kwa kiasi kikubwa yametokana na uchambuzi wa Kamati na maoni ya wadau mbalimbali pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Serikali. Hata hivyo, kabla ya kuanza kuwasilisha maoni ya Kamati ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, jedwali la marekebisho mlilopewa, ni matokeo ya Uchambuzi wa Muswada iliyofanywa na Kamati kutokana na Muswada wenyewe na maoni ya wadau.

**Mheshimiwa Spika**, hoja zote zilizoibuliwa na Kamati kuhusu marekebisho ya Muswada huu zilikubaliwa na Serikali na kuhitimishwa kama zinavyoonekana kwenye kiambatanisho ambacho ni Jedwali la Uchambuzi wa Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo haya ambayo muktadha wake unapatikana katika sehemu ya Muswada ijulikanayo kama madhumuni na sababu *(objects and reasons) yanalenga* kuwezesha yafuatayo kutokea:-

i) Kuwepo kwa utaratibu wa kufuata kwenye tafiti zinazofanyikia nje ya nchi kwa kutumia rasilimali za uvuvi kutoka Tanzania bara;

ii) Kuongezeka kwa tija katika ugunduzi kwenye tasnia ya uvuvi;

iii) Kufutwa kwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Na.6 ya Mwaka 1980;

iv) Taasisi kuwa na hati miliki ya aina zote za ugunduzi ilioufanya au uliofanywa kwa niaba yake;
v) Kuwepo kwa vituo vya utafiti vitakavyotambulika rasmi na vitakavyoanzishwa kisheria chini ya Taasisi;

vi) Kupanuka kwa matumizi ya sayansi na teknolojia;

vii) Kupanuka kwa wigo wa upatikanaji wa matokeo ya tafitii za uvuzi;

viii) Kukuza ufugaji wa viumbe kwenye maji (aquaculture);

ix) Kupungua kwa makosa yatokanayo na ukiukwaji wa Sheria;

x) Taasisi kuweza kufuatilia watafiti wa ndani na nje ya nchi;

xi) Kuongeza uwajibikaji wa watafiti;

xii) Kuwepo kwa ushiriki wa watafiti binafsi katika utafiti wa uvuvi;

xiii) Taasisi kuwa na mfumo mzuri wa utendaji kazi na

xiv) Kuianisha sheria zingine za uvuvi zilizopo pamoja na sheria mbalimbali zinazogusa sekta ya uvuvi. Sheria hizo ni pamoja na:-

- Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003;

- Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Sura 388;

- Sheria za Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya Mwaka 1994;

- *Territerial Sea and Exclusive Economic Zone Act* 1989;

- Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004;

- Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Na. 7 ya Mwaka 1986;
- Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya Mwaka 2009;

- Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999;

- Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono madhumuni na sababu (*objects and reasons*) ya Serikali kuhusu Muswada huu kwani yanalenga kuimarishas Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania na kuainisha kazi za mamlaka ya

Taasisi kuhusiana na uendeshaji wa utafiti wa uvuvi na utafiti wa ukuzaji viumbe kwenye maji.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na madhumuni na sababu ya Serikali kuleta Muswada huu Bungeni, napenda ieleweke wazi Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 6. ya Mwaka 1980 ambayo imekuwa ikisimamia utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Taasisi hii. Hata hivyo, kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia na ukweli kwamba sheria iliyopo imefanya kazi kwa takribani miaka 36, mapungufu mengi ya kisheria yamejitokeza na kukwamisha baadhi ya shughuli za Taasisi.

**Mheshimiwa Spika,** Wabunge wanaweza kujiuliza kwanini Sheria iliyopo isingeletwa Bungeni kwa utaratibu wa *Miscellaneous Amendments, utaratibu* ambao umekuwa ukitumika kufanya marekebisho kwenye sheria mbalimbali?.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulihakikishia Bunge lako kuwa**,** Kamati imejiridhisha kuwa marekebisho yanayohitajika kwenye Sheria iliyopo ni mengi kiasi kwamba haiwezekani kuifanyia marekebisho sheria iliyopo. Aidha, kwa mujibu wa taratibu za uandishi wa sheria, sheria ikihitaji marekebisho zaidi ya nusu ya sheria yenyewe hakuna budi kuifuta sheria hiyo na kuiandika upya.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huo, Kamati imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa ili kuwezesha nchi kuwa na sheria mpya ambayo itafuta Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Na. 6 ya Mwaka 1980. Na kuanzisha Sheria Mpya ambayo itawezesha kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (*Tanzania Fisheries Research Institute* -TAFIRI), Taasisi ambayo itakuwa chombo huru cha kisheria cha kusimamia na kuratibu utafiti wa uvuvi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kuunga mkono mapendekezo ya sheria inayokusudiwa kutungwa, yapo mambo kadhaa ambayo yaliibua wasiwasi kwa Wajumbe wa Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada na hivyo kuhitaji ufafanuzi wa kina kutoka kwa Serikali. Mambo hayo ni pamoja na:-

- Kwa kuwa Chuo Kikuu cha Sokoine, Chuo Kikuu cha Dar es salaam na Tume ya Sayansi na Teknolojia ni Taasisi za Serikali zilizoanzishwa kisheria na zinamamlaka ya kutoa vibali vya tafiti vya uvuvi, je sheria inayopendekezwa ni kwa kiasi gani imezingatia kutokuwepo kwa mwingiliano wa majukumu.

- Wajumbe walitaka kufahamu sababu za msingi zilizopelekea Serikali kuleta Muswada Bungeni unaotunga jina la Sheria iliyopo? Kamati ilitaka kufahamu kwanini marekebisho yanayopendekezwa yasirekebishwa kupitia utaratibu wa Miscellaneous *Ammendment.*

v Wajumbe walitaka kufahamu utaratibu utakaotumika kuhakikisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya tafiti za uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, Kamati ilifanya kikao cha majumuhisho na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi ambapo Waziri alitoa ufafanuzi wa hoja zote zilizoibuliwa na kufikia mwafaka.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 3.1 SEHEMU YA KWANZA YA MUSWADA INAYOHUSU MASHARTI YA UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** katika sehemu hii ya kwanza, Kamati ilitoa maoni na mapendekezo kwenye maeneo kadhaa yaliyohusu:-

· Kuongeza na kufuta baadhi ya maneno ambayo tafsiri ya maneno hayo ilileta mkanganyiko;

· Kuongezwa kwa vifungu vipya na

· Kusahihisha makosa ya kiuchapaji.

### 3.2 SEHEMU YA PILI YA MUSWADA INAHUSU UANZISHWAJI WA TAASISI NA MAJUKUMU YAKE

**Mheshimiwa Spika,** katika sehemu hii Kamati ilipendekeza:-

· Kuondoa kifungu cha 5(5) ambacho maelezo yake yameshaelezwa kwenye kifungu cha (4) (1) (c);

· Kurekebisha kifungu 6(1) (d) kwa kuondoa maneno **"*carried out within Mainland Tanzania*"** ambayo yamejirudia;

· Kurekebisha kifungu cha 6(3) kwa kuondoa neno "*shall*" ambalo matumizi yake yanalazimisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) kushirikiana na Taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa wakati wa kutekeleza majukumu yake. Badala yake Kamati inapendekeza kuweka neno **"*may*"** ambalo litaiwezesha (TAFIRI) kutekeleza majukumu yake bila kushurutishwa.

**Mheshimiwa Spika,** katika sehemu hii pia kifungu cha 6(3) kipengele (g) hakijaweka uhakika wa kushirikisha Taasisi za Elimu ya Juu zinazojihusisha na tafiti katika uvuvi. Kamati imependekeza kuongezwa kwa kipengele kipya ambacho kitakuwa (h) ambacho kinalenga kuhusisha Chuo Kikuu kinachotambulika nchini kwa kufanya tafiti za uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipendekeza pia katika kifungu cha 6(3) (a) -(f) Kamati imependekeza Sheria sita (6) zinazotajwa kwenye maelezo ya pembeni haziwiani na madhui ya maelezo yaliyotolewa. Hivyo, Kamati imependekeza ili kuleta mantiki sheria zinazotajwa zipangwe kwa kufuatana na kifungu kilichotolewa maelezo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kifungu cha 7 kinaelezea muundo wa Taasisi ambapo Taasisi inaweza kuanzisha kurugenzi, Idara, Kamati za Ufundi au Vitengo kulingana na majukumu yaliyoanishwa kama Bodi itakavyoamua. Kamati imependekeza kwa kuzingatia muundo wa uendeshaji wa shughuli za Taasisi, mpangilio wa Taasisi yoyote uanaelezwa kwa kufuata utaratibu ufuatao: kurugenzi, idara, vitengo na sehemu. Kwa muktadha huo, Kamati inapendekeza kuongezwa kwa neno ***"units"*** baada ya neno ***"department".*** Aidha, Kamati pia imependekeza maneno **"*Techinical Committee*"** yaondolewe na badala yake yayaelezwe kwenye kanuni zitakazotungwa.

## 3.3 SEHEMU YA TATU INAHUSU UTAWALA WA TAASISI

**Mheshimiwa Spika,** sehemu ya tatu (3) inaelezea muundo na utaratibu wa Bodi kutekeleza majukumu yake, ambapo kwa kawaida inakuwa na kifungu kinachoelezea kuanzishwa na Muundo wa Bodi ya Taasisi. Kwa sababu maelezo hayo yameelezwa kwenye Jedwali la Pili, yenye kichwa cha habari kinachosomeka masharti kuhusu Bodi ya Wakurugenzi, Kamati imependekeza maelezo ya maneno hayo yahamishiwe kwenye kifungu kipya cha 8(3).

**Mheshimiwa Spika,** kifugu cha 12 (2) kilikuwa na makosa ya kiuchapaji tu, ambapo Kamati imeshauri kosa hilo lisahihishwe kwa kuondoa herufi ***"n"*** kwenye neno ***"Tanzanian"*** na neno hilo sasa litasomeka "***Tanzania"***.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 12 (b) kinaelezea Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na Watendaji wengine wa Taasisi. Kipengele cha (6) kinaeleza Mkurugenzi Mkuu atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Kamati inapendekeza maneno ***"for another term of five years***" yaondolewe kwa kuwa yanajirudia na badala yake yawekwe maneno ***"for one more term"*** ili kuzingatia kanuni za kiuandishi na kuongeza ladha ya usomaji.

**Mheshimiwa Spika,** katika sehemu hii pia, kifungu cha 14(i) kinaelezea uteuzi wa wakurungezi na wafanyakazi wengine wa Taasisi. Kwa kawaida mpangilio wa muundo wa Taasisi unakuwa na Idara, Vitengo na Sehemu. Neno "units" limesahaulika, Kamati imependekeza liongezwe neno ***"units"*** mara baada ya maneno ***"Heads of Departments"*** na kabla ya maneno ***"and Sections".***

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 14(3) kina makosa ya kiuchapaji ambapo alama ya **mkato (,)** imesahaulika baada ya neno **"basis".** Hivyo, Kamati imependekeza kuweka alama ya **mkato (,)** kati ya maneno **"basis" na "professional"**.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 14(4) kina makosa ya mpangilio ambapo rejea iliyofanywa kwenye kifungu kidogo cha (1) hailengi watumishi waliotajwa kwenye kifungu kidogo (2) hivyo, Kamati imependekeza kifungu hicho kisahihishwe kwa kufanya rejea kwenye kifungu kidogo cha (2) ili kuleta maana iliyokusudiwa na sheria.

## 3.4 SEHEMU YA NNE INAHUSU MAMLAKA NA UENDESHAJI WA TAASISI

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha **20(2)** kinaeleza sharti la Taasisi kuzingatia mtafiti toka nje ya nchi kufanya utafiti kwa kushirikiana na mtafiti toka ndani ya nchi. Wakati kifungu cha **20(3)** kinataka rejea ifanywe kwenye kifungu cha **20(2)** ambacho hakijamaanisha mahitaji ya tafiti. Kamati imependekeza rejea ifanywe kwenye kifungu **19(2)** ambacho kimeorodhesha mapendekezo ya kuzingatia wakati wa kufanya utafiti wa viumbe kwenye maji.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 22 kwenye maelezo ya pembeni kinaelezea usitishwaji wa utafiti, ambapo sehemu ya 22(b) inaeleza endapo mtafiti atashindwa kuwasilisha taarifa inayoridhisha, Taasisi inaweza kusitisha utafiti huo na kumtaka mtafiti kurudisha fedha zote alizopewa kwa madhumuni ya utafiti huo endapo hautakuwa wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imependekeza neno ***"satisfactory"*** liondolewe baada ya neno **"is"** badala yake liwekwe neno ***"prescribed."*** Aidha, kanuni zitakazotungwa zieleze vigezo vya kutambua taarifa ya utafiti unaoridhisha. Vile vile Kamati imependekeza hitaji la kumtaka mtafiti kurudisha fedha zote alizopewa kufanya utafiti liondolewe na badala yake Kamati imependekeza kanuni zieleze kutakuwa na Kamati ya ufundi ambayo pamoja na majukumu megine itafanya kazi ya kufuatilia hatua mbalimbali za utafiti ili kuweza kubaini makosa kabla ya taarifa ya utafiti kufika mwisho.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 25 kwenye maelezo ya pembeni kina makosa ya kiuchapaji katika neno **"Directors",** Kamati inapendekeza neno **"s"** liondolewe ili kuandika lugha ya kiingereza kwa ufasaha.

## 3.5 SEHEMU YA TANO INAHUSU MASUALA YA FEDHA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imependekeza kiongezwe kifungu kipya katika sehemu hii kitakachoeleza kuanzishwa kwa mfuko wa Taifa wa utafiti wa uvuvi. Kamati imefikia uamuzi huu kutokana na ukweli kwamba shughuli za utafiti

zinahitaji fedha nyingi ambazo uzoefu unaonyesha kuwa, fedha zinazopatikana mara nyingi ni fedha za wadau wa maendeleo ambapo fedha hizo hutolewa kulingana na masharti yanayoendana na vipaumbele vyao ambavyo si vipaumbele vya Taifa. Mathalani, sekta ya uvuvi inaweza isiwe kipaumbele cha mipango ya fedha za nchi wahisani.

**Mheshimiwa Spika,** sababu nyingine iliyoifanya Kamati kupendekeza sheria iweke hitaji la kuwa na mfuko maalum wa tafiti za uvuvi ni kutokana na kutotekelezwa kwa azimio la Serikali la kutenga **asilimia 1%** ya pato ghafi la Taifa kila mwaka kwa ajili ya kugharamia tafiti, kwani hadi hivi sasa Serikali imeweza kuchangia chini ya **asilimia 0.5** ya pato ghafi la Taifa kwenye tafiti. Aidha, fedha kidogo zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya tafiti mbalimbali huelekezwa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ambayo hutolewa kwa vigezo vya ushindani ambavyo si lazima vilenge sekta ya uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 28 kinachoelezea uwekezaji kwenye maelezo ya pembeni kinapendekeza kuwa Bodi inaweza kwa kibali cha Waziri, kuwekeza sehemu yoyote ya fedha zilizopo kwenye mfuko wowote wa Taasisi katika uwekezaji kama itakavyoidhinishwa na madhumuni kuhusu uwekezaji wa fedha kwenye Sheria ya Uwekezaji wa Wadhamini.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa kifungu cha 28 hakijazingatia hitaji la kumhusisha Msajili wa Hazina kama Sheria ya Msajili wa Hazina inavyohitaji. Sheria ya Msajili wa Hazina Sura Na. 370 ya Mwaka 2002 na kama ilivyorekebishwa Mwaka 2010, inaipa majukumu Ofisi ya Msajili wa Hazina kusimamia uwekezaji unaofanywa na Taasisi, Mashirika ya Umma na Makampuni yote ambayo Serikali ina hisa.

**Mheshimiwa Spika,** kukosekana kwa kifungu hiki kunamkosesha Msajili wa Hazina nguvu ya kufuatilia miradi ya uwekezaji kuanzia ngazi ya awali (ubunifu wa mradi) hadi katika hatua ya utekelezaji na utendaji.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi zote zilizo chini ya msajili wa Hazina zinatakiwa kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kupata idhini ya Msajili wa Hazina juu ya posho zinazolipwa na Taasisi kwa Bodi na watumishi;
ii. Kupata kibali cha Msajili wa Hazina cha Sera ya uwekezaji;
iii. Mpango wa uwekezaji wa Taasisi uidhinishwe na Msajili wa Hazina;
iv. Kama Taasisi imechukua mkopo kwa ajili ya uwekezaji kwa kutumia dhamana ya mali za Taasisi inatakiwa ipate idhini ya Msajili wa Hazina na

v. Taasisi inatakiwa kuwasilisha Mpango wa Biashara (*Business Plan*) kwa Msajili wa Hazina kwa Uchambuzi na idhini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huo, Kamati imependekeza kiongezwe kifungu kipya kitakachoweka sharti la kumhusisha Msajili wa Hazina katika uwekezaji utakaofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi.

### 3.6 SEHEMU YA SITA INAHUSU MASHARTI YA UJUMLA

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 37(2) kina kosa la kiuchapaji ambapo neno **"Minster"** limeandikwa kimakosa. Kamati imependekeza neno hilo lirekebishwe kwa kuongeza herufi **"i"** kati ya herufi **"n"** na herufi **"s"**, na neno hilo liandikwe kwa ufasaha na kusomeka **"Minister."**

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 38 kinaelezea masharti ya ajira kwa wafanyakazi waliokuwepo kwenye Taasisi ambapo wafanyakazi wote wa Taasisi ya utafiti wa Uvuvi watahamishiwa na kuajiriwa kwenye Taasisi hii kuanzia muda wa kuanza kutumika kwa sheria hii.

**Mheshimiwa Spika,** katika kifungu hiki, Kamati imefanya marekebisho kwa kuondoa maneno **"*be transferred to and be employed by the institute*"** na badala yake kuweka maneno **"*continued to be employees of the institute*"** kwa sababu Taasisi hii haijaanzishwa upya, kilichofanyika ni kuboresha sheria iliyopo kwa kuiandika upya ili kukidhi mahitaji halisi ya uendeshaji na usimamizi wa sekta ya uvuvi nchini na hivyo watumishi walipo wataendelea kuhudumu katika nyadhifa zao.

### 3.7 SEHEMU INAYOHUSU MAJEDWALI - JEDWALI LA PILI

**Mheshimiwa Spika,** kipengele cha 1(1) kinazungumzia masharti kuhusu Bodi ya wakurugenzi na Muundo wa Bodi. Hata hivyo, hakuna kifungu kinachozungumzia muda maalum wa Mwenyekiti wa Bodi kukaa madarakani. Hivyo, Kamati imependekeza kuongezwa kwa kifungu kipya kinachoeleza Mwenyekiti wa Bodi atashika madaraka yake kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu kuanzia tarehe ya kuchaguliwa kwake, na anaweza kustahili kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine kisichozidi miaka mitatu.

**Mheshimiwa Spika,** aya ndogo ya (2), inaeleza Mkurugenzi Mkuu au Afisa yeyote wa Taasisi atakayeteuliwa na Mkurugenzi Mkuu atakuwa Katibu wa Bodi. Kamati inapendekeza maneno ***"or any employee of the Institute appointed by him" na*** badala yake yaweke maneno ***"The Director General shall be the Secretary of the Board".*** Kamati imependeka hivyo kwa sababu Mkurugenzi Mkuu ndiye Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi na ndiye atakayewajibika na kutekeleza maamuzi yaliyofikiwa na Bodi.

**Mheshimiwa Spika,** aya ya 2 inaelezea utaratibu wa kumpata Makamu Mwenyekiti wa Bodi na muda wa kushika madaraka. Ambapo Muswada unaeleza Makamu Mwenyekiti wa Bodi atashika ofisi kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe ya kuchaguliwa kwake, na anaweza kustahili kuchaguliwa tena.

**Mheshimiwa Spika,** hii ina maana kuwa, atachaguliwa kila baada ya mwaka mmoja tofauti na mwenyekiti wa Bodi ambaye atachaguliwa kila baada ya miaka mitatu. Kamati imependekeza ili kuleta tija na ufanisi na kwa kuwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti majukumu yao yanafanana, aya hii iweke hitaji la Makamu Mwenyekiti kushika ofisi kwa miaka mitatu kama ilivyo kwa Mwenyekiti na kwamba anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kisichopungua awamu moja.

**Mheshimiwa Spika,** aya ya 4 inafafanua muda wa Mjumbe wa Bodi kushika ofisi, hata hivyo, muda wa Wajumbe wa Bodi kukaa katika nafasi zao haujaelezwa wazi.

**Mheshimiwa Spika,** kasoro hii ya kisheria isiporekebishwa inaweza kupelekea Mjumbe wa Bodi kudumu katika nafasi aliyonayo kwa muda mrefu na kwa sababu mbalimbali. Hivyo, Kamati imependekeza kama ilivyo kwa muda wa miaka mitatu kwa Mwenyekiti wa Bodi na Makamu Mwenyekiti hivyo hivyo muda huo utumike kwa Mjumbe wa Bodi.

**Mheshimiwa Spika,** aya ya 4(3) inawataka Wajumbe wa Bodi wanaojiuzulu nafasi zao, kutoa taarifa ya maandishi kwa kwa Rais. Aya hii imekosewa kwani aya ya 3 inaeleza kwamba Waziri ndiye mwenye mamlaka ya kuteua Wajumbe wa Bodi, Ikiwa Mjumbe wa Bodi atajiuzulu atalazimika kutoa taarifa ya maandishi kwa Waziri ambae ndio mamlaka yake ya uteuzi. Kwa mantiki hiyo, Kamati imependekeza aya hii iandikwe upya ili kumuwezesha Mjumbe wa Bodi anayejiuzulu kutoa taarifa ya maandishi kwa mamlaka yake ya uteuzi.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumpongeza Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi Mhe. Dkt. Charles Tizeba (Mb), Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi Mhe. William T. Olenasha (Mb), Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. George W. Masaju (Mb), pamoja na wataalamu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wataalamu kutoka Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi Tanzania (TAFIRI). Michango yao na maelezo ya ufafanuzi waliyayatoa kwa Wajumbe wa Kamati yamesaidia Kamati kuwa na ulewa mpana kuhusu shughuli zao na uwiano uliopo na Muswada husika.

Aidha, nachukua fursa hii pia kuwashukuru wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao. Kipekee nawashukuru Ofisi ya Makamu wa Rais – Idara ya Mazingira, Ofisi ya Bunge -kitengo cha Sheria, Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA), Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Chuo Kikuu cha Dar es salaam kupitia Taasisi ya Sayansi za Bahari, Mamlaka ya Usimamizi wa Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority* - DSFA), Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), na Chama cha Wavuvi wa Kati Tanzania Bara (CHAWAKATA) ambao michango yao ya kitaalam imeisaidia Kamati kuboresha Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kuchambua kikamilifu maoni yaliyowasilishwa na wadau na hivyo kuwawezesha kuchambua Muswada kwa kina na hatimaye kukamilisha taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na taadhima, naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb – M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Emmanuel P. John, Mb
4. Mhe. Philipo A. Mulugo, Mb
5. Mhe. Dkt. Immaculate S. Semesi, Mb
6. Mhe. Mahmoud H. Mgimwa, Mb
7. Mhe. Salum M. Rehani
8. Mhe. Khadija H. Aboud, Mb
9. Mhe. Kunti Y. Majala, Mb
10. Mhe. Marwa R. Chacha, Mb
11. Mhe. Mashimba M. Ndaki, Mb
12. Mhe. Oliver D. Semuguruka, Mb
13. Mhe. John J. Mnyika, Mb
14. Mhe. Hamidu H. Bobali, Mb
15. Mhe. James K. Millya, Mb
16. Mhe. Njalu D. Silanga, Mb
17. Mhe. Pascal Y. Haonga, Mb
18. Mhe. Salim M. Bawazir, Mb
19. Mhe. Deo K. Sanga, Mb
20. Mhe. Abdallah H. Ulega, Mb
21. Mhe. Daniel N. Nsazugwako, Mb
22. Mhe. Upendo F. Peneza, Mb
23. Mhe. Haji A. Haji, Mb

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu,napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah pamoja na makatibu wa Kamati Ndg. Virgil Mtui, Ndg. Martha Chassama na Ndg. Rachel Nyega na Watumishi

wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Mary M. Nagu (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**
15 Septemba, 2016

**MWENYEKITI:** Sasa namuita Msemaji wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, napenda kuwasilisha maoni kuhusu Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania ya mwaka 2016 chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Tolea la 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu wa sheria unapendekeza kutungwa kwa Sheria mpya ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, ikiwa na madhumuni ya kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania na kuainisha kazi na mamlaka ya taasisi na uendeshaji wa utafiti wa uvuvi na utafiti wa ukuzaji wa viumbe kwenye maji na kuainisha masuala mengine yanayohusiana na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Uanzishwaji wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(TAFIRI)* kwa mara ya kwanza ilitungwa na Bunge la Tanzania hapo mwaka 1980, na sheria hiyo ikapewa Namba sita (6) ambayo ilishughulikia uendeshaji pamoja na usimamizi wa utafiti wa uvuvi Tanzania. Hivyo basi, ingekuwa ni vyema kama mapungufu ambayo Serikali imeyabaini kwamba ndiyo yamepelekea sheria hiyo kufutwa kabisa na kutungwa sheria mpya, ili Waheshimiwa Wabunge wawe na ufahamu wa nini hasa kilikuwa kikikwamisha utendaji mzuri wa kazi wa *TAFIRI*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, sheria hiyo namba 6 ya Mwaka 1980, ilikuwa inatumika Tanzania nzima, na kwa sababu hiyo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Utafiti wa Uvuvi na Viumbe wa Baharini *(Institute of Marine Sciences – IMS)* kikawa na tawi lake Zanzibar kwa minajili ya kuendeleza utafiti wa viumbe wa baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naenda kuwapitisha Waheshimiwa Wabunge, mapitio ya vifungu katika muswada husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu hiyo ya tafsiri, muswada umeshindwa kugundua kwamba katika shughuli zifanyikazo baharini, si tu kwa samaki na kwa mazao yake tu, bali kuna mazao ya mimea ipatikanayo baharini kwa kitaalam kama *aquatic flora*. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka maneno *aquatic flora* kwenye tafsiri ya neno *fisheries*, kwani kwenye tafsiri ya neno *fishing* tayari maneno hayo yamekwishawekwa. Sambamba na hilo maneno hayo yatolewe tafsiri kwenye muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 4(3) kinasema kwamba, nina *quote; 4.-(3) Notwithstanding the provisions of this section, the Attorney General shall have the right to intervene in any suit or matter instituted by, or against the institute.*

Mheshimwia Mwenyekiti, aidha, kifungu cha 4(4) kinasema kwamba, nina *quote; 4.-(4) Where the attorney General intervenes in any matter in pursuant of sub section (3), the provision of the Government Proceeding Act shall apply in relation to the proceedings of that suit or matter as if it had been instituted by, or against the Government.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 4(2)(b) kinasema kwamba, nina *quote; 4.-(2)(b) In its corporate name, be capable of suing and being sued.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ni kifungu kidogo cha 6(1)(k) kinasema, na nina *quote*; 6.-(1)(k) *Do anything or enter into any transaction which, in the opinion of the Board, is necessary or desirable for the purposes of the better performance of the functions of the Institute under this Act.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba vifungu hivyo tajwa hapo juu vinachanganya kwani taasisi ni chombo hodhi na chenye mamlaka kamili, sasa inakuwaje pale kinapotakiwa kushitaki au kushtakiwa iwe kana kwamba, inayoshitaki au kushtakiwa ni Serikali na masharti ya kuishtaki Serikali ndiyo yatumike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushahidi huo wa wazi ni kuwa Serikali inaonesha kwamba, haina nia njema na wadau wa sheria hii, kwani kuna uwezekano wadau wasiridhike na huduma itolewayo na taasisi na hivyo ikawalazimu kuishtaki, jambo ambalo ni haki yao ya kimsingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa kuangalia vyema vifungu husika Kambi Rasimi ya Upinzani inashauri kwamba kifungu cha 4(3), 4(4) na 4(5) vifutwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 6, kuhusiana na kazi za taasisi kuwa pamoja na kazi nyingine kifungu kidogo cha (2)(b) kinasema kwamba na nina *quote; 6.-(2)(b) Uundertake the collection, preparation, publication and*

*distribution of statistics relating to fisheries and the fishing industry, and promote and develop guidelines and training in fisheries.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba, kifungu hiki kinatoa uhuru uliopitiliza na hivyo hakuna chombo kinachofanya usimamizi. Haiwezekani taasisi yenyewe ikawa kila kitu na kosa hili ni sawa na lile lililofanywa na kuipa Wizara ya Elimu kuwa ni kila kitu katika elimu, kwa maana ya kumiliki shule, kusajili shule, kutunga mitaala, kufundisha, kukagua mashule, kusimamia ubora wa shule na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara ya uhuru huo ni kwamba, sasa hivi shule za Serikali ndizo ambazo hazina vyoo, hazina madawati, hazina vyumba vya madarasa wakati shule binafsi vyote hivyo si tatizo. Na hiyo ni kwa kuwa Wizara ya elimu haifuati utaratibu *(check list)* waliojiwekea wakati wa uanzishwaji wa shule za Serikali. Hivyo basi, kuna uwezekano mkubwa sekta ya uvuvi ikawa inatoa taarifa za kuwafurahisha watu, lakini hazina uhalisia kwani mtengeneza takwimu ndiye huyo huyo mtoa takwimu. Ni vyema sheria ikaweka angalizo kuzuia ukiritimba huu unaopendekezwa katika muswada huu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 7 cha muswada kinahusu uwezo wa taasisi kuanzisha kurugenzi, idara, kamati za kiufundi na vitengo mbalimbali kama Bodi itakavyoona inafaa. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kunukuu usemi wa kiingereza usemao kuwa *absolute power corrupts absolutely*. Mamlaka haya ya bodi inaweza kuwa ni chanzo cha kutengeneza idara za kiundugu au kikabila na jambo hili linaweza kuwavunja moyo watendaji wenye sifa na hivyo ukawa mwanzo wa taasisi kufanya kazi chini ya kiwango. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Idara kuu ya Utumishi wa Umma ndiyo iwe mamlaka pekee yenye uwezo wa kushauri na kupendekeza kuanzishwa kwa muundo mzima wa kiutendaji kwa taasisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 8(3) kinachotambua uwepo wa jedwali la pili la sheria hii linaloweka masharti kuhusu Wajumbe wa Bodi; kifungu cha 8(1)(a) cha Jedwali kinasema kuwa Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais na kifungu cha 2 kinahusu upatikanaji wa Makamu Mwenyekiti wa Bodi na kifungu kiko wazi kabisa kuwa Makamu Mwenyekiti atachaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe.

Kwa mantiki hiyo ya upatikanaji wa Makamu Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa Mwenyekiti pia achaguliwe na Wajumbe wenyewe kutoka miongoni mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 11 kinahusu posho na marupurupu kwa Wajumbe wa Bodi. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kufutwa kwa

maneno, na *quote:-"upon the recommendation of the board,"* na kumwachia Waziri na Msajili wa Hazina kupanga marupurupu yao kwa mujibu wa kanuni na sheria zinavyohitaji. Kwa kutoa nafasi wajumbe kuamua ni sawa na hakimu kuitolea hukumu kesi inayomhusu yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu vya 13 na 14(1) vinaonesha dhana ya uteuzi. Kwa kuifanyia tafakuri dhana hiyo ya uteuzi kwa mazingira ya Tanzania ni kwamba wateuliwa hata kama wana sifa za kazi husika, lakini bado wanafanyakazi kwa maelekezo na sio kwa mujibu wa matakwa ya kazi zao zinavyohitaji. Kwa muktadha huo Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri nafasi zote za kiutendaji zipatikane kwa njia ya ushindani wa wazi *(recruit upon competition)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi mara zote wanaochukuliwa ni wale waliokaribu au wanaojulikana na wahusika na hivyo kuwanyima fursa wale wote ambao hawafahamiki lakini wana sifa na uwezo unaohitajika kwa nafasi kazi zinatakiwa kujazwa. Hivyo basi, masharti ya kifungu kidogo cha 14(3) yatumike pia kwa upatikanaji wa Kaimu Mkurugenzi, kifungu cha 13 na kwa Wakuu wa Idara na Vitengo, kifungu cha 14(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 19 kinachohusu mtafiti wa ndani anayetaka kufanya utafiti kwamba anatakiwa kuwa na andiko linalooonesha eneo analotaka kulifanyia utafiti na baadae apeleke andiko hilo kwa taasisi ili apewe idhini ya kuendelea au kutokuendelea na kifungu cha 19(4) kinahusiana na kupewa fedha za kufanyia utafiti.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kuna watafiti hawahitaji kupewa fedha za kufanya utafiti toka kwenye taasisi hii husika, hivyo ni muhimu kifungu hiki kikawa wazi kama ni kutoa taarifa tu kwa taasisi au kuomba ufadhili. Hivyo basi, itakuwa ni vyema kwa watafiti ambao hawahitaji ufadhili wa taasisi wasihusike na masharti ya Kifungu cha 19(3) na 19(4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa uchambuzi huo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MAONI YA MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI MHESHIMIWA MAGDALENA HAMISI SAKAYA (MB), KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI TANZANIA, WA MWAKA 2016 *(The Tanzania Fisheries Research Institute Act, 2016)***

*(Chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016)*

A. **UTANGULIZI:**

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu wa sheria unapendekeza kutunga kwa sheria mpya ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania ikiwa na madhumuni ya kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania na kuainisha kazi na mamlaka ya Taasisi na uendeshaji wa utafiti wa uvuvi na utafiti wa ukuzaji wa viumbe kwenye maji na kuainisha masuala mengine yanayohusiana na hayo.
Mheshimiwa Spika,

Sheria ya uanzishwaji wa taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) kwa mara ya kwanza ilitungwa na Bunge la Tanzania hapo mwaka 1980, na sheria hiyo ikapewa namba 6 ambayo ilishughulikia uendeshaji pamoja na usimamizi wa utafiti wa uvuvi Tanzania. Hivyo basi, ingekuwa ni vyema kama mapungufu ambayo Serikali imeyabaini kwamba ndiyo yamepelekea Sheria hiyo kufutwa kabisa na kutungwa sheria mpya ili Waheshimiwa Wabunge wawe na ufahamu wa nini hasa kilikuwa kikikwamisha utendaji kazi mzuri wa TAFIRI.

**Mheshimiwa Spika,** ukweli ni kwamba sheria hiyo namba 6 ya mwaka 1980 ilikuwa inatumika Tanzania nzima na kwa sababu hiyo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Idara ya Utafiti wa Uvuvi na Viumbe wa Baharini kikawa na Tawi lake Zanzibar kwa minajili ya kuendeleza utafiti wa viumbe wa baharini.

**B. MAPITIO YA VIFUNGU KATIKA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika,** katika sehemu hiyo ya tafsiri, muswada umeshindwa kugundua kwamba katika shughuli zifanyikazo baharini, sio tu kwa samaki na mazao yake tu, bali kuna mazao ya mimea ipatikanayo baharini kwa kitaalam kama "aquatic flora". Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka maneno "aquatic flora" kwenye tafsiri ya neno fisheries, kwani kwenye tafsiri ya neno "fishing" tayari maneno hayo yamekwisha wekwa. Sambamba na hilo maneno hayo yatolewe tafsiri kwenye muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 4 (3) kinasema kwamba ***"Notwithstanding the provisions of this section, the Attorney General shall have the right to intervene in any suit or matter instituted by, or against the institute". Aidha,*** kifungu cha 4(4) kinasema kwamba ***"where the attorney General intervenes in any matter in pursuant of sub section (3),the provision of the Government Proceeding Act shall apply in relation to the proceedings of that suit or matter as if it had been instituted by, or against the Government."***

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 4(2) (b) kinasema kwamba ***"in its corporate name, be capable of suing and being sued".*** Sambamba na hilo ni kifungu kidogo cha 6(1) (k) kinasema kuwa, ***"do anything or enter into any transaction which, in the opinion of the Board, is necessary or desirable for the purposes of the better performance of the functions of the Institute under this Act."***

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba vifungu hivyo tajwa hapo juu vinachanganya kwani kama Taasisi ni chombo hodhi na chenye mamlaka kamili, sasa inakuwaje pale kinapotakiwa kushtaki au kushtakiwa iwe kana kwamba inayoshitaki au kushtakiwa ni Serikali na masharti ya kuishtaki Serikali ndiyo yatumike.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ushahidi huo wa wazi ni kuwa Serikali inaonesha kwamba haina nia njema na wadau wa sheria hii, kwani kuna uwezekano wadau wasiridhike na huduma utolewayo na taasisi na hivyo ikawalazimu kuishtaki, jambo ambalo ni haki yao ya kimsingi. Kwa kuangalia vyema vifungu husika Kambi Rasimi ya Upinzani inashauri kwamba kifungu cha 4(3), 4(4) na 4(5) vifutwe.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 6 kuhusiana na kazi za taasisi kuwa pamoja na kazi nyingine kifungu kidogo cha (2)(b) kinasema kwamba, ***"undertake the collection, preparation, publication and distribution of statistics relating to fisheries and the fishing industry, and promote and develop guidelines and training in fisheries."***

**Mheshimiwa Spika,** kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kifungu hiki kinatoa uhuru uliopitiliza na hivyo hakuna chombo cha kuwa kinafanya usimamizi, haiwezekani taasisi yenyewe ikawa kila kitu na kosa hili ni sawa na lile lililofanywa la kuipa Wizara ya Elimu kuwa kila kitu katika Elimu, kwa maana ya kumiliki shule, kusajili shule, kutunga mitaala, kufundisha, kukagua mashule, kusimamia ubora wa elimu n.k.

**Mheshimiwa Spika,** Madhara ya uhuru huo ni kwamba sasa hivi shule za Serikali ndio hazina vyoo, hazina madawati, hazina vyumba vya madarasa wakati shule binafsi vitu vyote hivyo sio tatizo na hiyo ni kwa kuwa Wizara ya elimu haifuati utaratibu (***check list***) waliojiwekea wakati wa uanzishwaji wa shule za Serikali.

Hivyo basi, kuna uwezekano mkubwa Sekta ya Uvuvi ikawa inatoa taarifa za kuwafurahisha watu lakini hazina uhalisia kwani mtengeneza takwimu ndiye huyo huyo mtoa takwimu. Ni vyema sheria ikaweka angalizo kuzuia ukiritimba huu unaopendekezwa katika muswada huu wa sheria. Kwa ufupi kazi za taasisi kifungu cha 6 kwamba hakuna haja ya kuwa na wizara upande wa Uvuvi kwani taasisi kwa mujibu wa muswada huu tayari inashughulika na kila kitu.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 7 cha muswada kinachohusu uwezo wa taasisi kuanzisha Kurugenzi, Idara, Kamati za kiufundi na vitengo mbalimbali kama bodi itakavyoona inafaa. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kunukuu usemi wa kiingereza usemao kuwa **"absolute power corrupts absolutely"** mamlaka haya ya bodi inaweza kuwa ni chanzo cha kutengeneza idara za kiundugu au kikabila na jambo hili linaweza kuwavunja moyo watendaji wenye sifa na hivyo ukawa mwanzo wa taasisi kufanyakazi chini ya kiwango. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Idara kuu ya Utumishi wa umma ndiyo iwe mamlaka pekee yenye uwezo wa kushauri na kupendekeza kuanzishwa kwa muundo mzima wa kiutendaji kwa taasisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 8(3) kinacho tambua uwepo wa jedwali la pili la sheria hii linaloweka masharti kuhusu wajumbe wa bodi. Kifungu cha 1(1)(a) cha Jedwali kinasema kuwa Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais na kifungu cha 2 kinahusu upatikanaji wa Makamu Mwenyekiti wa Bodi, na kifungu kiko wazi kabisa kuwa Makamu Mwenyekiti atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe. Kwa mantiki hiyo ya upatikanaji wa Makamu Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa Mwenyekiti pia achaguliwe na wajumbe wenyewe kutoka miongoni mwao.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 11kinahusu posho na marupurupu kwa wajumbe wa bodi, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kufutwa kwa maneno, **"upon the recommendation of the board"** na kumwachia Waziri na Msajili wa Hazina kupanga marupurupu yao kwa mujibu wa kanuni na sheria zinavyohitaji, kwa kutoa nafasi wajumbe kuamua ni sawa na hakimu kuitolea hukumu kesi inayomhusu yeye mwenyewe.

**Mheshimiwa Spika,** vifungu vya 13 na 14(1) vinaonesha dhana ya uteuzi, kwa kuifanyia tafakuri dhana hiyo ya uteuzi kwa mazingira ya Tanzania ni kwamba wateuliwa hata kama wana sifa za kazi husika lakini bado wanafanyakazi kwa maelekezo na sio kwa mujibu wa matakwa ya kazi zao zinavyohitaji. Kwa muktadha huo Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri nafasi zote za kiutendaji zipatikane kwa njia ya ushindaji wa wazi (recruit on open competitive).

**Mheshimiwa Spika,** uteuzi mara zote wanaochukuliwa ni wale waliokaribu au wanaojulikana na wahusika na hivyo kuwanyima fursa wale wote ambao hawafahamiki lakini wana sifa na uwezo unaohitajika kwa nafasi kazi zinatakiwa kujazwa. Hivyo basi, masharti ya kifungu kidogo cha 14(3) yatumike pia kwa upatikanaji wa Kaimu Mkurugenzi Mkuu kifungu cha 13 na kwa wakuu wa Idara na vitengo kifungu cha 14(1).

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 19 kinchohusu mtafiti wa ndani anayetaka kufanya utafiti, kwamba anatakiwa kuwa na andiko linaloonesha eneo analotaka kulifanyia utafiti na baadae apelike andiko hilo kwa Taasisi ili apewe idhini ya kuendelea au kutokuendelea, na kifungu cha 19(4) kinahusiana na kupewa fedha za kufanyia utafiti. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kuna watafiti hawahitaji kupewa fedha za kufanya utafiti toka kwenye Taasisi, Hivyo ni muhimu kifungu hiki kikawa wazi kama ni ***kutoa taarifa***(***informing the institute***) tu kwa taasisi au **kuomba ufadhili (seeking approval to be funded).**

Hivyo basi, itakuwa ni vyema kwa watafiti ambao hawahitaji ufadhili ya taasisi wasihusike na masharti ya vifungu vya 19(3) na 19(4).

**Mheshimiwa Spika, b**aada ya kutoa uchambuzi huo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**……………………..**
**Dr.Sware Semesi (Mb)**
**K.n.y Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-**
**Wizara ya Kilimo,Mifugo na Uvuvi.**
**14 Septemba, 2016**

**MWENYEKITI:** Ahsante Dkt. Sware.

Waheshimiwa Wabunge, orodha tunayo, ningependa kuishauri Serikali kuwa mjiandae, mnaweza mka-*wind up* kesho asubuhi. Kwa hiyo, katika michango hii *just bear it in mind* inawezekana mka-*wind up* asubuhi na jioni

tukaingia moja kwa moja kwenye Kamati ya Bunge. Nawashauri wale Waheshimiwa ambao wana *ammendments,* mnaweza mkazipelekeka vilevile kwenye Kamati, ili mmalizane na Serikali hukohuko, kuepusha kuwa na mijadala mirefu sana ndani ya Bunge na kumaliza Bunge usiku sana. Kwa hiyo, huo ni ushauri, tutatizama itakavyokuwa!

## MWONGOZO WA SPIKA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba Mwongozo wako. Katika Hotuba za Kamati, nikitolea mfano Hotuba juu ya Muswada wa Taasisi ya Kilimo, ukurasa wa pili inaeleza kwamba hata hivyo kabla ya kuanza kuwasilisha maoni ya Kamati, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Jedwali la Marekebisho mlilopewa ni matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati kutokana na muswada wenyewe na maoni ya wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpaka sasa tunavyozungumza hayo majedwali ya marekebisho ambayo tunasema hapa tumepewa hatujapewa bado. Na litakuwa jambo jema kama Wabunge wanakwenda kuchangia huku wakiwa na ushahidi kama mambo ambayo Kamati imeeleza kuwa tayari Serikali imeyakubali yaonekane kweli kwenye Jedwali la Marekebisho kwamba kweli Serikali imeyakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mwongozo wako, ili haya Majedwali ya Marekebisho yaweze kutolewa, haya ya Serikali. Kwa sababu ni *commitment* ya kwamba yanakubaliana na maoni ya Kamati na kwamba yanapaswa kutolewa kabla ya mjadala.

**MWENYEKITI:** Kulikuwa na tatizo la uchapishaji, marekebisho yote Serikali italeta Bungeni.

Waheshimiwa tunaendelea, tuna wachangiaji, naanza na mchangiaji Mheshimiwa Mashimba Ndaki, ajiandae Mheshimiwa Salim Rehani.

Mheshimiwa Ndaki hayupo!

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Enhee!

**TAARIFA**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa yapo kwenye taarifa tuliyopewa na Kamati ambayo ukifungua mwishoni utayakuta.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa siikubali kwa sababu Taarifa ya Kamati inaeleza yale ambayo Serikali imependekeza kwa Kamati, na kwamba Serikali imeelekea kuyakubali. Sasa ili Bunge lie na ushahidi wa kwamba Serikali imeyakubali ni lazima kuwe na Jedwali la Serikali liwepo Mezani lenye ushahidi wa kwamba, Serikali imeyakubali hayo marekebisho. Na hili litaepusha Waheshimiwa Wabunge kuchangia mambo ambayo pengine Serikali imeshayakubali na imeshayaingiza yakarudiwa kwenda kujadiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni jambo la Kikanuni tu kwamba jedwali hili litolewe kwa Wabunge kabla ya mjadala kuendelea. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika nafikiri nimesema vizuri, Majedwali yanaandaliwa na huo ndio Mwongozo wangu toka ulivyotaka kujua. Serikali inaandaa na kila mtu atapata jedwali kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa Ndaki!

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ili niweze kuchangia miswada hii miwili iliyowekwa mbele yetu; Muswada wa *TARI* na wa *TAFIRI.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kuleta miswada hii miwili ambayo itasaidia. Sisi kama wawakilishi wa wananchi tuna matumaini kwamba inaweza ikatusaidia sana huko tunakofanya kazi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze tu na maelezo na maoni yangu ya jumla kuhusiana na miswada yote miwili. La kwanza ni kuhusiana na *TAFIRI* na *TARI;* upande wa *TAFIRI* muswada wake unasema utakuwa na *Deputy Director General* na upande wa muswada ule wa *TARI* wenyewe utakuwa tu na *Director General,* hayupo *Deputy Director General.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimejaribu kuangalia na kulinganisha hizi taasisi mbili ukubwa wake, na kuona kwamba ukiangalia *TARI* ni kubwa kuliko *TAFIRI* kwa maana ya idadi ya watu na kwa maana ya taasisi zake pia. *TARI* ina taasisi 16, *TAFIRI* itakuwa na taasisi nne, lakini *TAFIRI* ina *Deputy Director General*

ambaye kwenye muswada wake wamesema atafanya kazi kama zile atakazokuwa akifanya *Director General.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa ninasita kidogo hapa kwa sababu taasisi hizi ukiziangalia ni taasisi za kitaalamu, na ni taasisi ambazo zinatakiwa zitoe mazao yatakayotusaidia sisi kama nchi kitaalam. Sasa kuzijaza na watu kama *TAFIRI* kuiweka na watu wawili ambao hata ujuzi wake na weledi na uwezo wao ni kama unalingana naona kama ni kuipa mzigo *TAFIRI* kubeba watu wawili viongozi wakubwa badala ya kuiacha tu na *Director General* peke yake.

Pia hili linasababisha kubebesha watu wetu mzigo kwa sababu, hizi taasisi zinapata ruzuku kutoka kwa Serikali. Na ruzuku inapatikana kutokana na kodi ambazo wananchi wa nchi hii wanatoa. Sasa kwa nini tusiwe tu na *Director General* kwa *TARI* kama walivyoainisha kwenye sheria, lakini pia kwa *TAFIRI* tuwe na *Director General* tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu *Deputy Director General* hatuna sababu ya kuwanaye kwa sababu mimi naona ni kama tu tunaongeza mzigo kwa taasisi hii ambayo ni ndogo, itakuwa na taasisi nne na wafanyakazi wake watakuwa wachache, lakini chini ya Mkurugenzi Mkuu, pia wapo wakurugenzi wengine ambao wanaweza wakamsaidia kazi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni suala la *succession plan w*akurugenzi watakaokuwa chini ya Mkurugenzi Mkuu wanatosha kabisa kuwa *succeeded* kupata cheo cha Mkurugenzi Mkuu baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo ni *observation* yangu ya kwanza. Nilikuwa naomba kwamba, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*conclude* atuambie ni kwa nini sasa *TAFIRI* inakuwa na *Deputy Director* halafu *TARI* ambayo ni taasisi kubwa inakuwa na *Director* peke yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nililotaka kusema la jumla ni matokeo ya tafiti kutokana na sheria hizi tunazopitisha. Tuna matatizo makubwa kwenye sekta za kilimo na uvuvi kwa ujumla. Tuna matatizo ya masoko, tuna matatizo ya mbegu, ya viuatilifu na matatizo mengine mbalimbali ambayo tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilidhani kwamba, kwa kuwa na taasisi hizi ambazo sasa, kwa mfano *TARI* ni taasisi itakayokuwa huru ambayo itatoka kuwa Idara ya Wizara, itakuwa taasisi inayojitegemea vivyo hivyo *TAFIRI;* kwamba sheria hii sasa ingeainisha tafiti zitakazofanyika, matokeo yake yanaweza yakafikaje kwa wadau; kwa wakulima kwa mfano tutapata faida gani za moja

kwa moja kutokana na kuwa na Taasisi hii ya Kilimo kisheria? Faida zinazotokana na upatikanaji wa masoko, mbegu zilizo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumepata matatizo ya mbegu za mazao mbalimbali, mazao ya biashara lakini pia mazao ya chakula; tuna matatizo makubwa hapa. Sasa mimi nlitegemea sheria hizi mbili tunazotaka kuzipitisha zingeainisha ni kwa namna gani tafiti zake zinawafikia walengwa kwa muda unaotakiwa, lakini pia zinatoa matokeo ambayo yanagusa wananchi wetu. Mimi natoka sehemu wanayolima pamba, kuna wakati wakulima wetu wanapewa mbegu za pamba ambazo hazioti, lakini zinapitia kwa hawa talaam na zimepitia hii michakato yote hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa najaribu kuangalia sheria hii sasa inatusaidiaje sisi kama wawakilishi wa wakulima kupata mbegu bora, masoko kwa ajili ya mazao yetu? Tumezungumza hapa siku chache zilizopita kuhusiana na mazao ambayo yanaozea kwenye mashamba ya wakulima wetu. Sasa tafiti hizi zinatusaidiaje? Kwa sababu tunapitisha hizi sheria lakini sasa zitagusaje watu wetu kihalisia kuliko tu kuziacha kitaalam namna hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nimejaribu kulilinganisha kwenye sehemu zote mbili, kwenye muswada wa *TAFIRI* na *TARI* ni kipengele kile cha kukopa na kuwekeza. Kipengele hiki cha kukopa na kuwekeza mapendekezo ya Kamati yamesema vizuri kwamba kukopa na kuwekeza kwa taasisi ya *TAFIRI* kwa mfano Kamati wamesema ni muhimu kwamba Msajili wa Hazina aweze kuhusishwa. Lakini upande wa ule Muswada wa Kilimo haujasema chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza kwamba pia huu Muswada wa Kilimo pia useme wazi kwamba Msajili wa Hazina anahusishwaje inapokuja suala hasa la kuwekeza. Kwa sababu mali hizi ni taasisi za Serikali na mwenye kujua mali na thamani yake kwa upande wa Serikali ni Msajili wa Hazina. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwamba kwa upande huo pia kipengele upande wa *TARI* wamuhusishe Msajili wa Serikali ili kujua uwekezaji unaowekwa ni kiasi gani na anaweza kuufuatilia kwa namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha mwisho ni sehemu ya tano ya muswada ule wa *TARI* kipengele kile cha nane kinasema kwenye uwakilishi wa bodi atakuwepo mwakilishi mmoja kutoka kwa wakulima. Kwa nini awe mmoja na wasiwe wawili kama ambavyo Kamati imependekeza? Mimi nashauri kwamba wawe wawili kama ambavyo Kamati imependekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwenye kipengele cha tisa wamependekeza pia awepo mwakilishi mmoja kutoka kwa wale wa wawakilishi wa *Agri-business Organizations.* Mimi pia hapo nilikuwa napendekeza wawepo

wawakilishi wawili, kwa sababu ukizingatia pia maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani hao wanaokuwa ni *members* wa Bodi kwenye *TARI* wengi wao ni wafanyakazi kwenye Serikali. Sasa tukiwa na wawakilishi pia wanaoongezeka kutoka kwa wakulima na hawa wanaowakilisha watu wanofanya shughuli zinazohusiana na kilimo lakini za kibiashara na wenyewe wakaongezeka tutaweka uhusiano ambao utakuwa ni mzuri kwenye Bodi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu yalikuwa ni hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Salim Rehani, jiandae Mheshimiwa Zuberi Kuchauka. Nafikiri Mheshimiwa Zuberi utakuwa jioni.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kupata fursa hii ya kuchangia hii miswada miwili iliyo mbele yetu. Kwanza nishukuru Mungu kwamba Serikali imeshtuka na kuweza kujitambua katika eneo hili. Na mimi ni-*declare interest* kwamba na mimi ni mtafiti na nimefanya hii kazi kwa muda wa miaka tisa, najua machungu na najua kazi inayotakiwa kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaloweza kusema la mwanzo, sheria hii ndiyo roho ya nchi ya uhai wa chakula cha nchi hii ya Tanzania. Dunia yoyote bila ya kuwa na utafiti/watafiti haiwezi kupata maendeleo. Tanzania tumekuwa siku zote watafiti kama watoto waliokuwa yatima; kila mmoja anafanya shughuli zake kwa mujibu wa anavyoona yeye na kwa mujibu wa fedha alikozipata. Lakini kuweko na sheria hii utaweza kuifanya nchi kuwa na mwelekeo na kuratibu hizi tafiti mbalimbali ambazo zimeshafanywa, na nyingine ambazo zinahitajika kufanywa katika utaratibu ambao wa kuleta maendeleo au tunaita *research impact. Act* hii imeweza kutuonesha mwelekeo sasa vipi tuweze kuelekea na vipi tuweze kujipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulilokuwa nalo ndani ya nchi hii watafiti wamekuwa hawana *coordination* ya kuweza kujua kwamba huyu mtafiti anatakiwa afanye utafiti huu kwa ajili gani. Matokeo yake siku zote tunapata tatizo kubwa la asilimia 80 ya mbegu ambazo tunatumia katika mazao yetu tunaagiza nje au mbegu hizo zinatumika zile ambazo zilikuwa zimeshatumika miaka mitatu ama minne nyuma, yaani wakulima wetu bado wana ule utamaduni wa kutumia mbegu wanazoweka katika moshi; zikapigwa na moshi kwa muda wa mwaka mzima baada ya mwaka unaofuata zikaenda shambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa utafiti huu kutaweza sasa kuratibu utaratibu mzuri wa upatikanaji wa mbegu katika vituo vyetu mbalimbali vya uzalishaji mbegu lakini vile vile itawasaidia watafiti na Sheria ile ya *Breeding Act* kuweza kkujitambua na kutoa mbegu hizi kwa mujibu wa mahitaji ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi itawasaidia wajasiriamali mbalimbali waliohusiana na utafiti kuweza kupata soko la uzalishaji wa mbegu ambazo zitaweza kutumika nchini na kupunguza tatizo la upatikanaji wa mbegu mbovu, zisizo na viwango na zisizotoa mazao ambayo yanalingana na uzalishaji kwa eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linajitokeza, sheria hii itaweza kuisaidia nchi kuanza sasa kupata fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali vya taasisi vya utafiti duniani. Kuna mashirika manne makubwa duniani ambayo wao kazi yao kubwa kusaidia taasisi za utafiti. Kwa hiyo, kuanzishwa kwa mfuko wa utafiti utasaidia mashirika yale kuitambua nchi hii kwamba ina sheria ya utafiti na kuweza kuleta fedha zao ambazo zitawasaidia watafiti kwa kiasi kikubwa kufanya shughuli zao na kuleta mabadiliko chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hilo tu, hata kwenye vyuo vyetu vikuu ambavyo kwa kiasi kikubwa ndizo zinazoratibu na kufanya tafiti nyingi ambazo hazichukuliwi zikafanyiwa kazi. Sheria hii itaweza kuvifanya vile vyuo zile tafiti zao zitambulike na ziweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa lililokuwepo ni *database* ya utafiti haipo, kila mmoja amekusanya *data* zake kwa mujibu wa vile alivyokuwa nazo yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kubwa linalotakiwa hapa ni kuwepo na uratibu mzuri wa Mkurugenzi huyu wa *TARI* kuweza kukusanya taarifa za tafiti mbalimbali katika vituo mbalimbali na kuweza kuzi-*publish* lakini nyingine kuanza kuzifanyia kazi kama zilivyopendekezwa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa hivi ni msimu wa kilimo katika maeneo yetu mbalimbali, Tanzania hii mikoa minne tu ndio yenye uhakika wa kupata mvua ya milimita 800 kwa mwaka, mikao iliyobaki mvua zake ni za kubahatisha; zipo chini ya milimita hizo 700 na wakati mwingine zinanyesha katika mazingira tofauti kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa utafiti kila Mkoa utaweza kusaidia sasa watu hawa wanatakiwa wapande zao gani, kwa wakati gani na kiwango gani ambacho cha mazao kinachoweza kutoka katika yale mashamba kulingana na uwezo wa uzalishaji na nyenzo zile alizozipata za kuzalishia. Lakini vilevile itaisaidia Serikali kuweza kuweka nguvu katika ile Mikoa ambayo ina uhakika wa uzalishaji, ili kupeleka mbolea na pembejeo nyingine kwa wakati unaofaa na kuwa na uhakika wa uzalishaji kuliko hali ilivyo sasa hivi, kila mmoja anakwenda kulingana na mazingira yanayomkabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nimeliona na nililotaka kuchangia ni suala zima la kazi za hizi taasisi. Taasisi ina kazi nyingi na ni za msingi. Kwa bahati na mimi ni mjumbe wa Kamati hii, nilichangia mengi katika Kamati lakini yapo yale ambayo nilikuwa nataka kukazia tu. Moja kati ya kazi ambayo nlitakiwa kuhakikisha ina-*coordinate* ni kukusanya *database* ya utafiti iweze kuwa alive, iweze kuwa *strong* na kuwe na mfumo mzima wa upashanaji habari; hiki ndicho kitu kitakachoweza kutusaidia. Kwa sababu wavumbuzi ni wengi, wanavumbua vitu vingi lakini hakuna taarifa zinazotangzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, juzi kulikuwa na kikao cha wavumbuzi waliokuwa wamefanya tafiti za kuzalisha miche bora ya kahawa ambayo inakubali katika mazingira ya baridi kama maeneo ya Arusha, Moshi, Mbeya na maeneo mengine ambayo yana baridi ambayo inafikia mpaka degree 18 na miche ile inafanya uzalishaji ulio mzuri. Taarifa zile ni nzuri, miche ile inakomaa au inazaa kwa muda mfupi lakini vile vile inastahamili yale magonjwa ambayo yanasababisha miche ile ieweze kufa. Kwa mfano *leaf mina* ni tatizo kubwa, *coffee stem borer,* wale ambao wana athiri katika maeneo yale, wamefanyia utafiti mzuri, wamepata tiba ya kuweza kuhakikisha kwamba miche ile imekuwa *resistance* na mazingira yetu. Kinachotakiwa sasa hivi ni kuwepo uhakika sasa wa kuisambaza kwa wakulima. Lakini vilevile kuwepo na taaluma ambayo itatolewa na mabwana shamba na mabibi shamba katika maeneo mbalimbali ili uzalishaji uweze kubadilika baada ya miaka mitatu. Miche mingi tuliyokuwanayo sasa hivi inazaa hasa kuanzia miaka mitano, lakini hii ya sasa hivi iliyokuwa imegunduliwa na vituo vyetu vya utafiti vya Arusha na *KCU* wameweza kutoa miche ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu kuna tafiti ambazo zinafanywa siku nyingi na bodi ya korosho, kule Naliendele, mpaka tafiti zile hazitangazwi, mpaka leo tafiti zile hazijaleta matunda. Kunachohitajika ni kupata mikorosho ambayo itazaa kwa muda mfupi, njia za kufanya hivyo zipo. Kumepatikana njia za kuweza kufanya grafting ya mikorosho ambayo itaweza kuzaa kwa muda wa miaka mitatu na ikifika miaka mitano tumeshafikia *pick* ya *production* na kuweza kupata matunda kwa muda mfupi, lakini yaliyo bora na yanayoweza kustahamili ukungu kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamefanya utafiti watu wengi lakini tafiti zile bado zipo kwenye makabati; tunahitaji zitoke, tunahitaji ziwasaidie wakulima waweze kuzalisha mazao kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine linalokuwa linaleta ukakasi ni suala zima la tafiti zinazofanyika hasa kwa nzi wa maembe au wadudu ambao wanaathiri matunda mbalimbali. Tanzania ilikuwa ni moja kati ya nchi ambayo inasafirisha matunda nje kwa kiasi kikubwa sana. Lakini kutokana na tatizo la kupatikana na

hawa nzi wa maembe ambalo limekuwa ni tatizo kubwa hapa nchini tumeshindwa kabisa kuweza kuingia katika hayo masoko ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zipo za kugundua tiba ya hawa nzi wa maembe lakini vilevile tiba ya nzi ambao wanasababisha matunda mbalimbali kuweza kuharibika, lakini bado zimefungiwa kwenye makabati. Lakini watu tayari wameshachukua *Ph.D* kwa tafiti hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii timu ya watafiti au huyo *director* aweze kukusanya hizi taarifa mbalimbali za tafiti na kuzitangaza ili watu ambao wanaweza kusaidia kutoa ufadhili wa kutengeneza hizo dawa au kununua hizo dawa nje ya nchi ziweze kuja, ziweze kutusaidia ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa mtaalam umezungumza vizuri sana, muda wako umekwisha.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuna nyongeza ya wageni, napenda kumtambulisha Mheshimiwa Salim Kikeke na Ndugu Ando Khorsa ambao wanatoka Idara ya Kiswahili ya *BBC London* ambayo leo wapo hapa. *(Makofi)*

Mgeni mwingine kutoka *Azam Media Group* ambaye ni Ndugu Hassan Mhelela, karibuni Dodoma na hongereni kwa kazi nzuri mnazozifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa jioni tutaanza na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na wa pili atakuwa Mheshimiwa Paschal Haonga na wa tatu atakuwa ni Mheshimiwa Richard Mbogo. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11 jioni.

*(Saa 6.57 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Namwita Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, ajiandae Mheshimiwa Haonga.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii niwe mchangiaji wa kwanza na mimi mchango wangu utajikita sana kwenye hii Taasisi ya Utafiti wa Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno ya utangulizi, Watanzania tumekuwa Wataalam wazuri sana wa kutunga sheria kama ambavyo tuko wataalam wazuri sana wa kupanga mipango, tatizo letu kubwa liko kwenye upande wa utekelezaji, kwamba ni nani anaingia kwenye utekelezaji. Kwa hiyo, kuja na Muswada huu, Serikali imeleta Muswada huu ni mahali pake kabisa kama ambavyo kauli mbiu inavyosema kwamba tunakwenda kwenye nchi ya viwanda na hatuwezi kwenda kwenye nchi ya viwanda kama tukisahau kilimo na hatuwezi kufanikiwa kwenye kilimo kama hatukuweza kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, tatizo langu ni matumizi ya hizi tafiti. Je, tuko tayari kutumia hizi tafiti? Je, tunao wataalam wa kutosha wa kutafsiri hizi tafiti? Je, tuna mikakati ya kufikisha matokeo ya hizi tafiti kwa walengwa? Hapo ndipo ambapo napata ukakasi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu muundo wa Bodi ya Utafiti wa Kilimo, hapa naona pana upungufu kidogo, sijawaona watu wa Bodi za Mazao, kwa sababu hawa watu wa Bodi za Mazao ndiyo hasa mara nyingi wako na wakulima wa mazao husika, lakini hapa kwenye Bodi hii hawa Watafiti wa mazao sijawaona, badala yake nimekuta hapa hii namba 5(2) kuna Mkurugenzi wa Halmashauri, nafikiria badala ya kumweka huyu Mkurugenzi wa Halmashauri tungemweka Mwakilishi yeyote kutoka kwenye Bodi ya Mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija Namba Nne, unakutana na kazi za taasisi, moja ya kazi za taasisi nimeona hapa wameandika kuhamasisha matumizi ya mbegu bora. Matumizi ya mbegu bora ni lazima yaende sambamba na matumizi ya pembejeo za kilimo, sasa nazo hapa sijaona, Ningependekeza kazi mojawapo hawa Watafiti angalau wangepewa ni hii ya kuhamasisha matumizi bora ya mbegu na viuatilifu kama mbolea na pembejeo nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye muundo tumeambiwa patakuwa na Baraza, hili Baraza nalo sijaona katika wawakilishi sehemu hii namba 12, sijaona Mwakilishi hapa kutoka Bodi ya Mazao, bado wanaendelea kusahaulika hawa na hawa mara nyingi wana vikao vya Bodi vinakaa *at least* kila mwaka kufanya tathmini ya mazao mbalimbali. Ningetegemea kwamba pangekuwepo na ripoti ya utafiti ikaletwa kwenye vikao hivi vya Bodi vikatusaidia, lakini hapa napo sijaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matokeo ya utafiti. Sijaona mkakati kwenye Muswada huu ni namna gani matokeo ya utafiti yatawafikia walengwa ambao ndiyo hasa wazalishaji. Kwa sababu tunayo matatizo, nikitolea mfano,

mimi ni mdau wa zao la korosho, kwenye zao la korosho tunayo matatizo na hawa watu wa utafiti, mara ya mwisho tuliambiwa pembejeo, viuatilifu wanasema vile vya maji ni bora zaidi kuliko vile vya unga. Tukaja tena tukaambiwa lakini vile viuatilifu vya kimiminika (maji) vinatumika masika, wakati korosho sisi tunapulizia kiangazi, sasa bado tunapata mkanganyiko na mkanganyiko huu ulitakiwa tupate majibu kutoka kwa hawa Watafiti wanatusaidiaje, lakini utaona kwamba *chain* ya kutoka kwa Watafiti mpaka kwa watumiaji sijaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirejea hapo kwenye korosho, tumeletewa mbegu tukaambiwa hizi mbegu ni za muda mfupi. Ni kweli baada ya miaka mitatu hii mikorosho huwa inazaa lakini tatizo lake iko kwenye *lifetime* ya mkorosho. Ile mikorosho yetu ya asili hata miaka 20 unavuna tu, lakini hii mikorosho ambayo imeletwa na hawa watafiti bado inatupa shida. Utakuta kwamba tunakosa watu sasa wa kuja kututafsiria au kutuelekeza kwamba hii mikorosho itakaa kwa muda gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye jedwali namba moja, sehemu ya tatu. Kuna hawa Wajumbe wa Bodi, inasemwa kwamba pakiwa na mgongano wa maslahi, kuna neno limetumika hapa kwamba ikiwezekana, sijaelewa unaposema ikiwezekana maana yake nini, kwamba *it is optional,* anaweza aka-*declare* au la. Mimi naona hapa kipengele hiki nacho kingeweka wazi ili na sisi watumiaji wa hii sheria tuweze kupata ufafanuzi unaoridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utafiti, nimeangalia kwenye huu Muswada wote, mkazo kwenye utafiti wa masoko sijauona na tatizo kubwa la mazao ya kilimo ni masoko. Kwa sababu hata ukiangalia upungufu wa uvunaji au uzalishaji unategemeana na soko. Mfano kule kwetu tunalima sana korosho, ufuta na mbaazi, haya mazao yana matatizo ya kubadilishana masoko. Mwaka ambao soko la korosho limepanda, basi mwaka unaofuata litashuka na mwaka ule likishuka watu wanalima mbaazi, mbaazi nazo zikishuka watu wanalima korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo watu wetu hawako *stable*. Sasa na hawa watu wa utafiti nao sijaona, sijui kwa sababu sasa hivi ndiyo wamesema kwenye Muswada huu kwamba tutaimarisha hiki kitengo cha utafiti, lakini bado naona tuna matatizo, tuna-*base* sana kwenye utafiti wa mazao, kuongeza ubora na wingi labda hivyo, lakini bado kwenye upande wa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeona kwenye huu Muswada, kipengele hiki cha maeneo ya utafiti, sehemu ya Nane, kipengele (l) nafikiri ndiyo kimegusia kidogo kuonesha kwamba, yaani kama kuna masoko. Ningetegemea hivi vitu vyote viwili vingeenda sambamba, unapozungumzia utafiti wa kilimo moja kwa

moja hapohapo lazima uingie kwenye utafiti wa masoko kwa sababu tatizo kubwa tunalo hapo kwenye upande wa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla basi ningependekeza kwamba ili tuweze kwenda sambamba na utafiti wa kilimo, basi ni lazima twende sambamba na utafiti wa masoko, tena hili la masoko kwenye hii sehemu ya maeneo ya utafiti, yaani imetupwa mbali sana kuonekana kwamba hatuko tayari. Vilevile, tukirudi kwenye utafiti nafikiri kwamba watu wanaoweza kututafsiria hizi tafiti na kutuletea hizi tafiti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kuchauka. Sasa namwita Mheshimiwa Pascal Haonga, ajiandae Dkt. Christina Ishengoma na Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami niweze kuchangia juu ya Miswada hii miwili ambayo wenzangu tayari wameshaanza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo. Nimesoma Muswada huo nimeupitia vizuri, lakini tatizo ninaloliona ni kwamba sijaona eneo ambalo ni *specific* kabisa linalohusu namna ya upatikanaji wa fedha za kwenye hii taasisi ya utafiti ambayo tunakwenda kuipitisha. Tatizo hili tusipoweza kujadiliana kwa makini sisi kwa pamoja leo kwamba fedha zinapatikana wapi, tutarudi kwenye kutelekeza hizi Taasisi za utafiti ambazo nyingi tumeshazianza tayari na nyingine nyingi tulishazitelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wapo hawa jamaa tunawaita *TaCRI,* hawa wanaofanya utafiti wa zao la kahawa. Tunafahamu kabisa na Mheshimiwa Waziri anajua kabisa hili kwamba waliokuwa wanafadhili *TaCRI* ni *European Union* ambao hadi sasa hajawahi kupeleka fedha, tunajua kwa nini hajapeleka fedha kwa sababu tunajua *European Union* iko miradi mbalimbali ambayo walikuwa wanaendesha, lakini baada ya kutokea mgogoro wa kisiasa kule Zanzibar wameamua kujiondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo bado tunaona kuna wadau wengine, kwa mfano mkulima wa kahawa alikuwa anakatwa karibu asilimia 0.75 anapouza kahawa yake ili aweze kuichangia *TaCRI,* lakini leo tutakwenda kuwabebesha wakulima wetu mzigo mzito sana tusipokuwa makini namna ya kuweza kupata fedha za kugharamia utafiti huu. Tunajua kabisa kwamba

wakulima wetu kila tunapoanzisha utafiti wa aina yoyote ile tunaangalia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ni sawa na mzazi unakwenda kuzaa watoto halafu unapanga gharama kwamba bajeti ya chai atakunywa kwa jirani, chakula atakula kwa mtu fulani. Kwa hiyo, tusipokuwa makini tutatelekeza hata hii Taasisi ya Utafiti wa Kilimo. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* labda kesho hiyo, naomba atuambie hizi fedha zinatoka wapi na nimepitia sijaona ni maeneo gani wanapata hizi fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu huyu Mkurugenzi Mkuu wa Utafiti, wanasema awe na ujuzi uliothibitika na uzoefu usiopungua miaka 10 katika masuala ya sayansi na utafiti wa kilimo. Ukisoma ukurasa wa 41 na 42. Huyu Mkurugenzi unayeniambia kwamba awe na uzoefu usiopungua miaka 10, hili litakuwa kama ni eneo ambalo watu wetu wenye uwezo mzuri tutawanyima nafasi kama hizi. Leo unaweka miaka 10 uzoefu, kwa hali ya kawaida miaka 10 ni mingi sana, kama amezaa mtoto maana yake yuko darasa la nne au la tano. Sasa hii nadhani tungepunguza kidogo hapa, kwa nia njema, siyo kwa nia mbaya, angalau tuweke hata miaka mitatu, siyo dhambi, tuweke miaka mitatu, naamini tutapata watu wazuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo naomba niondoke kidogo niingie kwenye huu Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania. Amezungumza Mbunge mwenzangu aliyekaa, kuna tatizo moja ambalo linaonekana lazima tulijadili mapema kwa mfano suala la utafiti wa masoko ya samaki ili kuongeza pato la wavuvi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima hapa tujaribu pia kuzingatia haya, tueleze vizuri kwamba utafiti huu utasaidiaje kutafuta masoko kwa sababu shida katika Taifa letu ni kwamba tunao samaki wa kutosha na mazao mengine ya baharini, tatizo kubwa ni masoko na nadhani kwa sababu sheria hii tunakwenda kuipitisha, naamini kabisa hili suala la masoko pia tulizingatie tuweze kuangalia ni namna gani tutatafuta masoko kwa ajili ya samaki wetu na mazao mengine ya baharini, tutakuwa tumeongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua baadhi ya nchi duniani zinazotegemea zao la samaki kuendesha uchumi wa nchi zao, kwa mfano, zipo nchi kama Mauritius, nchi kama Seychelles, nchi kama *Phillipines,* Norway, Australia na nchi nyingine nyingi ambazo zinategemea samaki kwa ajili ya kuendesha uchumi wa nchi zao. Sasa na sisi hapa lazima tuangalie tunafanyaje kwenye huu utafiti, tunaingiza wapi angalau eneo la kuweza kutafuta masoko kwa ajili ya samaki wetu na mazao mengine ya baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo dagaa wengi sana wanavuliwa kwa mfano Ziwa Victoria wanapelekwa Congo, lakini hatujui nchi inapata shilingi ngapi, kwa sababu soko kubwa la samaki na dagaa tunajua kabisa ni Congo. Sasa leo tunapeleka kule, wenzetu wanapeleka kuchakata viwandani, wanatoa ajira lakini sisi Taifa hatunufaiki na chochote na kama ni kunufaika basi itakuwa ni kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naomba nizungumzie ni kwenye suala la udhaifu wa sheria za utafiti. Kumekuwa na tatizo kwa muda mrefu sana, leo wanakuja wageni katika Taifa letu, kwa mfano mdogo walipokuja wale jamaa wa China wamevua samaki kwa muda wa wiki tatu wamepata samaki wengi sana. Wale samaki wamepatikana wengi, lakini wale jamaa walikuja kwa njia za ujanja ujanja, sasa sijui kama walikuja kufanya utafiti au walikuja kufanya uhuni wale samaki jina maarufu samaki wa Magufuli nadhani mnakumbuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa kwa sababu ama kwa kukosa sheria ambazo haziwabani vizuri watu wa namna hii tukajikuta kwamba wale watu wamevua samaki wengi kwa muda wa wiki tatu wamepata samaki wengi na mwisho wa siku tukawakamata tukachukua na ile meli tuka- *seeze* lakini bahati mbaya sana ile kesi walitushinda Mahakamani, hadi leo hii tumeingia hasara kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mambo yote hayo naomba tu tujaribu kuangalia tuweke sheria ambazo zitawabana wale watu wanaokuja kufanya utafiti kutoka nje ya nchi, zitakazowabana wale wezi wanaotuibia samaki wetu. Tunaamini kabisa kwamba tukiwabana samaki tunao wa kutosha, tutauza nje ya nchi tutatengeneza ajira kwa watu wetu, lakini tukikaa kimya na sheria tusipoziweka vizuri itakuwa ni *business as usual,* tutaibiwa sana na tutaendelea kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba suala hili tujaribu kuliangalia kama Taifa kwa pamoja. Kwa mfano hizi tafiti tunazozianzisha zote kwa maana ya hizi sheria, hii Miswada tunayoipitia, yote miwili inafika mahali kama alivyoongea Mbunge mwenzangu, tumepitisha sheria, ukiangalia unaona kama nzuri kwenye maandishi lakini hizi tafiti zinaishia kwenye makaratasi, haziwasaidii wananchi wetu, hatuzifikishi kule chini ili watu wetu waweze kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano leo bado kama tunazo hizi sheria za utafiti ambazo tumeshazipitia siku nyingi, bado kwenye mazao mbalimbali hapa nchini tumeona kuna ugonjwa wa mihogo, kuna ugonjwa wa kahawa. Kwa mfano, kwenye kahawa kuna ugonjwa fulani unaitwa *CBD (Coffee Berry Disease)* leo ukimuuliza hata Mheshimiwa Waziri anajua kwamba hadi leo ukiuliza ugonjwa huu wa *Coffee Berry Disease,* hadi leo hauna dawa

zaidi ya kusema kwamba unatakiwa uzuie. Sasa tujue je, hizi taasisi za utafiti ambazo tunazo, tumezianzisha zimetusaidia kwa kiwango gani na tunapoenda kuanzisha nyingine zitatusaidia kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba mwisho wa siku tutaishia kuanzisha hizi taasisi za utafiti, hazitatusaidia lakini tukiwa makini naamini kabisa kwamba zitatusaidia. Shida kubwa katika Taifa hili, ameongea Mbunge mwenzangu, ni kwenye suala la *implementation*. Tumekuwa na Taasisi nyingi, tumekuwa na tafiti nyingi, tumezipaki kwenye makabati, tumezipaki huko hatuzifanyii kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kwa pamoja bila kujali itikadi ya Vyama vyetu, tunapokwenda kujadili haya mambo yakafanye kazi kwa wananchi wote kule chini. Taifa lolote lile duniani ambalo halifanyi tafiti, Taifa hili limekufa na mwisho wa siku haliwezi kuwasaidia wananchi wake. Kwa hiyo, naomba kwa nia njema hizi tafiti ziwafikie wananchi wetu na ziweze kuwanufaisha, hatutaki ziishie kwenye makabrasha kama ilivyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna Sheria hii ya Uvuvi ambayo ilianzishwa siku za nyuma huko, tujue je, upungufu ambao yalikuwepo siku za nyuma, je tunaweza kuyarekebisha kiasi gani kwa kuanzisha sheria nyingine hii ya uvuvi. Kama kuna upungufu ulikuwepo, tumekwenda kuanzisha sheria nyingine tafsiri yake ni kwamba hii sheria pia itaishia kwenye makabrasha humu, tutaiacha hapa na mwisho wa siku tutakuja miaka mingine mbele kuanzisha sheria nyingine.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.  Dkt. Ishengoma, jiandae Mheshimiwa Mbogo na Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia Miswada hii miwili. Nitachangia kwa pamoja Muswada unaohusu Taasisi ya Utafiti wa Kilimo pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi *(TAFIRI)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema tafiti kwa kuanzisha hizi Taasisi na sheria naamini ni kitu kizuri sana ambacho kinamfanya Mtafiti aweze kumiliki tafiti zake badala ya kudhibitiwa pamoja na Taasisi nyingine. Naungana na Kamati  jinsi ilivyoongea pale asubuhi na tuliweza kusema kuwa uwepo Mfuko wa Tafiti, kwa sababu ukianzishwa  Mfuko huo, utamuwezesha hata Mtafiti yeyote yule anayetoka kwenye shughuli za kilimo pamoja na Mtafiti kwenye upande wa uvuvi kuweza kupata hela hasa za kufanyia tafiti zake.

Kitu kingine tulichoongelea ambacho inabidi kukazia ni kile ambacho kilikuwa kinasema kwenye Muswada ambao ulikuwa kwa upande wa uvuvi kuhusu yeyote yule ambaye atakuwa anafanya utafiti na kama utafiti wake haukwenda vizuri aweze kurudisha hela, hiyo, kwa kweli nasema hapana na bado nasema hapana. Haiwezekani ndiyo sababu ikaeleweka kuwa afadhali wawepo watu au *group*, Maprofesa au Bodi ambao wanaweza wakafuatilia huo utafiti wa huyo mtu tangu anapoanza mpaka anapoendelea. Mahali inapoonekana utafiti hauendi vizuri aweze kuachia hapo hapo badala ya kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukulie kwa mfano wanafunzi ambao wanasoma Vyuo Vikuu, unasema kuwa wafanye utafiti mpaka mwisho na kama pale ambapo hawata-*succeed* kuwa tafiti zao zimekubalika waweze kuleta hizo hela, hela hizo watazitoa wapi? Kwa hiyo, hapo naungana na Kamati kuwa kwa kweli tuangalie mlolongo wa utafiti unavyokwenda na pale inapoonekana kuwa utafiti haueleweki, hauendi vizuri aweze kuachia hapo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni la kuongelea ni wale watafiti kwenye *deep sea*. Kwa kweli hapa tunavyotunga Kanuni naomba kanuni zinavyotungwa Serikali iangalie jinsi ya kuangalia uvuvi wa kwenye *deep sea* kwa sababu tunaibiwa sana kwenye *deep sea* bila ya kuangalia na mapato mengi sana tunayapoteza pale ambapo hatuendi vizuri. Kuna vifungu ambavyo vinaongelea kuhusu umiliki wa tafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtafiti anayetafiti utafiti wake naomba aweze kumiliki huo utafiti. Bila ya tafiti hatuwezi kufika popote. Kwa hiyo, naunga mkono hizi sheria ziweze kupitishwa kusudi kwenye tafiti hizi tukitafiti, tafiti nyingi zimeshatafiti, Vyuo Vikuu vingi vimeshafanya tafiti, lakini kweli kufikia kwa mlengwa wakati mwingine inakuwa ni ngumu. Kwa hiyo, kwenye Kanuni iweze kuonekana jinsi inavyoweza kumfikia yule mlengwa na walengwa hasa ni wale wananchi ambao ni Wavuvi na ambao ni Wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi nilikuwa nimechangia asubuhi nilipokuwa nachangia kwenye Kamati na sasa hivi naomba niongezee hayo machache ambayo nimechangia. Naomba Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono Miswada hii yote miwili kusudi iweze kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Richard Mbogo, jiandae Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa hii nafasi, nitaenda haraka kidogo kwa sababu muda siyo rafiki sana. Kwanza niipongeze Serikali na Wizara husika kwa kuweza kuwasilisha huu Muswada, kwa sababu sasa hivi Serikali yetu mwelekeo ni kwenye nchi ya viwanda na tukiangalia nchi ya Tanzania imebarikiwa sana. Tuna Bahari, tuna Maziwa katika hii dunia tumebarikiwa mno. Kwa hiyo, hizi sheria kuja kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali inabidi tuziboreshe na ziweze kutumika ipasavyo kwa ajili ya kunyanyua uchumi na kutengeneza ajira katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Muswada huu kuna maoni maeneo mbalimbali ambayo nimeweza kuyaona, nikianzia na Muswada huu wa *agriculture*, kuna *comment* ilitoka kuhusiana na mambo ya mifugo. Ingekuwa ni bora iunganishwe iwe ni kilimo na mifugo ili na wenyewe tuweze kutengeneza ajira na kunyanyua uchumi, mifugo iweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha Nane uteuzi wa Mkurugenzi kinaeleza kwamba Rais atamteua baada ya kushauriwa na Waziri. Tumepitisha Miswada takribani minne, lakini ushauri kama huu nakumbuka hapa haukuungwa mkono suala la kushauriwa Rais kupitia Mawaziri wetu katika uteuzi. Kwa hiyo, itabidi tuwe na *consistency* tuweke kama katika Miswada mingine ambayo tumepitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Baraza la Taifa la Ushauri. Naona tuone jinsi gani ya kuhusisha pia na Bodi mbalimbali za Mazao wawe ni moja ya Wajumbe kwenye hili Baraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 14 ni maeneo ya tafiti, lakini nilivyoangalia humu ndani kuna baadhi ya Mikoa ambayo imesahaulika kuwekewa kuwa ni sehemu pia ya Vituo vya Tafiti. Kwa mfano; mapendekezo ambayo nitayaleta Mkoa wa Njombe tuwe na Kituo cha Utafiti ili kiweze kukidhi Mkoa wa Iringa na Ruvuma; na pia Mkoa wa Katavi tuwe na Kituo cha Utafiti ili tuweze kukidhi Mikoa ya Katavi, Kigoma na Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 16 kwamba tutakuwa tuna-*commission* baadhi ya kazi, sasa ni wakati gani ambapo tutaweza kuwajengea uwezo vijana ambao wamemaliza kwenye vyuo vyetu, kwa nini tusiwajiri na wafanye hizi kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tukienda Kifungu cha 18(2) kwamba Taasisi inaweza ikafanya biashara kwa kuuza, kununua hizi tafiti. Ningeshauri kwamba Waziri ajaribu kuangalia tusije tukauza utafiti ambao ukatoka na Tanzania isiweze kufaidika. Tukienda Kifungu cha 19, kuhusu utangazaji wa matokeo ya utafiti, tumeonesha tu kwamba tuna-*review* na kupitia kwa mtu ambaye ametutumia mali za Taasisi na kufanya utafiti, ili tuweze kuwa na tafiti

zilizo bora, nitashauri Waziri aangalie hata wale ambao wanafanya tafiti kwa gharama zao wenyewe wawe wanakuwa *reviewed* na hii Taasisi ili tuwe na matokeo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 20 kimenifurahisha kuhusu kufanya utafiti mpaka nje ya mipaka. Tunakumbuka Vietnam miaka ya 1970 walichukua zao la korosho lakini walichukua kwetu wamepeleka nchini kwao na ni moja ya nchi duniani ambazo zinatoa sana zao la korosho. Kifungu cha 20(3) kuna masuala ya watu ambao wameathirika kutokana na huu utafiti, tutaomba Waziri aziweke athari kwenye Kanuni ili ziweze kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 23, mtu anayeomba kusajiliwa kama Mtafiti au Taasisi yake anaweza akakataliwa, lakini hapa hakuna nafasi ya jinsi gani mtu anaweza akakata rufaa au akarekebisha makosa aliyoyafanya na kuweza kuomba tena, hilo nalo tutaomba Waziri aliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya utafiti kufanywa na mtu wa nje lazima ashirikiane na wa ndani yaani Mtanzania kifungu cha 24, basi kwenye Kanuni ielezwe faida itakayopatikana, Mtanzania atakuwa na asilimia kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la adhabu, masuala ya adhabu kwa makosa mbalimbali hayana *consistency,* adhabu zake kidogo zimekuwa ni ndogo na suala ambalo limepigiwa kelele sana mtu anapofanya kwa nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa *research,* upande wa Wavuvi, Kifungu cha 6(1)(c) kwamba utafiti na uchunguzi magonjwa ya samaki lakini kwenye maji hatuna samaki tu, tuna viumbe wengine pia wanaishi ndani ya maji sasa wenyewe kuhusu magonjwa yao utafiti hautafanyika? Kuna hadithi zile za nguva, tuna mamba, tuna viboko, tuna vyura na tuna nyoka wengine ambao wanaishi ndani ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wavuvi kuna Kifungu cha 8(4) kidogo kinanitatiza hapa, Waziri anapewa Mamlaka ya kubadilisha kwa namna yoyote ile atakavyoona suala la Jedwali baada ya kuwa ametangaza. Sasa majedwali tunapitisha humu ndani Bungeni na hayo marekebisho Waziri akifanya atarudisha tena Bungeni? Kwa hiyo sioni haja ya kumpa Mamlaka haya Waziri kufanya mabadiliko kwenye majedwali wakati majedwali haya tumepitisha hapa ndani Bungeni maana yake akifanya marekebisho lazima alete tena huku. Kwa hiyo, ni bora tumwachie huru kwenye upande wa Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine upande wa Wavuvi ni uteuzi wa Naibu Mkurugenzi. Ametajwa lakini kazi zake hazijatajwa. Kwa hiyo, tutakuwa

na mtu ambaye *functionally* atakuwa yupo kusubiri Mkurugenzi hayupo yeye ndiyo akaimu, hivyo sioni haja ya kuwa na Naibu Mkurugenzi katika hii sheria na nitaleta mapendekezo kwamba aondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mtu ambaye hajakamilisha utafiti arudishe gharama, sasa je, akishindwa na hizo adhabu zimetajwa? Kwa hiyo basi, tuweke mazingira ya kwamba mtu awe na dhamana kwa pesa tunayompa ili akishindwa utafiti basi iwe ni moja ya kinga ya kumwezesha kurudisha pesa ambayo tuliweza kumpatia kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la kuomba vibali katika kifungu cha 20, napendekeza taasisi yenyewe ndiyo itoe kibali na siyo mtu aende kwenye Tume ya Sayansi na Teknolojia, tutaweka ukiritimba kwenye utoaji wa vibali kwa watu wanaotaka kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni dhana nzima ya watu ambao wamefanya vizuri, kuna suala la *intellectual property* inabidi tuliangalie kwa umakini zaidi ili watu wetu ambao Mungu amejaalia na wameweza kufanya utafiti waweze kufaidika na kile ambacho wamejaaliwa. Kifungu cha 31, masuala ya *report*, kinasema siyo chini ya miezi miwili, hii inatakiwa iwe miezi mitatu na kifungu cha 33 imeandikwa miezi mitatu kwenye *report* ambayo imekaguliwa iwe angalau miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mengine ni jedwali; tumetaja bahari, tumetaja vituo lakini tumesahau Ziwa la Rukwa ni moja ya Ziwa kubwa nalo liingie kwenye jedwali la kwanza kama moja ya vituo vya utafiti kwa sababu hata hivyo hivi karibuni tu Serikali ilisema kuna madini yamepatikana kule ambayo ni adimu. Mapendekezo mengine nitayaleta kwenye jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jitu Soni, jiandae Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuja na Miswada hii yote miwili kwa muda muafaka, ilitakiwa ije mapema, lakini niipongeze sasa kwamba zimekamilika. Hii itatusaidia sana kusonga mbele katika Sekta ya Kilimo, Mifugo pamoja na Uvuvi na zote zinaingiliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo machache ambayo ningependa nichangie, moja tunaendelea kuunda hizi Taasisi mbalimbali. Tayari tunazo nyingine nyingi upande wa mifugo hata hii upande wa uvuvi, lakini

ningependekeza tuwe na *Tanzania Research Institute* moja, hizi zote zingeunganishwa tuwe na *Institute* moja tu ambapo huu chini sasa pawe na Idara mbalimbali ya Kilimo, ya Mifugo, ya Misitu na nini ili kupunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaunda hizi Bodi, tutaunda muundo mzima ambao tumependekeza hapa na matokeo yake kila mwaka tutakuwa tunapeleka fedha kwenye bajeti za *OC,* lakini hatutakuwa na pesa za *development* ambapo tungekuwa na Taasisi moja tu, nina uhakika kwamba tungeweza kuwa na timu ndogo, kila sekta ingekuwa inatoa mtu mmoja kuingia kwenye ile Bodi, basi gharama zingekuwa zinapungua, halafu fedha nyingi ziwe zinaenda kwenye kufanya utafiti yaani kwenye *development.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hapa bado kila mmoja atakuwa anashindana hivyo hivyo. Kilimo atataka, wa Mifugo atataka, wa Uvuvi atataka, ukija kwenye Misitu kila mmoja anataka fedha tofauti tofauti. Sisi hatuna fedha hizo na hata leo hii *COSTECH* ndiyo ambayo inasimamia utafiti karibu wote. Hao wote wanategemea pesa kutoka huko, ni bilioni nane tu ambazo zimetengwa mwaka huu ambayo haitoshi hata kwenye chuo kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo fedha sasa ni vizuri tuanze kufikiria pamoja na hii itakuwepo lakini ziunganishwe sasa tuwe na *Tanzania Research Institute* ambayo itakuwa inasimamia sasa mambo ya utafiti mbalimbali na hapo patakuwa na *coordination* nzuri, hapo ndiyo patakuwa mahali ambapo unapofanya utafiti labda kwenye Ziwa fulani siyo lazima aende mtu wa samaki tu. Huyu wa mafuta ataenda kuangalia madini kama yapo, kama kuna masuala ya maji, ubora wa maji wote watakuwa wanashirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependekeza, kwa baadaye tufikirie kuwa na *Tanzania Research Institute* moja ambapo taasisi zote hizi zitakuwa chini yake, itakuwa ni *umbrella* kwa ajili ya taasisi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwenye hii ya uvuvi, ningependekeza taasisi zetu badala ya kuwa na vituo vyao ambavyo wanafanyia kazi zao wako peke yao na tafiti zao nyingi hazifiki kwa walengwa, tungeunganisha na Vyuo Vikuu vyetu na tungeunganisha na vyuo vingine. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Sokoine, basi Taasisi hii ya Utafiti ya Kilimo ingekuwa humo ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulienda na Kamati ya Kilimo Holland, unakuta Chuo Kikuu huwezi kutofautisha nani ni mwanafunzi, nani ni mfanyakazi wa chuo na nani mtu wa utafiti. Mwanafunzi anayeingia wakati anafanya utafiti wake hahitaji kusubiri kupewa fedha ya kwenda *field,* anapoanza tu shughuli tayari hapo anakutana na Watafiti, anakutana na vifaa mbalimbali ambavyo asingeweza kuviona angekuja kuvipata baada ya miaka mitatu, minne wakati

anakaribia kumaliza elimu yake ya chuo ndiyo atakutana na hivyo vitu, lakini hapa kuanzia siku ya kwanza anakuwa tayari anapata *on job training* na hapo anakuwa Msaidizi wa hao Watafiti na lingeweza kuwa ni jambo ambalo lingetusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganda wenzetu tayari wameshaanza hivyo. Unakuta *University* ya Kampala tayari iko imeunganishwa na vituo vya utafiti, kwa hiyo wanafanya kazi *under one roof,* lakini kila mmoja anakuwa kwenye Idara yake ndani ya ofisi moja. Unakuta wengine ni watu wa wanafunzi na wengine ni watu wa utafiti ambayo itatusaidia katika tafiti mbalimbali na wanafunzi wetu watakuwa wanapata *exposure* na watakuwa wanapata *on job training* hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nashukuru kwamba ikishaundwa basi tafiti mbalimbali ambazo zimefanyika sasa matokeo yake na namna ya kufanya majaribio yatakuwa yanaenda sasa kwa walengwa. Muhimu tafiti hizi wakati zinafanyika basi tungehakikisha kwamba kwa mfano kama ni za kilimo ziende kufanywa katika mashamba ya wakulima ili wakati wanafanya majaribio, basi wakulima pia yule ambaye hata kama hajasoma atajifunza jambo moja au mawili pale na yeye anaweza kushika yale mazuri na tukawa tunaboresha kilimo chetu na pia katika masuala ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uvuvi sehemu kubwa Tanzania tumebarikiwa kuwa na maji ya kutosha; Mito, Maziwa lakini hatuna *industrial fishing* yaani ufugaji wa samaki ambao ni *commercial,* hiyo yote inatokana kwa sababu hatuna suala zima la utafiti ambao umefanyika na ni muhimu sasa tuunganishe nguvu zetu kwamba utafiti wowote ambao unafanywa uende ufanywe huko kwa walengwa na nina uhakika kwamba matokeo yake walengwa watakuwa wananufaika, kama ni wakulima, kama ni wafugaji, kama ni wavuvi, wote watanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye suala la *Board Member* nilikuwa napendekeza pia iongezwe na nitakuja na *amendment* kwamba pawe na *Board Member* mmoja kutoka *private sector* ambaye yuko kwenye kazi hii ya utafiti, kama ni *Researcher,* kama ni wa mbegu, kwamba anafanya *biotechnology* mambo ya *tissue culture* nini, kama wana *association* yao, basi mmoja wao pia tofauti na yule anayetoka kwenye *farmers group* ambaye ni mkulima wa kawaida, yeye atakuwa anapeleka mahitaji, lakini huyu ambaye yupo kwenye *field* moja kwa moja na ni mtaalam, basi mmoja wao pia aunganishwe kwenye hiyo Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine ambaye pia ningependekeza awepo kwenye Bodi na iwe katika Bodi zote ambazo tutaunda ni mtu kutoka Idara ya Mipango. Mara nyingi hapa tunaweka watu mbalimbali, lakini watu wa Idara

ya Mipango hatuwaweki na tusipowaweka watu wa Idara ya Mipango na watu wa Fedha matokeo yake huko tutajiandaa vizuri, *planning* inakuwa vizuri, lakini mwisho wa siku ambaye anaamua kwamba fedha ziende wapi kama hajui na haelewi, fedha hizo hatutapata. Kwa hiyo, ningependekeza mtu wa mipango na fedha wawepo pia katika Bodi hii ili wawe na uelewa kwamba nini kinatakiwa na wakati tunapopanga bajeti zetu wawe wanahakikisha kwamba mpango unawekwa kwamba bajeti hiyo itapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependekeza kwamba tafiti zimefanywa nyingi, sasa namna ya kusambaza zile tafiti iwe katika kilimo, mifugo iangaliwe namna ya kutumia pia vijana wetu kuanzia ngazi ya sekondari, kama utafiti mbalimbali unafanywa wangekuwa wanafanya pia katika shule zetu za sekondari, wanafanya pia katika vyuo mbalimbali, nina uhakika kwamba tungekuwa tunafika mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu hapa kuliko yote ni namna ya kupata fedha ya uhakika. Kipindi cha bajeti hapa tulipendekeza kwamba shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta iwekwe iende kwenye utafiti ambayo tungepata karibu bilioni 100. Hapa kwenye Kamati wameandika kwamba Serikali imetenga chini asilimia 0.5 ya Bajeti nzima, siyo 0.5 ni 0.0005 kwa sababu bilioni nane kwa trilioni 29 haionekani wala haipo kwenye mahesabu ni sawa na hatujatenga fedha yoyote kwenye utafiti. Lazima tuwe na chanzo cha uhakika ambacho fedha zake zitakuwa zinakwenda kwenye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Uganda leo asilimia 40 ya fedha kwa ajili ya kuendeleza mambo ya utafiti iko kwenye bajeti yao. Majengo pamoja na vifaa, Serikali inanunua asilimia100 na ukienda pale unakuta vijana wadogo wenye umri wa miaka 25 mpaka 35. Ukienda kwenye vituo vyetu kwakweli inasikitisha kwa sababu wako watu waliosoma sana wana *Masters, Phd, Doctorates* mbalimbali, mwingine amesoma katika kozi tatu, nne kwa sababu pesa za kufanya maendeleo ya kufanya kazi hamna, kwa hiyo anabaki pale anajiendeleza kusoma, mwisho wa siku anakuja kustaafu hajatumika kabisa na mifano mingi tunayo hapa Tanzania. Sasa watu wale badala ya kugharamia kuwasomesha tungehakikisha kwamba tafiti mbalimbali ziendelee kufanywa na Watanzania wanufaike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuje kwenye suala la *biotechnology* ambayo inakuja kwenye kilimo, inakuja kwenye mifugo, inakuja kwenye uvuvi, ni vizuri sisi wote tukapata uelewa mpana kuhusu masuala ya *biotechnology,* wengi hapa wanapinga na wanapiga vita masuala ya *biotechnology*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipojiendeleza kwenye masuala ya *biotechnology* Watanzania tutakuja kupitwa na wakati kwa sababu wenzetu Waganda 2020 wataanza kutoa ndizi na mazao mengine ya *GMO* na sisi

hatuna ukuta wala hatuna namna ya kuzuia vile vitu kuja hapa. Tayari leo Watanzania tunakula vitu vingi ambavyo ni *GMO* bila kujijua. Kwa hiyo ni vizuri tupate uelewa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Fatma Toufiq, jiandae Mheshimiwa Paresso na Mheshimiwa Waitara Mwita ajiandae.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa nami nichangie katika hii Miswada miwili ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba moja kwa moja nijielekeze kwenye Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya mwaka 2016, nianzie pale katika Kifungu cha pili (2) ambacho kinatoa tafsiri ya maneno yatakayotumika katika Sheria hii. Naomba ninukuu ukurasa wa 36 kwenye tafsiri ya maneno ya Chama cha Wakulima ambayo inasema kwamba maana yake ni Chama ambacho kimesajiliwa na mamlaka husika na kilichoanzishwa na watu wanaojihusisha na uzalishaji, usindikaji au biashara ya mazao maalum ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri wangu hapa kwamba kwa nini ibainishe kwamba mazao maalum ya kilimo, hapa tungeweza tukasema kwamba ni mazao ya kilimo, lakini huko kutakuwa kuna vikundi vidogo vidogo kile chama kiwe ni *umbrella organization*. Naona kwamba tujaribu kuliona hili na kwamba libadilishwe hapa kwa sababu kama tukisema kwamba ni mazao maalum ya kilimo ina maana kwamba itabidi yabainishwe, kama ni ufuta ubainishwe kwamba ni ufuta, kama ni alizeti au chochote basi tubainishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichangie katika Kifungu cha 18(4) naomba ninukuu, kimesema: "Endapo ugunduzi, uvumbuzi au ubunifu ni mali ya taasisi chini ya Kifungu cha (1), Taasisi inaweza, (a), (b), (c) kwamba kutoa tuzo kwa mtu yeyote aliyehusika na ugunduzi, uvumbuzi au ubunifu huu inaendelea mpaka (c)."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba badala ya kusema kwamba hii taasisi inaweza litumike neno, ilazimike, kwamba iwapo ugunduzi au uvumbuzi au ubunifu ambao uko chini ya kifungu hiki, taasisi inalazimika kutoa tuzo, kwa sababu tukisema kwamba inaweza, ina maana kwamba hapa ni *optional,* kwa hiyo inawezekana kabisa kwamba mhusika katika taasisi hii anaweza asiitoe ile tuzo iwapo hata kama yule mtafiti anastahiki kupewa hiyo tuzo. Kwa hiyo, huo ulikuwa ni ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba nitoe pongezi zangu kwa Kifungu cha 24(1) na (2) ambapo sheria hii imebainisha kwamba lazima Mtafiti ambaye atatoka nje ashirikiane na Mtafiti wa kutoka Tanzania, ndani ya nchi. Kwa kweli nipongeze sana jambo hili na hili nadhani lingetumika kwa baadhi ya sheria zetu za nchi hii. Hata Sheria ya Uwekezaji na sheria zingine kwamba Watanzania wangekuwa wanashiriki au ni lazima washirikiane na wawekezaji, hili naomba niipongeze sana Wizara, hii itasaidia sana kuwapa weledi watafiti wetu na hivyo wajione kwamba wanakubalika na wanaaminika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kutoa mapendekezo ni kwamba katika Kifungu cha 35 ambacho kinazungumzia masuala ya rufaa, naona kwamba pale kifungu kidogo cha (1), (2) na (3) cha Muswada huu ambacho kinapendekeza kwamba Waziri peke yake ndiye awe na mamlaka ya kumaliza ile rufaa. Nashauri ingewezekana kwamba hata Mahakama kwa sababu Waziri ni binadamu na yeye, kwa kuwa ni binadamu inawezekana kabisa kuna vitu vingine na yeye anaweza akakosea, nashauri kwamba kwenye suala la rufaa ingekwenda zaidi kwenye Mahakama nayo ipewe mamlaka ya kutoa rufaa kwa mtu ambaye atahitaji kupata rufaa hiyo badala ya kuwa Waziri peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kupendekeza kwenye Kifungu cha 36 Kifungu (1), (2) pia nikiangalia zile herufi kuanzia (a) mpaka (m) kwamba, kwa kuwa Muswada umependekeza Kifungu kitekelezwe kupitia Kanuni zitakazotungwa na Waziri, nashauri pale kuna maneno yameandikwa katika Muswada huu Kifungu 36 kwamba Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya sheria hii. Naomba nishauri kwamba hapa siyo lazima Waziri aweze, hapana, nashauri iwe Waziri inabidi alazimike kutunga Kanuni hizi kwa sababu kama tukimpa *option* ina maana kwamba inawezekana asitunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni haya machache niliyoyaona, nikaona na mimi nitoe ushauri wangu *otherwise* nawapongeza sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Paresso, jiandae Mheshimiwa Waitara Mwita.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Miswada iliyoko mbele yetu, mchango wangu utajikita katika Muswada wa kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni takriban asilimia 73 ya Watanzania hutegemea kilimo na ni muhimu sana ili kilimo hiki kimnufaishe Mtanzania au

Watanzania hawa wa asilimia 73 ni lazima hiki kilimo kiwe na manufaa, kiwe na tija lakini ni lazima kiwe ni kilimo ambacho tafiti zitafanywa zitaweza kuwasaidia kuboresha kilimo chao ili kiweze kuwasaidia kwa maana ya uchumi, mahitaji ya familia na mahitaji ya nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tumekuwa tukianzisha hizi taasisi. Hii ni moja tu ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo lakini tunakuwa na taasisi nyingi na Muswada huu unapendekeza kuanzisha taasisi hii ambayo itakuwa ina Bodi, Menejimenti na Itakuwa na Baraza la Taifa la Utafiti. Kikwazo kikubwa ambacho mara nyingi tunakiona ni uwezeshwaji wa hizi Taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna changamoto kubwa sana, Taasisi zinaundwa, zinaachwa, fedha inapewa 'kiduchu', inapewa *OC*, zile za *other charges* lakini fedha kwa ajili ya maendeleo na fedha kwa ajili ya shughuli maalum hasa ya utafiti inakuwa ni mtihani na mara nyingi hili tumeliona. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Wizara na Serikali kwa ujumla kwamba ni muhimu sana mtakapokamilisha mchakato huu kuhakikisha hii taasisi inapatiwa fedha ya kutosha kuhakikisha inaendesha shughuli zake, inafanya utafiti ili iweze kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na fedha, wanahitaji pia kupata fedha au wanahitaji kupata fedha za uwezeshwaji wa kununua hivyo vitu ambavyo watafanyia utafiti au ambavyo vitaendana na teknolojia ya kisasa zaidi ili kuwasaidia na kurahisisha ufanyaji wao wa kazi. Kwa hiyo, ni muhimu sana, pamoja na kwamba tunapitisha hii Miswada, tunaunda hizi Taasisi ambazo ziko nyingi lakini bila kuwezeshwa kwa bajeti ya uhakika ya maendeleo mwisho wa siku hizi taasisi zitabaki tu kwenye makaratasi itakuwa hakuna kazi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi hii itakuwa ina kazi ya kuratibu utafiti, ufuatiliaji na tathmini, kwa hiyo, ni muhimu sana inapofanya tathmini yake, inapofanya tafiti yake, haya matokeo yanayopatikana ni lazima yawe-*shared* yaweze kushirikisha na mrejesho uweze kuwafikia wadau husika kwa maana ya wakulima au wale wote ambao wananufaika kwa namna moja ama nyingine. Kwa hiyo, haya ni masuala ya msingi sana kuyazingatia kuona tathmini hii inayofanyika ni lazima wadau washirikishwe, ni lazima wadau waweze kunufaika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii taasisi sasa ni lazima iangalie namna ambavyo itaungana au itaunganisha nguvu za pamoja na vyuo vyetu vikuu ambavyo vimekuwa vikifanya tafiti mbalimbali. Kwa hiyo, tusiwaache pembeni pia wataalam wetu, kwamba leo tunaanzisha hii Taasisi lazima pia tuangalie namna gani tutaendelea kushirikisha na kuunganisha nguvu za pamoja na hivi vyuo vikuu ambavyo vimekuwa vikifanya tafiti miaka yote kabla ya kuanzisha chombo hiki. Kwa hiyo, haya ni mambo ya msingi ya kuzingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kuanzisha Taasisi hii, tunatarajia kwamba ni lazima Serikali sasa itumie takwimu hizi, itumie matokeo ya tafiti hizi katika upangaji wa mipango yake, katika upangaji wa bajeti, katika kukifanya kilimo kiwe na tija kwa wakulima. Kwa hiyo, ni lazima hili likazingatiwa kuona tunaanzisha taasisi inakuwa na matokeo fulani, inakuwa na mitazamo fulani, inakuwa ina ushauri fulani kuhusiana na masuala haya ya kilimo, ni vyema Serikali ikayafuata, ikayachukua, ikawa ni dira yake ya kupangia bajeti na mipango mbalimbali ya sekta ya kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie sasa kwa kuchambua kidogo Muswada na kutoa mapendekezo. Ukisoma Muswada huu wa Kiswahili, kwenye *heading* pale inahitaji kufanyiwa marekebishao kwa sababu kule juu inasomeka Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi, lakini *content* zote ni Taasisi ya Kilimo na mwanzo kabisa wa *heading* hapa kwenye Kiswahili, ya Kiingereza iko sawa, lakini kwenye Kiswahili imeanza, ukurasa wa kwanza iko sawa, kwamba ni Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, lakini ukiendelea *page* ya pili mpaka ya mwisho inasomeka Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na siyo Mifugo. Kwa hiyo, nadhani inahitaji kufanyiwa marekebisho ili iweze kuleta maana sahihi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha 5(2)(a) kinasema, Mwenyekiti wa Bodi atateuliwa na Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 8(1) pia kinaeleza, Mkurugenzi atateuliwa na Rais. Kama ambavyo Kambi ya Upinzani imependekeza ni lazima tuondoke kwenye huu mfumo wa uteuzi, tuingie kwenye mfumo wa ushindani, tushindanishe watu wenye sifa, tutangaze hizi kazi, ni kazi ambazo kwa kweli zinahitaji utaalam na watu ambao wako tayari. Kwa hiyo, ni lazima tuondokane na huu mfumo wa uteuzi ambao umekuwa ni mwingi mno wa kubebana. Ni lazima tutoke huku tushindanishe hizi kazi, watu wenye sifa waombe, wachujwe kwa vigezo ili mwisho wa siku waweze kupata hizi nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukienda Kifungu cha 8(2)(d) wanasema katika uteuzi wa huyu Mkurugenzi anasema awe mbunifu, najiuliza hivi utapimaje ubunifu wake wakati ndiyo uko kwenye uteuzi? Sina hakika kama unaweza ukapimika ubunifu wa mtu kabla hujampa *task* fulani aifanye. Kwa hiyo, nadhani hapa inahitaji kurekebishwa labda ibaki tu yale maneno mengine kwamba awe na uzoefu na uadilifu, lakini ubunifu sina uhakika kutakuwa na kigezo gani cha kumpima ubunifu wake. Kwa hiyo, nadhani inahitaji kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kifungu cha 21(1)(c) kinazungumzia kuanzisha Kamati ya Kitaifa za kuratibu tafiti za mazao. Mwanzoni kwenye vifungu vingine inaeleza mfumo wa taasisi, kutakuwa kuna Bodi, kutakuwa kuna

Menejimenti, kutakuwa kuna Baraza la Ushauri la Utafiti la Kitaifa, lakini huku tena mnasema kutakuwa kuna Kamati za Kitaifa za kuratibu utafiti wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunaweza tukawa na Kamati na Mabaraza mengi ambayo mwisho wa siku ukiyapima au pamoja kuyapima yatakuwa na gharama kubwa za uendeshaji lakini ukipima hata matokeo yake yanaweza mengine yanaingiliana kazi zake au majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani ama Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi wakati anahitimisha ama hili liweze kufanyiwa marekebisho na kuona namna gani linaondolewa ili kupunguza hizi Kamati na haya Mabaraza ambayo yamekuwa mengi, mwisho wa siku inagharimu fedha nyingi ikiwa na matokeo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimalizie tu kwa kusema kwamba ni lazima Serikali iangalie umuhimu wa kuwezesha hizi taasisi ambazo zimekuwa zikianzishwa, siyo tu kuwapa fedha za mishahara, fedha nyingine za *OC,* lakini fedha za maendeleo hamuwapi. Kwa hiyo, ni lazima Serikali muwajibike kuwapa fedha ili hiki kinachokusudiwa katika Muswada huu na kuwalenga Watanzania asilimia 73 ambao wao wanategemea kilimo, basi kiweze kuwa na tija na manufaa, kwao binafsi, jamii zao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara, wajiandae Mheshimiwa Sakaya na Mheshimiwa Ester Mmasi.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Utafiti wowote, ukitaja tu neno utafiti kwa lugha ya kawaida mtu anategemea kwamba ni kazi ambayo inafanyika kujibu baadhi ya matatizo au kuleta mafanikio au kuboresha. Kwa namna yoyote ile lazima kuwe na kitu kinafanya utafiti ufanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia tu uanzishwaji wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na sitaenda sehemu nyingine ile. Pamoja na kwamba nimepata marekebisho ya Serikali, lakini nina shida ya mwanzoni kabisa hapo anapozungumzia hii *section* ya kwanza tu, mwanzoni walikuwa wamesema kwamba sheria hii itatumika Tanzania, lakini baadaye wameandika kwenye Ibara ya kwanza wanasema ni Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni walikuwa hawajasema inatumika wapi ndiyo wamefanya marekebisho kwenye *schedule of amendment* ambayo ninayo hapa wakasema itafanya kazi Tanzania Bara. Ukisoma Katiba ya Tanzania Nyongeza ya Kwanza katika mambo ya Muungano neno la 18

inaonesha kwamba utafiti ni jambo la Muungano. Ikishakuwa jambo la Muungano sasa vinginevyo Waziri aje anieleze au alieleze Bunge na Watanzania waelewe wanapozungumza hili jambo ni miongoni mwa mambo ya Muungano halafu baadaye unaleta sheria ambayo inasema itatumika Tanzania Bara, unataka kuniambia kwamba ni kauli ya Waziri alichokiandika hapa ndiyo inafanya kazi au ni Katiba ndiyo inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati gani neno utafiti linakuwa jambo la Muungano na ni wakati gani neno hili linakuwa siyo la Muungano. Tukisema ni jambo la Muungano maana yake inabidi uende kwenye Katiba Ibara 98 ambayo inaeleza namna ambavyo sheria hii inapaswa kupitishwa. Sasa kama ni jambo la Muungano kwenye Ibara ya 98 ya Katiba ya nchi inaeleza kwamba jambo hili litapitishwa kwa 2/3 ya Wabunge wa Tanzania Zanzibar na kwa 2/3 ya Bunge hili la Tanzania kama hivi tulivyo humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mambo haya yameshafanyika maana yake vinginevyo maelezo yaletwe kwa nini inageuzwa hapa, kama wenzetu wa Zanzibar waliwahi kujadili jambo hili kama ambavyo imefanyika katika maeneo mengine kwenye Ibara hizi basi ni muhimu. Vinginevyo huu Muswada maana yake utakuwa haujatimiza vigezo ilibidi uahirishwe ili Katiba ifuatwe na uletwe hapa pia. Sasa nitategemea kwamba kabla ya kwenda mbele haya mambo inabidi yatolewe ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye huu Muswada wa Sheria ukisoma hapa sijajua Waziri anamaanisha nini, nimejaribu kuangalia hivi nini malengo yake! nimesoma mwanzo mpaka mwisho haya mapendekezo ya Muswada wa Sheria hii inaonesha kwamba bado mambo ya msingi hayatajibiwa. Kwa mfano, wakulima wa kawaida wa Tanzania hata kama ni wa mahindi, korosho wanatarajia ukitaja tu, kwamba sasa Tanzania inakuwa na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo yaani waone sasa shida ya mbegu mbovu haitakuwepo, hilo jibu kama Watanzania kupata sijaliona hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watumia mbolea wanataka waone kwamba taasisi hii ikiwa imeimarika sasa itasaidia kuboresha kwamba mbolea itakayotumika haitaharibu ardhi yao, yaani kuchujuka kwa muda fulani baada ya kutumia mbolea zetu za kawaida, hayo majibu inabidi yawepo. Sheria inabidi pia itaje kwamba hivi uchumi wa Tanzania *economic growth* itakuwaje kama kuna taasisi ambazo zita-*control* mambo hayo, mambo ya msingi mimi sikuyaona hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji, *(productivity)* kwamba hii sheria inawezaje kusaidia Watanzania kuboresha mazao yao wazalishe kwa faida na walime kilimo cha kisasa hayo mambo hapa sikuyaona. Kilimo cha kisasa kwamba angalau ipendekeze kusimamia mambo gani kufanya watu wasilime

kutegemea mvua ya kawaida baada ya utafiti wa tasnia ya kilimo hii watu watalima kwa kutumia mvua ya kawaida au umwagiliaji au nini, hayo mambo yote ya msingi hapa hayajajibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tulitegemea malengo ya sheria hii lazima yaoneshe kwamba *contributional agriculture research* kuleta kilimo cha kisasa itasaidia nini hii taasisi. Mambo haya ni mambo ya kawaida kabisa kwamba angalau katika malengo ya sheria Mtanzania wa kawaida bila kuwa Mtaalam, bila kuwa Mbunge, mkulima wa kawaida huko aliko awe na matumaini na atamani kwamba sheria ikipitishwa moja kwa moja ananufaika bila kumuuliza Waziri, bila kumuuliza Mbunge, kwa maneno tu ya mazungumzo humu ndani, mambo hayo sikuyaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sheria hii itawasaidia nini wakulima wa Tanzania kwa kuanzishwa kwa mambo ya soko *(market economy)* inawajibika vipi kutafuta soko la wakulima wetu, hilo pia katika mazingira hayo sikuona chochote hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile usalama wa mbegu zetu na mazao wamesema wenzangum wamelalamika kwamba nchi hii kumekuwa watu wanalima mazao kwa sababu hatusindiki mazao yetu yanaharibika, thamani yake inashuka, haya mambo yote yalipaswa yawepo maana yake inapendekezwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Tanzania, sasa haya mambo yote ya usalama sikuyaona mahali popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *cost effectiveness* sijaona teknolojia itasaidia vipi kwenye teknolojia ya kisasa wakulima walime; teknolojia gani itumike ku-*control* bei yake na vitu vingine vya namna hiyo, hayo mambo yote sijayaona. Mamlaka ya Taasisi ya Utafiti itakuwaje *coordinating* ata-*oversee* namna gani au atatoa *guidance* namna gani katika taasisi zingine za utafiti wa mambo ya kilimo hilo sikuliona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilivyozungumza hapa sikuona mahali ambapo inaonesha kwamba kuna mambo ya ku-*control* mbegu kama nilivyosema. Wenzetu kama Waganda wana taasisi wanayo *National Crop Resource Research Institution*. Hapa tunazungumza lakini ukiangalia kwa namna yeyote ile inabidi ihusiane na mambo ya mifugo hivi kwa sababu huwezi kuzungumza habari ya kilimo bila kuzungumza habari ya mifugo, maana yake ndiyo chakula chao, hivi vitu vinategemeana sana. Leo kuna ugomvi katika maeneo mbalimbali sasa utasaidiaje katika mazingira hayo. Hayo mambo mengine nimeona nizungumze.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo pili ambalo nataka nilizungumze hapa sijaliona kwenye haya mapendekezo usalama wa chakula chetu nimesema,

lakini vilevile hii sheria lazima ionyeshe kwamba taasisi itasaidia kupunguza umaskini wa Watanzania uliokithiri, tumeona mashahidi hapa juzi kama hii taasisi ikiwepo je, wale watu ambao wanalima nyanya hapa Kilosa hivi halafu ngombe wanakula, hivi hii itasaidia nini katika mambo hayo. Walime mazao gani kwa wakati gani na soko likoje na hao wana-*link*, maana yake kwenye sheria hapo wameonesha tu kwamba anaweza mtu akafanya utafiti kutoka nje, lakini hawaoneshi kwamba tunaweza tukafanya utafiti Tanzania tukaunganisha na sehemu nyingine tukaboresha kilimo chetu kiwe cha kisasa. Hiyo na yenyewe haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inasema tu kwamba wanaweza wakaruhusu mtu ambaye siyo Mtanzania akaja akafanya utafiti na akishafanya utafiti; je, wenzetu mbona hamsemi sheria itaruhusu hawa na wenyewe wafanye utafiti mahali popote, waende wakope teknolojia ya kisasa waboreshe kilimo chetu ili tuweze kushindana na nchi zingine, hilo jambo pia silioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sheria haisemi hapa kuna adhabu nyingi sana zimeoneshwa, kwa mfano haioneshi kwamba hii sheria itaifanya Taasisi ya Kilimo iwe ni kitu shirikishi, haioneshi kwamba kama kutakuwa na *transparency,* haioneshi kwamba mwananchi wa kawaida, mkulima wa kawaida kama ana malalamiko!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnajua mbolea zinaletwa hapa wenzetu wakulima wa pamba wamesema, wanapewa mbegu za pamba zinaharibu ardhi yao, zingine hata hazioti, hiyo *transparency,* uwezo wa mkulima wa kawaida kuhoji na kupata taarifa kwenye taasisi ya utafiti wa kilimo nakulalamika, hapa vilevile sioni jambo hilo. *Integrity* ya hii italindwa namna gani, *accountability* ya hawa watu wote wanaohusika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshangaa sana nchi hii ina Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, chuo ambacho ni chuo kikongwe katika Afrika Mashariki na Kati, lakini hii sheria inaletwa hapa ya kuunda Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ambayo haigusi au haitaji kabisa kwamba *SUA* ina mchango wowote, nimeshangaa sana! Maana yake wanataka kutuambia hawa wataalam wetu ambao wapo siku zote hamtambui mchango wao, najua hawa ndiyo benki yetu ya mawazo, hawa wana uzoefu wa muda mrefu sana, wangeweza kutushauri namna ya kwenda mbele, mambo gani yamekosewa na hawa ndiyo tumewapa *task* hiyo kwa muda mrefu na Wakufunzi wengi nchi hii wametoka pale. Mambo haya ningeomba nimshauri Mheshimiwa Waziri mnapoleta sheria kama hizi, haya mnazungumzia maisha ya wakulima wa Tanzania, wafanyabiashara na watu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine wamependekeza maneno mengi, sikuona wanasema hawa kama watafanya utafiti kwenye taasisi ya kilimo, kilimo ni chakula, hawaoneshi kwamba watashirikiana namna gani hata na hii Mamlaka ya Chakula Tanzania, hawatajwi katika hii sheria mahali popote, nimesoma sikuona. Sasa mambo kama haya nadhani na wengine watakaofuata hata hiyo Miswada inayofuata ya kesho ule wa *Fisheries,* ni lazima mkileta Muswada hapa hata kama mmeandika Kiswahili/Kingereza mwananchi wa kawaida aweze kuona, hivi ananufaika namna gani bila kuhoji bila kuuliza, kukusikiliza tu ataona kwamba hii kitu kweli ni ukombozi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Magdalena Sakaya, wajiandae Mheshimiwa Ester Mmasi, Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mheshimiwa Gregory Flatei na Mheshimiwa Ulega.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Muswada ulioko mbele yetu na mchango wangu utajikita kwenye Muswada wa kuanzisha Taasisi ya Utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Muswada huu nilipoenda kwenye lile jedwali namba tatu, nikaangalia maeneo ya utafiti nikaona *almost* tume-*cover* mambo mengi sana, ukiangalia karibu kila kitu, kwenye uboreshaji wa mazao, afya ya mimea, utafiti, mavuno, matumizi ya ardhi kilimo, usimamizi, mambo mengi yamekuwa *covered.* Nilipokuja kwenye namba 26 namna ya kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza yote haya yaliyoko hapa karibu mambo 11 sioni dalili za kutekelezwa kwa mambo hayo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukiangalia *source* za fedha ni hiyo mikopo, ruzuku ya Serikali, kuangalia ruzuku itakayopangwa, posho, sheria hii tunataka ituambie namna gani fedha zitapatikana kutekeleza hapa. Mimi nina imani kwa kupitia sheria hii kama kweli tutapata fedha za kutosha, tumekuwa na magonjwa ya mimea ya muda mrefu, tuna magonjwa ya migomba kule Bukoba zaidi ya miaka 20 utafiti hautoi majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna magonjwa ya machungwa leo hatusafirishi machungwa nje kutokana na kwamba magonjwa hayapatiwi majibu. Tuna magonjwa ya mihogo, tuna magonjwa ya nazi, hatuwezi kama hatuna namna ya kupata fedha za kutosha. Kwa hiyo, shida kubwa ya Muswada huu hakuna namna ya kupata fedha kutekeleza haya yaliyoainishwa yote kwenye hili Jedwali Namba Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na Vyuo vyetu vingi tu vya utafiti hapa nchini vyuo vilikuwa 16 vyote leo tunaambiwa vitakuwa chini ya hii Taasisi ya Utafiti, Vyuo hivi siyo kama vilikuwa havina wataalam, vilikuwa na wataalam wa kutosha, wana majengo yao mazuri, tatizo ni *financial support*. Kuna wataalam wenye uwezo, kuna Madokta lakini tatizo hakuna fedha, hakuna vitendea kazi, hakuna madawa ya maabara, matokeo yake vimekuwepo kama ni picha. Kwa hiyo ni lazima kwanza sheria hii ituambie namna gani tunapata fedha za kutosha kuweza kuendesha Taasisi ya Utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliweka utaratibu ndani ya nchi yetu kuhakikisha kwamba angalau asilimia moja ya mapato ya nchi ndani ya mwaka yanakwenda *COSTECH* hatujaweza kufika hata hapo. Kwa hiyo, hata tungekuja na sheria nyingi kiasi gani, kama hatutoi fedha, hakuna utafiti usiokuwa na fedha, hakuna mafanikio ya utafiti ambao haujawekezwa, kuwa na utafiti ni kuwekeza vya kutosha. Nimeona hiyo ndiyo kwanza shida kubwa sana kwenye Muswada wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na maoni yaliyotolewa kwamba lazima tuje na Mfuko Maalum wa Utafiti, tuwe na nidhamu nao na uwe *ring fenced* tuhakikishe kwamba fedha inakuwepo. Leo hii tunaposema tunaingiza mpaka mambo ya mazingira, nimeshukuru sana kwamba angalau sasa tunaanza kuoanisha hata kilimo na mazingira, kilimo na mabadiliko ya tabianchi, kilimo na matumizi bora ya ardhi, ni mambo mengi lakini kwa namna gani? Naomba sana sheria hii ingeanza kwanza namna gani tunapata fedha, hapo ningejisikia burudani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Mheshimiwa Waziri hapa atuambie namna gani tunapata fedha ya uhakika, siyo tunasema tu kwenye bajeti ya Bunge, kwani miaka yote hatutengi, tunatenga lakini haiendi! Mara tozo haziendi, hivyo kwanza ni *financial support* namna gani tunawekeza kwenye taasisi hii iweze kuwa na mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nikienda kwenye Muswada wenyewe sasa kwenye baadhi ya vifungu, kwenye Kifungu cha nne (4), kinasema kuhamasisha matumizi ya uzalishaji mbegu. Hapa ni kweli tumekuwa na shida katika nchi yetu kwa muda mrefu, asilimia 60 ya mbegu za Tanzania zinatoka nje na ni makampuni ya nje, mbegu zetu nyingi zimedumaa, leo ukienda kwenye maduka ya mbegu za mazao wanakwambia kabisa tunataka mbegu fulani kwanza zile za nje ni *expensive,* watu hawawezi kuzimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pamoja na hiyo wafanyabiashara wale wanakwenda mpaka vijijini kwenda kuhamasisha zinanunuliwa. Kwa hiyo ni *expensive* halafu nyingine zinafanyiwa majaribio kwa kuwa hakuna utafiti ambao unatangulia. Ningeshukuru sana, kwa kupitia Muswada huu nina imani

sasa tutakuwa na uhakika tunazalisha mbegu ndani ya nchi yetu za kutosha, lakini pia wananchi wetu wahamasishwe watumie mbegu za ndani ya nchi yetu na hivyo tuhakikishe kwamba tunajitosheleza vya kutosha kwa kutumia mbegu za mazao kutoka ndani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha tano (5) napendekeza wale Wajumbe wa Bodi lazima kuwepo angalau Mwakilishi kutoka kila Kanda, hii kusema kwamba Mwakilishi mmoja awakilishe wakulima sikubaliani nayo! Kwa sababu wawakilishi wa kila Kanda watasaidia, leo mkulima wa korosho kule Kanda ya Kusini hawezi kujua changamoto za mkulima wa tumbaku kule Tabora. Mkulima wa mahindi kule Mbeya hawezi kujua changamoto za mtu anayelima mwani labda yuko upande wa Pwani. Kwa hiyo, lazima kila Kanda itoe Mwakilishi wanapokaa kwenye Bodi kila mmoja aainishe changamoto za Kanda yake na mazao yanayozalishwa kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha saba (7) posho za Wajumbe. Huwezi kusema kama Wajumbe wapendekeze posho, Waziri aende aidhinishe hapana! Wanajipendekezea posho kwa nini? Lazima kuwepo chombo kinachopendekeza posho, leo Mjumbe wa Bodi hawezi kujipendekezea posho mwenyewe, lazima kuwepo na chombo kinachopendekeza washauriane na Waziri wakubaliane tusitoe *loophole*. Wanaweza wakasema kila mmoja milioni mbili kwa siku siyo wao wenyewe? Tusiwape *loophole* hiyo tunataka fedha nyingi ziende kwenye kazi husika siyo kwenda kulipana posho kwenye vikao mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 10(4) pia napendekeza kwenye Baraza la Taasisi lazima kuwepo Wajumbe kutoka kila Kanda tofauti na wanavyosema hapa ni Mjumbe mmoja wa kuwakilisha Wakulima kwa maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 22 kusajili miradi utafiti wa kilimo na utoaji wa huduma. Kifungu hiki ndicho kitakachosaidia sasa kuweza kupata watoaji wa huduma ya kilimo wenye uelewa na weledi. Leo tumekuwa na watu wanaosambaza mbegu za kilimo, wanasambaza mbolea ni *business oriented,* ni wafanyabiashara, hajasoma kilimo, hajui kilimo, hajui msimu, hajui ni madhara namna gani unavyochelewesha mbolea unaathiri nini, unapeleka mbolea muda ambao siyo unaathiri nini. Unapeleka mbegu muda umepita, unaathiri nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia Muswada huu na kifungu hiki, lazima tuainishe sasa watu wenye uwezo wenye weledi, wenye elimu kuweza kutoa huduma za mazao, huduma za kusambaza mbegu, mbolea, hata kwenye manunuzi, mtu ambaye anaona hiyo ni fani yake, tofauti na sasa hivi ambapo mara nyingi tumekuwa tukiwatumia watu ambao ni wafanyabishara,

hawanufaishi wakulima, tunaishia kupata hasara, mwisho wa yote wakulima wetu wanakuja kuwa ni maskini wa kutupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 26 ningependa sana kuhusiana na namna gani, tuna vituo vingine kwa mfano pale *Sokoine University*, kuna taasisi ya *TOSCI* inayoshughulika kuhakikisha kwamba mbegu zinakuwepo za kutosha na ubora wa mbegu, sijaona imeguswa kabisa humu, namna gani sheria hii inashirikisha taasisi nyingine tofauti na vyuo kuweza kufanyakazi kwa pamoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima waone ni namna gani wanafanya kazi kwa pamoja kwa sababu kama mmesema sasa ni kama *umbrella,* taasisi nyingine zote lazima zishirikishwe na wataalam wale washirikishwe kuhakikisha kwamba mwisho wa siku tunaweza kuwa na tija nzuri kwenye sheria hii ambayo imekuja mbele yetu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 29(7)(a) kwa idhini ya kimaandishi ya Waziri anaweza kutumia fedha bila kujali kwamba matumizi hayo hayapo kwenye bajeti yoyote. Naomba kifungu hiki kiondolewe, tumekuwa tunasema hatuna nidhamu ya matumizi ya fedha, fedha tunaipeleka kwenda kwenye shughuli fulani, inatoka inaenda sehemu fulani, haiendi kwenye lengo, leo tunaweka sheria kwamba kwa maandishi ya Waziri anaweza kuagiza Bodi itumie fedha tofauti na bajeti iliyokuwepo. Lazima tuwe na nidhamu ya matumizi ya fedha, hapa tunaweka mwanya tunaweka upenyo namna gani Bodi itumie fedha za miradi bila kuwa na utaratibu wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kifungu hiki kiondoke kwa sababu hakitatusaidia, kwanza tutaleta matatizo, fedha zitaenda kutumika sehemu ambapo haikupangwa kwenda kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tumeambiwa kwamba pale mtu anaomba usajili akinyimwa aende kwa Waziri na Waziri awe ni namba ya mwisho. Hapa naomba Waziri asiwe namba ya mwisho. Inawezekana ikatokea figisu au utaratibu fulani wakamnyima tu huyu mtu kwa makusudi, akienda kwa Waziri na yeye asimsikilize. Kwanza ni muda mrefu wanasema siku 21 anaomba, Waziri ndani ya siku 30 hapo tayari miezi miwili imekwisha mtu anaomba usajili, siku 30 anasubiri majibu, miezi miwili imekwisha kwanza ni muda mrefu, lakini pia Waziri asiwe ni namba ya mwisho. Waziri ni binadamu. Naomba kiwepo chombo kingine. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ester Mmasi, jiandae Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Flatei na Mheshimiwa Ulega.

**MHE. ESTHER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia kwenye Bunge lako hili Tukufu, zaidi nitajikita kwenye Muswada huu wa Sheria ya Uvuvi kama ulivyowasilishwa kwenye kikao chako kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuipongeza Wizara ya Kilimo na Uvuvi, binafsi naona dhamira ya dhati kwa viongozi hawa wawili. Mimi mwenyewe nikiwa na Mheshimiwa Charles Tizeba pamoja na Naibu wake tumefanya vikao na Taasisi za Elimu ya Juu kwa maana ya *graduates* kwa mikoa sita na hii ni *phase* ya kwanza. Kwa utaratibu wa Wizara ambao wameuweka, naona dhamira ya dhati katika kuona kwamba vijana wetu wanaingia mashambani wanalima, pia watakapoingia kwenye mabwawa yao ya samaki wavune samaki. Pongezi zangu za dhati kwa Viongozi wangu Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, Kaka yangu Mheshimiwa Ole-Nasha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kabisa moja kwa moja kuchangia Muswada huu mzuri ambao umeletwa kwetu ili kwa pamoja tuweze kuona uchumi wa nchi yetu unaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kabisa kwenye *Clause 6(1),* nitapenda pale kwenye *section (a)* tuweze kuongeza baadhi ya maneno. Hii nasema ili tuwe na *continuity* nzuri. Ukisoma *section (b)* na *(c)* utaona kila kwenye *function* ya hii *institute* kunakuwa na maana; yaani kazi, jukumu la taasisi pamoja na maana halisi ya jukumu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitapenda kwenye *section (a)* ambayo inasema kwamba, "*the function of the institute shall be to carry out and promote the carrying out of the enquiries, experiments and research in fisheries and aquaculture and generally.*" Kwa hiyo, naomba hapa tuongeze maneno yafuatayo, kwamba, moja ya jukumu la hii taasisi ni pamoja na

*"carry out and promote the carrying out of the experiment and research so as to provide scientific data and information to enhance sustainable exploitation management and conservation of Tanzanian fisheries resources and promote aquatic environment of Tanzania. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, nikienda kwenye ile *Clause 6(3),* hapa tunaongelea ushirikishwaji wa taasisi nyeti katika utafiti wa viumbe vya baharini. Ameliongelea pale Mheshimiwa mwenzangu aliyenitangulia, dada yangu Mheshimiwa Sakaya kwamba tuone sasa Serikali kupitia Muswada huu,

taasisi za elimu ya juu zishirikishwe na zitumike kikamilifu katika nyanja hizi za utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kwanza, mimi ni mdau kwenye taasisi ya Elimu ya Juu, lakini pia uwakilishi wangu, nawakilisha Elimu ya Juu. Nimefanya kazi kwenye Taasisi ya Elimu ya Juu. Pale nimeona ambavyo Walimu wangu wameishia kukata tamaa, wanafanya *research* nzuri sana za kuweza kusaidia hii nchi, lakini *research* hizi zinabaki kufungiwa kwenye makabati. Taasisi za Elimu ya Juu zimekuwa ni *centre of excellence,* lakini hazitumiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara husika iweze kufanya na kupokea haya marekebisho na kuweza kuingiza ushiriki wa taasisi za utafiti, elimu ya juu, kupitia Taasisi ya Tume ya Vyuo Vikuu Nchini Tanzania kuona nao wanakuwa ni sehemu ya wadau katika kutoa ushauri katika Taasisi hii ya *TAFIRI.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja, asije akaniingiza kwenye kipengele (g) kuniambia kwamba, kuna kipengele (g) ambacho kinasema "*and any other person or body of persons established by under any written laws which are performing the same functions as to those specified in sub-section (1).*" Naomba asinipeleke huko.

Taasisi ya Elimu ya Juu ni taasisi nzito na ni taasisi yenye unyeti wa pekee katika masuala mazima ya tafiti katika Muswada huu ninavyouangalia. Kwa hiyo, naomba yenyewe itokee pale kwa uzito wake na kwa upekee kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija *Part III, Clause (8);* pale tunaongelea *Composition and Proceedings of Board*. Kitu ambacho nakiona hapa, "*composition*" ni neno limewekwa pale, lakini ukiangalia kwenye huu mtiririko, sioni *composition* ya *Board of Directors.* Wameanza pale kwa kueleza kwamba, *there shall be a Board of Directors of the Institute, which shall be responsible for the exercise of the functions and the management of the Institute.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unaposema "*there shall be a Board,*" hiyo bodi nani kaiweka? Inawekwa na nani? *Number of Board of Directors,* hatuoni; *appointing authority by the Board of Directors,* hatuoni; *Appointing authority by the Chairperson of that Board,* haipo; *members composition,* hatuioni. Hiyo Bodi inaletwa na nani na inahalalishwa na nani kuwepo pale? Kwa hiyo, tunahitaji maelezo kamili. Katika hili, naomba, Taasisi ya Elimu ya Juu ipewe nafasi yake katika hili suala zima la *Board Composition. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda hapa *Clause 12,* utaona pale kwenye maneno "*Director General and other staff of the Institute,*" hapa tunaongelea

*appointment, functions and power of the DG*. Tunaambiwa kwamba Mheshimiwa Rais ndiye atakuwa na mamlaka ya kumteua *DG* katika taasisi hii na wakatoa pale *academic qualifications. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunaambiwa kwamba, *General Director* anatakiwa awe na *Doctorate Degree in Fisheries* au *Aquaculture*. Hii naomba niseme, inabidi tui-*recast* na badala yake tuseme kwamba, *primary* iwe ni *First Degree and Second Degree in Fisheries or Aquaculture*. Unaposema *Doctorate Degree;* huwezi kupata *discipline* ndani ya *Doctorate Degree*. *Doctorate Degree is all about methodology and tools that has been attained by that particular person.*

Kwa hiyo, kusema kwamba, *a primary* iwe *Doctorate Degree* kwenye *field* hii mimi nakataa. Naomba kwamba *primary* iwe ni *first Degree and second Degree* kwenye *this particular field;* na badala yake tuseme pia kwamba, awe na *first Degree* katika hizo *subjects plus Doctorate Degree in related subject.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Ni kwamba katika *Ph.D level* unaweza ukawa na *candidate* ambaye amefanya *Ph.D* katika *GIS in Marine Ecosystem,* lakini unaweza ukawa na *Ph.D Candidate* ambaye amefanya *GIS* kwenye *Climate Change and Marine Ecosystem,* lakini unaweza ukawa na *Ph.D Candidate* ambaye amefanya *Ph.D* kwenye *Development Studies* na *Fisheries.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwenye suala la *Doctorate Degree* isiwe *primary factor* na badala yake *First Degree* na *Masters Degree* ndiyo iwe *primary* kwa sababu, hapo *the only place tunaweza* ku-*capture discipline*. Huwezi ku-*capture discipline* kwenye *Doctorate Degree,* huwezi! Hapo uta-*capture methodology* na *tools* ambayo haimsaidii mtu katika ku-*head sections* kama hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuongelea masuala ya *Clause 19(1), conduct of research by local researchers.* Hapa tumeona kwamba, *local researcher* anapoenda kwenye *field* ni lazima aandike *proposal,* aombe *request* kwenye taasisi husika; lakini nafikiri ili kuweza ku-*safeguard our marine by diversity* ni vyema kwanza tukaanza na ku-*seek permission.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani? Mtu anaweza aka-*develop proposal* akatumia gharama nyingi na muda, lakini atakapofika ku-*submit* kuomba *permission* akaambiwa haifai na ikawa *redundant.* Kwa maana nyingine, ni vyema kwanza mtu akaanza ku-*seek permission* ndipo aje ku-*develop proposal. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwenye *foreign researchers* tunaambiwa kwamba, *foreign researcher* anatakiwa a-*submit final report upon the completion of that particular research*. Sidhani kama ni sahihi sana kwamba *foreign researcher* anapaswa ku-*submit final* lakini *progressive report* hazipo. Nasema hivi kwa sababu, sisi ni mashahidi, tumeona upotevu mkubwa na uharamia mkubwa kwenye Hifadhi za Taifa, ni kwa sababu, tunakosa *controls.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukikosa *controls* kwenye *ecosystem,* tunataka nini tena? Tumeshanyang'anywa maliasili kule kwenye mbuga zetu za Taifa; tena na kwenye viumbe vya bahari tunyang'anywe kwa sababu tu ya kutokuwa na macho ya kuona vitu kama hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji *control* zilizoimarika. Kwa hiyo, ninaposema kwamba, mtu yeyote atapaswa kuomba *permission,* lakini pia, ku-*submit progressive report,* hii ni sehemu ya *controls* kuona kwamba, tunalinda na kuhifadhi maliasili ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nina suala hapa ambalo Mheshimiwa ndugu yangu pale Halima Mdee jana aliliongelea, lakini sijui ilikwendaje, niseme tu tusione shida, hata kama mkipitisha kwangu, tusione shida, ipitishwe tu. Jana ndugu yangu pale, Mheshimiwa Halima Mdee alihoji, nami hapa nahoji…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakunda, ajiandae Mheshimiwa Flatei na Mheshimiwa Ulega. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami pia, nitoe pongezi nyingi sana kwa Serikali, hasa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Tizeba, kwa kuleta Muswada huu katika kipindi hiki muhimu kabisa. Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya mwaka 2016 pamoja na ile ya Uvuvi ni Miswada muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilikuwa nasema mara nyingi kwamba kazi za msingi za Serikali duniani kote kwenye Sekta ya Kilimo ni tatu kubwa; na katika kazi hizo tatu, ya kwanza kabisa ni utafiti; halafu ya pili ni kuwasaidia wakulima wapate mikopo, pembejeo, vifaa vya kilimo cha kisasa na ya tatu kuwalinda wakulima wapate jasho lao halali; wasinyonywe na wafanyabiashara wenye mbinu chafu ambao lengo lao ni kupata faida peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kazi hii ya msingi ambayo ni ya utafiti, naomba Serikali kama ambavyo imeleta Muswada huu, itoe kipaumbele cha

kutosha kwa taasisi hii ya utafiti ili kusudi sheria hii ijitosheleze na taasisi ya utafiti itakapoanza kazi zake, ifanye kazi zake kwa ufanisi unaotegemewa. Kwanza, tafiti zifanyike; pili, taarifa za utafiti zitumike kwa ajili ya maendeleo; mafunzo kuhusu matumizi ya taarifa za utafiti yasiwe kwa wataalam peke yao, bali yafikishwe mpaka kwa wadau wakiwemo wakulima; masuala ya teknolojia yawekewe umuhimu wa kipekee na yasimamiwe vizuri ili teknolojia itumike kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii na teknolojia ni sehemu ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wananchi wetu watabaki kutumia teknolojia zile zile za miaka yote; za tangu mwaka 1947 hatutafika popote. Vile vile bila utafiti kuhusisha masoko, mafanikio ya kilimo yatakuwa kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sina sababu ya kuchukua muda wako mrefu sana kujadili kitu ambacho ni kizuri sana. Nimepitia sheria yote, miundo ya usimamizi iko vizuri na mambo mengi sana yamewekwa vizuri na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naipongeza vile vile Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kushauri. Pia naipongeza Serikali kwa mambo mengi ambayo Kamati imeshauri wameyaweka kwenye *schedule of amendment*. Kwa hiyo, kwa kweli, nawapongeza sana kwa hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele kimoja ambacho ningependa kukitilia umuhimu wa kipekee ni *source of financing*. Vyanzo vya fedha vya taasisi hii ni kama vimefichwa. Naomba Serikali iweke wazi; kama nilivyosema, jukumu la kwanza kabisa la Serikali la msingi kwenye Sekta ya Kilimo ni Utafiti; ni lazima kuwe na Mfuko utakaosaidia tafiti za kilimo na Serikali itoe mchango mkubwa wa kibajeti kwenye Mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na taasisi huru kusiifanye taasisi hiyo iachwe kama yatima, iwe ndiyo kisingizio cha kutoipangia bajeti inayotosha kwa sababu wataachiwa wadau, wakiwemo wakulima kwamba sasa mazao yao yakatwe makato ili kusudi kuipa fedha Taasisi ya Utafiti. Naomba hili liwe wazi kabisa, Serikali ikubali kuweka Mfuko Maalum wa Utafiti na yenyewe ichangie zaidi ya asilimia 90 ya bajeti kwa ajili ya Mfuko huo na wadau wengine wataongeza pale ambapo patabaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusu uwakilishi wa wakulima kwenye vyombo vya usimamizi, umetajwa vizuri, napongeza sana; lakini kama sifa za wale wakulima watakaowakilishwa hazitaainishwa vizuri kwenye sheria, basi unaweza ukawa na mwakilishi ambaye mchango wake ni hafifu. Kwanza, mwakilishi lazima ajue maana ya utafiti na awe na uzoefu nao ili kusudi mchango wake uwe mzuri kwenye vikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda nizungumzie hapa ni uhusiano wa taasisi hii tunayoanzisha na taasisi nyingine zinazosimamia utafiti hapa nchini. Kamati ilizungumza sana kuhusu uhusiano na *COSTECH,* nami naongezea hapa, uhusiano kati ya taasisi hii tunayoanzisha na *NIMR*. Najua *NIMR* inasimamia tafiti za afya, lakini kuna baadhi ya mambo yanayohusu tafiti za afya yanahusu kilimo. Kwa mfano, kuenea kwa malaria inawezekana ikawa na uhusiano wa karibu sana na maendeleo ya kilimo, kwa sababu, malaria wale wakulima wanakolima ni kwenye maji na kwenye maji ndipo kunapozalishwa mbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo uwezekano tafiti zikagongana kati ya tafiti za afya na tafiti za kilimo. Kwa hiyo, uhusiano ni muhimu sana uwekwe vizuri kwenye hii sheria kwamba watahusianaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile *COSTECH*, ukisoma vizuri Sheria ya *COSTECH,* inaonesha kwamba, *COSTECH* ndiyo msimamizi mkuu wa tafiti zote, ukiacha zile za afya ambazo zinasimamiwa na *NIMR*. Kwa hiyo, mtafiti yeyote kwa mfano anayetoka nje akija Tanzania hapa kama anafanya utafiti; ukiwemo utafiti wa kilimo, lazima ajisajili *COSTECH* na afanye mtihani wa *COSTECH,* afaulu, ndiyo aruhusiwe kwenda kufanya utafiti wake. Kwa hiyo, ni muhimu sana uhusiano ukaelezwa vizuri kwenye sheria ili kusudi hapo baadaye kusiwe na mgongano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uzoefu wa kutosha katika hili kwa sababu nilifanya kazi Umoja wa Mataifa, *UNDP* na niliona kwamba *COSTECH* ndiyo msimamizi mkuu wa tafiti zote, ukiacha zile za afya ambazo zinasimamiwa na *NIMR*. Kwa hiyo, uhusiano wa taasisi hizi ambazo tunazianzisha, hii ya kilimo na ile ya uvuvi na *COSTECH* pamoja na *NIMR* ni muhimu sana ukaoneshwa vizuri kwenye sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu pili, la mwisho ni uhusiano wa taasisi hizi za Sekta ya Kilimo na Sekta nyingine wezeshi za kilimo. Mfano, huwezi kuendesha utafiti unaohusu kilimo cha umwagiliaji bila kuhusisha Sekta ya Maji. Sekta ya Maji ndiyo inabeba dhamana ya rasilimali za maji. Kwa hiyo, ni muhimu sana uhusiano ukawa vizuri kwenye sheria ili kusudi kusiwe na migongano na sekta nyingine wezeshi. Ushirikiano uwekwe vizuri na hasa kuwahusisha kwenye Kamati ndogo ndogo zitakazoundwa na kwenye Bodi na kwenye vyombo vingine vya usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mambo mengine, sheria imekaa vizuri. Natoa pongezi na naunga mkono Bunge hili lipitishe sheria ili zianze kutumika haraka iwezekanavyo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei na Mheshimiwa Ulega, jiandae.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu ambao kimsingi unaonesha una matumaini kwa wananchi wetu hasa kwa sehemu hii ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapotazama neno "utafiti," napata mwamko mzuri wa kuona kwamba sasa Serikali imekuja na mpango mzuri wa kusaidia jamii yetu; maana ni nini maana ya utafiti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema "utafiti," maana yake ni uchunguzi kuhusu jambo fulani kwa undani. Sasa kwa kuwa, naamini wakulima wetu hasa katika maeneo yetu tumekuwa na mambo mengi ambayo tuna matarajio hasa kuhusu kilimo; na leo Serikali wanapoleta Muswada huu, mimi kwa kweli kama mdau wa kilimo, nimefurahia sana hali hii. Hata hivyo yako maeneo machache ambayo nilipenda kushauri na kuchangia kama mchango wangu humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo hili la uwakilishi. Wameonesha kwamba kuna mwakilishi mmoja wa wakulima, lakini nilikuwa napenda kuona kwamba, kwa nini asiingizwe hata wa pili? Tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda moja kwa moja katika hizi Kanuni za Utafiti. Nimezisoma hapa vizuri sana, lakini ukiangalia na pia, hawa wanaoingia humu; kwa mfano, ukimwangalia kama Mkurugenzi anayetegemea kuteuliwa hapa, anatakiwa awe na sifa na hii inayoonekana kwenye Muswada huu wa sheria ya Kiswahili kwenye *page* ya 41 Kifungu cha 8(c) inaonesha kabisa mtu huyu lazima awe na uzoefu au ujuzi uliothibitika wa miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kabisa kwamba kuna hali ya kupunguza idadi hii ya miaka. Napendekeza kwamba, kwa kuwa miaka 10 ni sawa sawa na miongo miwili ya Mbunge, kwa mfano, mimi nimeingia hapa leo, kwa miongo hii 10 ndiyo unampata mtu ambaye anaweza kuwa na sifa ya kuingia humu kama Mkurungezi. Naishauri Wizara ione namna ya kupunguza huu uzoefu. Kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba muda huo nauona ni mwingi sana; kwa nini isifanywe hata miaka mitano? Uzoefu ukachukuliwa kutoka sasa na mtu basi akaajiriwa kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, utafiti ni jambo zuri sana, lakini zipo tafiti nyingi ambazo zimefanyika maeneo mengi katika vyuo vingi, zimekuwa zikiachwa. Naishauri sasa Wizara ijielekeze na Serikali iweke mazingira mazuri ya

hawa watafiti wetu ili wanapofanya utafiti, basi utafiti huu uchukuliwe kwa jinsi ambavyo wanaweza kupewa motisha. Maeneo mengi kwa nchi nyingine vijana wengi wanaingia katika utafiti kwa sababu wanajua wakifanya utafiti, utafiti huu ukazaa matunda, utafiti pia unalipa kwa maana ya kwamba wanaweka kwenye kumbukumbu za vitabu. Kwa hiyo, niliona niseme haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye taasisi za utafiti naomba kabisa ianzie chini. Hata utafiti huwa unazoelekea; pawe na *co-ordination*. Utafiti na tafiti nyingine huwa zinakaribiana, hata kama ukiwa utafiti wa sayansi ya kilimo, lakini kuna utafiti wa biolojia, kuna tafiti zote hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri paundwe chombo ambacho kitasaidia ku-*coordinate* tafiti hizi. Hii ikishafanyika itakuwa ni jambo zuri ambalo litasaidia watafiti wetu wa hapa nchini kuwa na muunganiko mzuri wa kufanya tafiti zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi tafiti sijaona mahali ambapo panaonesha tafiti hizi zitasaidiaje wananchi wetu? Nawapongeza sana, kwa sababu sisi wakulima tuna matatizo mengi sana, lakini labda matatizo yatatusaidia sasa katika tafiti hizi. Kwa mfano, yapo maeneo mengi ambayo wananchi wetu wanakuwa na kitu kinachoitwa maeneo ya kulima, lakini hawajui kwamba mbegu gani hasa inaweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kwamba, maeneo hayo nitashukuru sana kama tafiti zitasaidia pia kuona kwamba katika maeneo yote ya kule vijijini hawa watafiti watatusaidia, hivi ni mbegu gani na inafaa katika eneo hili? Kwa mfano, maeneo labda ya Babati au eneo fulani na udongo huu wa maeneo haya: Je, unafaa kwa zao gani? Nina uhakika kwamba watafiti hawa wakifika mahali hapo, basi Tanzania yenye kutakiwa kuwa na uchumi wa kati, labda tutaupata kwa njia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende eneo la fedha. Nimeona hapa kwenye eneo la (h), bodi hii inatakiwa kutafuta fedha, ni kweli. Naomba katika bajeti ya Serikali, Serikali ijielekeze yenyewe kutenga bajeti katika utafiti. Usipotenga bajeti na sisi Wabunge tukawa hapa tunapitisha sheria hii leo, kwa makofi, tutatafuta namna ya kuunda Bodi, tunaajiri Wakurugenzi lakini mwisho kama sisi Wabunge hatutatenga bajeti ya kuwezesha utafiti, sina uhakika kama utafiti huu utazaa matunda ya kwenda moja kwa moja kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika bajeti ijayo; najua bajeti imeshapita; Serikali iweke mazingira wezeshi na kutenga bajeti ya kuwasaidia hawa watafiti ili bajeti itakapokuwa wezeshi, utafiti utafanikiwa; na maeneo haya yatakuwa na afadhali kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijielekeze tena kuiomba Serikali; mara nyingi tunakwenda kusoma masomo haya ya utafiti kwenye *high level,* lakini ushauri wangu, kwa nini basi usianze huku chini? Nchi za wengine, wanaanza utafiti kwenye masomo ya msingi kabisa na mtu akifika sekondari amekomaa kwa jambo la utafiti. Kwa hiyo, kunakuwa na *co-ordination* kutoka maeneo haya; tutakuwa tunahamasisha vijana wetu kufanya utafiti. Waingereza wana msemo wao wanasema, *"if you have no research, you have no right to speak."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii basi, naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu. Kubwa zaidi naomba Wizara pia itusaidie; hawa watafiti wanaofanya mambo ambayo yanaonekana yapo vizuri, tuwe na mpango basi wa kuisaidia bodi hii na watafiti wa nchini kwetu kuwapa tuzo, pawepo na tuzo. Katika historia ya Tanzania sijaona mahali popote hata kwenye Muswada nimeangalia, hakuna mahali pa kumpa hata motisha mtafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia haya ili hata haya yakawe yanawezekana kwamba mtafiti apewe na motisha na Serikali yenyewe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ulega! Mheshimiwa Chuachua, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Japhet Hasunga na Mheshimiwa Jackline Msongozi wajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali kwa kuja na Miswada hii miwili ambayo ni Miswada muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu. Tumeona kabisa katika Miswada hii taasisi hizi inaonekana zitafanya kazi ya kufanya utafiti katika masuala ya kilimo na masuala ya uvuvi lakini pia itadhibiti na kuratibu shughuli zote zinazohusiana na maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Miswada imekuja kwa wakati muafaka, lakini naomba nichangie kwa maeneo machache. Nianze na maeneo ya jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hii Miswada yote miwili na mambo ambayo yanaelezwa katika hii Miswada miwili ni mazuri sana. Nianze kwanza na ukubwa wa Bodi. Nimekuwa nikisema na tutaendelea kusema, kwamba Bodi hizi ni gharama kubwa kuziendesha; Bodi hizi zinatumia fedha ya walipa kodi; na Bodi hizi zikiwa kubwa kiasi hiki, ufanisi wake unakuwa ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye hii sheria imeandikwa Bodi itakuwa na wajumbe tisa, ukijumlisha na Mwenyekiti pamoja na Mkurugenzi wanakuwa 11. Hiyo Bodi ni kubwa sana. Bodi hizi zikiwa kubwa namna hii, zinatuletea matatizo. Zinaongeza gharama za uendeshaji kwenye Serikali. Kwa hiyo, naomba waliangalie upya, hakuna sababu yoyote Bodi kuwa kubwa kiasi

hicho. Bodi nzuri zinakuwa na Wajumbe wanne na Mwenyekiti labda na Mkurugenzi, wanakuwa sita *maximum*; lakini Bodi ya Wajumbe 11, kidogo inanipa wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimeona katika muundo wa hizi taasisi, ni taasisi za utafiti nakubali, lakini najua kabisa katika hizi taasisi, nyingi ikiwemo Chuo cha Kilimo Uyole na vingine vingi, vilikuwa pia vinafanya kazi ya kutoa wataalam wanaohusiana na masuala ya kilimo na masuala mbalimbali. Wataalam hawa wa mafunzo mbalimbali ambayo walikuwa wanayatoa yalikuwa yanatolewa halafu wanasajiliwa, yanatambulika katika nchi. Vyuo hivi vilikuwa vimesajiliwa na Baraza la Taifa la Vyuo vya Ufundi *(NACTE)* na hivyo mafunzo waliyokuwa wanayatoa, iwe ni katika Astashahada au katika Stashahada au katika ngazi nyingine yoyote ni mafunzo yaliyokuwa yanatambulika na bado ilikuwa ni kazi muhimu sana katika kuchangia kupatikana kwa wataalam katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika huu Muswada sijaona mahali ambapo wanagusa hizi kazi kwamba pamoja na kazi za utafiti, lakini pia vyuo hivi vitafanya kazi ya kuzalisha hawa wataalam ambao tunawahitaji sana katika haya maeneo. Kwa hiyo, nafikiri ni suala la kuliangalia pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo, hizi taasisi ni nani atakayekuwa anazisimamia? Taasisi za Elimu ya Juu tunajua kwamba kuna *TCU* wanazisimamia; taasisi nyingine za mafunzo tunajua kuna *NACTE* wanazisajili, wanazisimamia. Hizi taasisi za utafiti, ni nani ambaye ni *regulator* wa hizi taasisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vitafuata muundo wa Baraza la Taifa la Vyuo vya Ufundi *(NACTE)* maana yake hata muundo wake lazima ufuate ule muundo ambao ulishapitishwa wa taasisi hizo. Ambapo kunakuwa na *Director General* au Mkuu wa Chuo, anakuwa na wasaidizi wake, inaeleweka kabisa na muundo upo wazi wazi. Sasa hii tunayoiweka kwenye hii taasisi moja naona kunakuwa; mmesema kutakuwa na Naibu Mkurugenzi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna Mkurugenzi Mkuu anateuliwa na Rais, Naibu Mkurugenzi Mkuu anateuliwa na Waziri, Wakurugenzi wanateuliwa na Bodi. Naona kama tunajaza mambo ambayo yataleta migongano mbele ya safari kiutendaji. Yatagonganisha tu! Mtu atashindwa kutekeleza majukumu yake anasema bwana kwa nini unaniambia hivi? Wewe umeteuliwa na Rais, nami nimeteuliwa na Waziri; inaleta migongano. Kwa nini huyu Naibu sasa asiteuliwe na Bodi? Kwa nini tuweke mpaka hadi aende kuteuliwa na Waziri? Mimi sioni sababu. Nafikiri hilo kuna haja ya kuliangalia vizuri ili muundo wao uwe ni mzuri na uendane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata kwenye taasisi ya kilimo, nimeona hakuna Naibu, lakini naamini kabisa wale Wakurugenzi wanatosha kabisa na wale watakaosimamia vile vyuo ambavyo vimezungumziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 22 mpaka 25 kimetoa masharti kwa watafiti wote watakaofanya utafiti wa masuala ya kilimo, wote lazima wasajiliwe na hii taasisi. Pia miradi watakayokwenda kuifanyia utafiti lazima isajiliwe, ni kitu kizuri tu, sina matatizo, isipokuwa naangalia, wapo watu walikuwa wanafanya utafiti wa masuala ya kilimo, wapo wanafunzi wanaosoma kwenye vyuo vyetu wanafanya utafiti huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, sasa tunataka kusema kwamba, hawa vijana ambao wanasoma au mtu kama yupo shuleni anasoma na anasoma *Ph.D* kwenye haya masuala, ni lazima kwanza akapate kibali kwenye hii taasisi ndiyo aendelee na utafiti. Sasa hilo naliona kidogo kama linakinzana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwamba kuna haja ya kuangalia vizuri hizi ili kusudi tunaposema kwamba kila utafiti lazima usimamiwe, nakubaliana, lakini kuwe na utaratibu unaoeleweka kwa wale ambao wapo kwenye mafunzo ili kusudi tuepukane na matatizo ambayo tumekuwa tukikutana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa tumekuwa na matatizo mengi sana. Tumeona kwa mfano, mwaka jana na mwaka juzi kule kwetu ilitokea kule Mbeya, watu walikuwa kwenye utafiti, wamefanya utafiti, wamepata mbegu mbovu, mbegu mbaya, badala ya kuzitupa, wamepeleka sokoni, wamewauzia wananchi wetu. Wamenunua mbegu mbaya na hadi ikaharibu kabisa kilimo. Sasa hiki siyo kitu kizuri, kwa hiyo, ni suala la msingi ambalo lazima tuliangalie katika mtazamo huo wa kudhibiti mambo yanayoendana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Miswada hii haijaonesha namna tutakavyokuwa tunashirikiana na vyuo vingine kama Chuo Kikuu cha Kilimo. Kwenye huu Muswada haijataja tutakuwa tunashirikiana nao vipi? Wale wataalam ambao wapo kule, watashiriki vipi katika hii taasisi? Kwa hiyo, nafikiri kuna haja ya kuliangalia vizuri na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nataka kuzungumzia kuhusu mapato. Katika taasisi yoyote kuna mapato yanayotokana na shughuli wanazozifanya, lakini pia kuna mapato ya ushauri na pia kuna mapato yanayotokana na utafiti, yaani *funded research*. Zile *funded research* nimeangalia katika vile vyanzo haijazungumzwa. Ule ushauri wa kitaalam watakaokuwa wanatoa, haujazungumzwa pale. Sasa nafikiri kwamba ni vyema

wakaangalia ili kusudi viweze navyo kuwa ni sehemu ya mapato ya taasisi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo sijafurahishwa nalo, nimeona kwenye taasisi hizi sheria inasema watarithi mali na madeni ya taasisi zilizokuwepo. Tunapoanzisha taasisi kama hizi, tukisema zirithi na madeni yaliyokuwepo kwenye vyuo hivyo, vitashindwa kusonga mbele. Hayo madeni Serikali ingeyachukua ili vikianza vianze *fresh* badala ya kurithi madeni. Hili sioni kama linakuja vizuri. Kwa hiyo, ni suala la kuliangalia vizuri badala ya kurithi na madeni ambayo yapo nafikiri tungekuwa na utaratibu mwingine ambao ungeweza kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeona kwenye adhabu zinazotolewa katika utekelezaji wa hizi sheria. Adhabu hizi napendekeza ziangaliwe vizuri. Naona kuna adhabu unakuta kwamba wanasema *fine* ya fedha, shilingi milioni 20; kifungo ni mwaka mmoja, *fine* ya fedha shilingi milioni 10; kifungo, miezi sita. Nadhani hizi adhabu zingehuishwa; afadhali ingekuwa inasema labda mwaka mmoja mpaka miaka mitano au muda gani; hii ingetusaidia sana katika kuweza kuweka vizuri hizi taratibu ambazo nafikiri ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niongelee pia kuhusu suala la utafiti. Umefika mahali ambapo Serikali lazima itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia taasisi mbalimbali zitakazotoa mchango katika nchi yetu. Kila mwaka tumekuwa tukiimba kilimo ni uti wa mgongo, sijui uvuvi, sijui nini na nini; bila kutenga fedha za utafiti, tutakuwa tunaimba kila siku, tutakuwa tunapiga kelele bila sababu yoyote. Lazima fedha za kutosha zitengwe na tuweke kama ni kuwekeza. Kufanya utafiti ni kuwekeza na matokeo ya tafiti… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, wajiandae Mheshimiwa Riziki Mngwali, Mheshimiwa Kubenea, Mheshimiwa Lijualikali na Mheshimiwa Silinde.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye amenijalia kusimama hapa siku hii ya leo. Pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii adhimu ili nami niweze kuchangia Muswada wa Sheria ya Kuanzishwa Taasisi ya Kilimo ambayo inaitwa *TARI.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, nashauri kwamba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa pamoja tukubaliane ili tuweze kupitisha sheria hii iweze kuanza kufanya kazi ili watafiti waweze kunufaika na sheria hii.

Lengo la Muswada huu, kwa maana ya sheria hii ni kusimamia tafiti zote za kilimo Tanzania nzima. Kwa kuwa sheria hii ilikuwa haijaundwa, basi ilikuwa inapelekea, watafiti wanapoanzisha utafiti, mwisho wa siku wanashindwa kufika mwisho na utafiti ule ulikuwa hauzai matunda yoyote. Kwa hiyo, ulikuwa haumnufaishi mwananchi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme tu, utafiti uliokuwa ukifanywa ulikuwa siyo mzuri kiasi ambacho kwenye maeneo mbalimbali tumeshuhudia. Kwa mfano, katika Mkoa wetu wa Ruvuma, mbegu ambazo zimeletwa kwa maana ya uzalishaji wa mahindi ni mbegu za ajabu sana. Unashangaa kuona kwamba mhindi unakuwa kufikia futi moja na nusu eti ndiyo unachanua. Sasa huo muhindi unaochanua hivyo ni wazi kwamba unakwenda kubeba kipande cha mhindi kidogo sana. Kwa hiyo, hizi mbegu nyingi ambazo zimekuwa zikiletwa kwetu siyo nzuri, hazifai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nadhani kwa kufanya maboresho na kwa kupitisha sheria hii sasa itakwenda kuhakikisha kwamba tunapata watafiti ambao watakwenda kufanya utafiti mzuri na kuweza kuongeza mapato katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado pia imeonekana kwamba Maafisa Ugani wapo tu jina, hawana kazi yoyote ambayo wanaifanya ya kuweza kuboresha mazao katika maeneo yetu ambayo tunaishi. Wapo wapo tu, wanapokea mishahara lakini kazi zile za msingi sisi hatuzioni. Kwa sababu kama mbegu ya mhindi inaletwa inafikia futi moja halafu inabeba mtoto pale; ni sawa sawa hata sisi akinamama, mwanamke ambaye anaweza akatotoa mtoto mzuri kweli kweli ni yule ambaye angalau anakuwa na urefu kiasi fulani, ingawa hata yule mfupi anaweza akatoa mtoto ambaye anafaa; lakini niseme tu kwamba mbegu ambayo inakuwa imekua kwa maana ya mahindi, ndiyo ambayo inaweza ikabeba mtoto mzuri. *(Minong'ono)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana, sina maana mbaya kwa wale wafupi, ni kwa ajili tu ya kuchambua ili nieleweke kwenye eneo hili la suala la mbegu. Tupo pamoja, naomba Waheshimiwa Wabunge wasinielewe vibaya. *(Makofi/Kelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na Maafisa Ugani, Maafisa Kilimo na wenyewe wapo lakini hizi mbegu zinakuja feki hawasemi chochote, wapo tu wamekaa. Kwa hiyo, suala la utafiti ni muhimu, naomba tupitishe hii sheria ili tuweze kupata mazao mengi na mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme faida ya kuhakikisha kwamba tunapitisha hii sheria, maana yake, uzalishaji utaongezeka. Pia teknolojia mpya dhidi ya kilimo zitagundulika kutokana na utafiti huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Taasisi ya Uvuvi kwa maana ya *TAFIRI.* Hapa kwenye suala la uvuvi utafiti huu utasaidia kuongeza uzalishaji wa viumbe hai kwenye mito, maziwa au bahari. Ni utamaduni ambao umezoeleka, watafiti wetu mara nyingi sana walikuwa wanajikita kwenye bahari na kwenye maziwa, lakini sijaona watafiti wanafanya utafiti wa uzalishaji wa samaki kwenye mito; sijaona watafiti wamejikita kisawasawa kwenye uzalishaji wa samaki kwenye mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watafiti wakijipanga vizuri, zao la uvuvi wa samaki linaweza likatusaidia kwa asilimia kubwa sana kuinua kipato katika nchi yetu. Niseme tu, kule kwetu huwa tunachimba na visima hivi vya maji; lakini unaona kisima wamekichimba kienyeji tu, baada ya miezi mitatu ukienda kusafisha unakuta kambale wamejaa kibao. Hivi hawa kambale, au hawa watafiti wetu hawawezi kuingia huko wakafanya utafiti wa kina wakatengeneza mazingira, hatuwezi kupata samaki wengi jamani? Hatuwezi kuinua kipato! Kwa hiyo, niseme tu huu utafiti na hii sheria tukiipitisha, itakwenda kuwasaidia watu wetu wafanye utafiti wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile mito iliyopo; Tanzania tunasema ni nchi tajiri ambayo ina mito na mabonde. Mito mingine jamani kwa haki ya Mungu imeamua tu sasa ijikaukie tu, kwa sababu hakuna jambo lolote linalofanyika dhidi ya hiyo mito, ipo tu. Zipo nchi ambazo, yaani mtoto anatolewa darasani kupelekwa kwenye mto ili awe kama anatembelea mto aone unafananaje; lakini huku kwetu hatua 20 mto, ukienda kilometa ngapi, mto; lakini ile mito imekaa tu, haifanyiwi utafiti wowote, hakuna kitu chochote ambacho inazalisha, mwisho wa siku inaamua ijikaukie tu. Nao uumbaji wa Mwenyezi Mungu kama huutumii, basi inaamua ijikaukie tu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sheria hii tukiipitisha itaongeza mazao katika suala la uvuvi, lakini pia itaongeza kipato na itaongeza lishe. Pia niseme, mimi sio daktari, lakini utafiti umeonesha kwamba samaki anaongeza afya nzuri sana, lakini pia inasaidia hata ukuaji wa ubongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukilalamika hapa tunasema watoto wengine hawana afya bora, nadhani kama tutaboresha na watafiti wetu wakafanya utafiti wakaona ni samaki wa aina gani, kama tukiwatunza vizuri, tukaona labda katika Nyanda za Juu Kusini kwamba ni samaki wa aina gani wazalishwe; haya, wakaenda labda kwa mfano, kwenye *centre* hii tuliyopo hapa Dodoma ni samaki wa aina gani wazalishwe ili samaki hawa sasa wawe wanazalishwa kila maeneo kwa ajili ya kusaidia lishe, hasa kwa watoto wetu ambao ndiyo tunatarajia kwamba ndiyo zao la watoto wetu wanaoanza sasa waweze kupata samaki wale, ili waanzie hapo sasa kuboresha afya zao na kukuza vizuri kwa ufasaha zaidi ubongo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu tunachokihitaji siyo tu uwezo wa kufaulu darasani, lakini tunataka mtoto mwenye akili ambaye anaweza akafanya utafiti mzuri kwa kutumia ile akili yake. Kwa hiyo, kama ukitaka tu kwa kufaulu, mtu mwingine anaweza akachungulia kwa mwenzake akafaulu. Tunataka watoto ambao kweli wana afya bora kwa kupitia huu uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani pia katika sheria hii iundwe *panel* ili iweze kwenda kusaidia kuwasimamia hao watafiti watakaokuwa wanaenda kufanya utafiti. Badala ya kujifanyia utafiti tu kiholela, ikafika mahali mtu ameshapiga mpunga wake, ameweka mfukoni, hana haja ya kuendelea na utafiti, anasema tu kwamba nimeishia hapo na wala hakuna sheria ambayo atachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme hii *panel* itakayokuwa inasimamia itatazama mwenendo wa wale watafiti, mwisho wa siku kabla hawajamaliza utafiti wao, wanaweza wakafikia nusu na wakaambiwa kwamba kwa utafiti wenu huu, tumeona kwamba hamtoshelezi na…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Riziki, Mheshimiwa Kubenea amejitoa; Mheshimiwa Lijualikali na Mheshimiwa Silinde wajiandae.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba mbingu na ardhi kwa kutujalia afya na uzima. Kisha nakushukuru kwa kunipa fursa nami ya kuchangia Miswada ambayo tunayo mbele yetu. Mengi yamekwishasemwa kwa hiyo, nami nitakuwa na machache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuilinganisha yote miwili nikiwa na uelewa kwamba taasisi hizi mbili ambazo sheria zake tunazitengeneza hapa zina uzito sawa na zinatarajiwa zitendewe haki sawa na Serikali hii. Sasa kwanza zenyewe ukiziangalia zote mbili, Miswada yote miwili, ukiangalia sababu za kuundwa kwake na ukiangalia jina lake, kuna walakini. Kwa hiyo, sitaki kwenda kwenye *details* kwa sababu ya muda, lakini naomba na kumsihi Mheshimiwa Waziri apitie kwa utaratibu kabisa na kwa kina, aangalie pale zinapoelezwa sababu na madhumuni, halafu aangalie na *title*. Kwa kweli nimeona kwa kupitia tu, haziendi sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo liko kote, nimeona suala la maslahi au posho. Sasa kwenye hizi *documents* mbili, moja inazungumzia

posho kwa Wajumbe, lakini nyingine inazungumzia marupurupu. Sasa kwa kile nilichosema mwanzo kwamba tunatarajia ziwe *treated equally,* huwezi ukazungumzia posho halafu mwingine ukasema unampa marupurupu; hayo ni mambo mawili tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye suala hilo hilo la hayo malipo au marupurupu, kwingine kunawekwa Msajili wa Hazina anahusika lakini kwingine inasemwa Waziri tu na Bodi. Sasa nadhani kuna mambo ya kuyapitia tena ili tuweze ku-*harmonise* ili mwisho wa siku tukitoa sheria ziwe kweli sheria zile ambazo tunazitarajia, *unless* Waziri aseme kwamba taasisi hizi hazitarajiwi kuwa na hadhi sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala lingine la ujumla la gharama. Kwenye moja ya *document* hii inaelezea sababu mojawapo ni kuondoa *duplication,* yaani kurudiarudia na vilevile kupunguza gharama. Sasa *the mere fact* kwamba tunaanzisha hizi *independent institutions* kila mahali, hiyo *by itself* ina maana tunaleta gharama na kuna uwezekano mkubwa wa ku-*duplicate* haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia pia wameeleza hayo; wanauliza, kwa mfano, nani anasimamia hizi mwisho wa siku? Kwa sababu ziko nyingi mno. Kwa suala la gharama peke yake, unapoanzisha Bodi, kuna Mwenyekiti, Makamu wake, Wajumbe hao wote wana haki na stahiki mbalimbali; hizo zote ni gharama Waheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mheshimiwa mmoja alizungumza, nafikiri ni Mheshimiwa Jitu kwamba kwenye nchi nyingine za wenzetu, masuala kama haya unayakuta yako *embedded* kwenye *higher learning institutions.* Vyuo vikuu vyetu vyenyewe zinakuwa ni *research based universities; most of them.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii inasaidia siyo tu kujenga *human resource* ambayo ni *skilled* na ina uwezo mkubwa, lakini pia inaimarisha vyuo vyetu kwa sababu vinakuwa vina *research* ambazo zinafanyika kwa muda wote. Wale walimu na ambao wengine wanakuwa *specialized* kama *researcher professors only,* lakini wanakuwa na kazi hiyo ya kufanya ambayo pia inawajengea uwezo wanafunzi wetu. Hii inapunguza gharama kama nilivyosema, lakini pia inajenga uwezo wa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Muswada wa Kilimo. Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wamezungumzia suala la masoko, sasa kwa kuwa huu Muswada wenyewe hauna uhakika sana, ukisoma, kwa sababu hata pale kwenye *item,* kwenye ukurasa huu wa 61 ambapo kunataja maeneo ya utafiti; 61 inaendelea mpaka 62, hata pale kwenye ile *item (8)* ambayo inazungumzia utafiti wa uchumi, jamii na masoko, hakuna masoko pale. Kuna ki-

*item* kimoja tu ndiyo kinazungumzia masoko, lakini mengine yote siyo masoko. Hayo masoko yenyewe, kuna *document* nyingine samahani siwezi kuwa *very specific,* inasema kuimarisha hayo masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sisi kwa mifano tuliyoiona kwenye *TV* wiki iliyopita tu na wiki hii, tunaimarisha masoko au tunatakiwa tutafute masoko? Ikiwa nyanya tu za Moshi na Kilosa pale zinaoza, unaimarisha soko kweli au hatuna hata hilo soko? Kwa hiyo, nadhani tuwe makini tunataka kusema nini hasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kwa uelewa wangu ni *very serious institutions,* kwa hiyo, yale majukumu tunayotarajia yafanywe na hizi taasisi kweli yawe *specific* na ule u-*specific* wake uende kwenye ku-*address the needs* kama alivyosema Mheshimiwa Waitara. *Research* ni lazima ziwe zinajibu yale masuala yaliyopo au zinatatua changamoto na matatizo yaliyopo. Sasa hizi *documents* je, zina-*address* hayo? Haya yaliyoorodheshwa humu kama majukumu ya taasisi hizi, hapo zitakapoanzishwa kama hizi sheria zitapita, je, kweli zitakuwa zinatupa majibu ya yale maswali ambayo sisi kwenye jamii hii yanatugusa kwa sasa hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye huu Muswada wa Uvuvi, nashukuru dada yangu Mheshimiwa Paresso aligusa hilo. Nilipoangalia kwenye *headings* kule kwenye ile *Kiswahili version* nikapata wasiwasi, nikasema huu sasa umekuwa mseto. Hili linaendana na suala ambalo nilishawahi kulisema hapa kwamba Watendaji wetu hawa wanakuwa *overworked most of the time,* ndiyo maana hata hizi *documents* ambazo nilidhani zingekuwa *identical twins* lakini zina tofauti ambazo sidhani kama *they were intended* kuwa na hizo tofauti, lakini inaweza ikawa ni kwa sababu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye suala hili la Muswada wa Uvuvi nilikuwa na swali ambalo Mheshimiwa Waziri ningependa ajibu, anijulishe baadaye kwamba ni vigezo gani vilitumika, kwa mfano, kutaja hivi vituo vinne; kimojawapo kikiwa Dar es Salaam na vingine Mwanza, Kigoma na Kyela?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema hivi Dar es Salaam kunawekwa Kituo cha Uvuvi, *research* kwa ajili ya bahari au kitu gani? Vipi mahali kama Mafia ambapo kuna lukuki ya matatizo yanayohusu uvuvi, hakuna hata ile *thinking* kwamba mahali kama pale panahitajika ule utafiti ukawa karibu zaidi kwa sababu kule kuna mahitaji mengi mahsusi. Kwa hiyo, naona kwamba kuhusu namna gani tunaamua, wapi kikae nini, pia ingekuwa ni suala ambalo tunalipa fikra zaidi ili mwisho wa yote tuwe na kitu ambacho kweli kinakidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zinapotajwa sifa za Wakurugenzi hawa, pale inapokuwa sifa hii au hii, sasa kwa mfano kwenye suala la *fisheries,* mimi sio mzoefu sana, lakini napata tabu kuelewa kwamba mtaalam wa *fisheries*

anaweza akawa sawa tu na yeyote ambaye amesomea viumbe vya majini. Sasa uvuvi na labda viboko na mamba vinaendana vipi? Sisi tunataka mtaalam ambaye amebobea kwenye uvuvi, masuala yanayohusu uvuvi, masoko na kila aina za uvuvi; lakini tunaambiwa hata yule aliyesomea viumbe vingine tu vya kwenye maji anaweza akasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia hapo Mheshimiwa Waziri labda wakati anajumuisha angetupitisha akatueleza hasa ni nini ambacho kinatakiwa hapa? Ni kweli tunataka wataalam ambao ni *very specific and specialized* kwenye hizo *areas* ambapo hizi *research institutes* zitakuwa zinashughulika nazo, au tunataka tu mtu yeyote ambaye angalau ana ujuzi au uelewa wa masuala hayo? Hii nadhani sitarajii kupata suala lile la jumla kama ambalo tulitolewa kwenye ile Miswada iliyopita juzi pale kwamba yoyote tu, hata *chemistry* inaweza kuwa *chemistry* lakini na *biology* pia ikawa ni *chemistry,* kwa hiyo, nilikuwa nimeomba sana Mheshimiwa Waziri atupe hayo majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna makosa madogo madogo tu ya *spelling,* kuna mahali wataalam wanaitwa wataaluma au vitu kama hivyo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Lijualikali, halafu Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Ulega wajiandae.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia nachukua nafasi hii kwa kuwa ni mara ya pili kuzungumza, lakini mara ya kwanza tangu baada ya kuwa nimeshinda kesi ya uchaguzi, pamoja na kwamba mapolisi walijaa Ifakara kwa kila aina ya dhana zote za kijeshi, lakini nashukuru kwamba Mahakama imetenda haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia Muswada huu unaoanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nikiwa natambua msimamo wa Serikali ya Awamu ya Tano kwenye uanzishaji wa viwanda. Nachangia Muswada huu nikiwa natambua ni Watanzania takribani asilimia 73 wataathiriwa na Muswada huu ambao ni wakulima wa mazao mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma sheria inayoanzisha, hasa pale inapozungumza Mkurugenzi atapatikana vipi; Mkurugenzi atapatikana kwa Rais kuteua. Sisi tumekuwa tukisema sana kwamba mamlaka hii ambayo tunaitoa kwa Rais ya kuteua Wakurugenzi, kuteua viongozi wa taasisi mbalimbali za Serikali, ni madaraka makubwa sana. Kwa kuzingatia asilimia 73 ya Watanzania watakaokwenda kuathirika; kwa kuzingatia msimamo wa Serikali ya Awamu ya

Tano ya ujenzi wa viwanda, napata mashaka; tena na katika Muswada huu Rais wetu anapewa mamlaka mengine makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Muswada ni wa kitaalam, *it's pure research, pure academic* na tumeona miaka hii ya sasa hivi zile *posts* ambazo ni za kitaalam wakipewa watu ambazo wana kadi za CCM. Hii tumeiona!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianzia kwenye uteuzi; uteuzi ulikuwa ni Wakurugenzi wa Halmashauri mbalimbali na juzi ameteuliwa mtu mmoja hapa Manispaa ya Dodoma kuwa Mkurugenzi wa Jiji ambaye kwa sababu tu ana kadi ya CCM, sheria inasema kabisa uteuzi uzingatie vigezo vifuatavyo; na hapa tumeweka vigezo, tumeweka… *(Kicheko/Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitashangaa sana…

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Lijualikali, kaa chini.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda nimpe taarifa mdogo wangu Mheshimiwa Lijualikali kwamba aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Dodoma ana *Masters* ya Sheria na hajachaguliwa kwa sababu ya kuwa na kadi ya CCM; na watu wote wanaoteuliwa sasa hivi wanaangaliwa sifa zao na siyo kadi za Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lijualikali, ningependa kuwasihi, mnapochangia humu ndani mchangie taarifa au chochote ambacho kina uhakika na ni cha ukweli. Siyo jambo sahihi kuzungumza vitu, kuwa-*defame* watu ambao hawapo humu ndani. Hilo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni zetu vilevile zinatoa haki kwa huyo unayemsema kuleta malalamiko Bungeni; huo ndiyo ukweli. Sasa msianze kulalamika ovyo ovyo. Hakuna haja ya kusema, ninyi kaeni kimya. *Referee* akipiga filimbi, ndiyo kashapiga. Hata mpirani pale *referee* akipiga filimbi, timu moja lazima italalamika. Ndiyo nyie mnalalamika ovyo ovyo tu hapa.

Mheshimiwa Lijualikali, endelea.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii taarifa siipokei. Nilichokisema kimo kwenye Muswada. Nazungumzia sifa za wanaoteuliwa. Ukisoma mwongozo wa kumchangua *DAS* anatakiwa kuwa mtu ambaye amefanya kazi kwenye Utumishi wa Umma miaka siyo chini ya 10. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lijualikali, jikite kwenye hoja ambayo iko mbele yako. *(Kelele)*

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye hoja, nazungumzia sifa za wanaoteuliwa. Nimesema huu Muswada unakwenda kuathiri asilimia 73 ya Watanzania, siyo kitu kidogo, lazima vitu hivi vifuate taratibu. Leo hapa tupo kwenye sheria, lakini kuna maamuzi mengine yanafanyika hayafuati sheria; na huu ni ukweli uko wazi. Kwa hiyo, naomba sasa tutunge sheria hii, kile ambacho kinapita hapa ndiyo kifanyiwe kazi, lakini siyo utafute kadi za watu, kwa sababu ya kadi ndiyo achaguliwe kuwa Mkurugenzi. *(Makofi/Kelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme jambo lingine. Kule kwangu Ifakara kuna Kituo cha *KATRIN,* ni kituo cha utafiti. Kituo hiki kinafanya tafiti ya mambo ya mpunga na nini, lakini ni kama vile kimekufa. Hakina nguvu, hakina fedha, hakifanyi kazi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani labda kwa sheria hii jinsi ilivyo, inaweza kusaidia na ndiyo maana nasema kwamba hii sheria inakwenda kuathiri watu wengi. Kwa hiyo, tunapoongea haya mambo, siyo kwa sababu ya mtu kumsema, tunasema kwa sababu haya mambo yanakwenda kuathiri Watanzania wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme jambo lingine kwamba sheria inasema taasisi hii itakuwa na uwezo wa kushtaki na kushtakiwa. Pia inasema Taasisi hii itakuwa na uwezo wa kumiliki mali za kila Taasisi, kila kituo ambacho kilikuwa kinafanya tafiti; lakini sheria inasema kwamba hakuna mtu atakayetakiwa kushiaki ikiwa hajapeleka *notice* ya siku 90 kwenda kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Asipofanya hivyo, maana yake ni kwamba anakosa haki ya kwenda kushtaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele hiki kinawanyima Watanzania wengi watakaokwenda kudhulumiwa haki zao na ukizingatia sasa hivi kuna migogoro mingi ya ardhi. Kwa mfano, kule kwangu Ifakara, Kituo hiki cha *KATRIN* kina migogoro mingi sana ya ardhi. Leo ukimwambia Mtanzania asiishtaki *KATRIN,* ashtaki taasisi kwa kutoa *notice* ya siku 90, maana yake ni kwenda kumdhulumu Mtanzania huyu asiweze kupata haki yake kisheria na ya Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria hii, huku mbele kwenye mambo ambayo yanahusu utafiti, inasema kwamba kutakuwa na tafiti wa kutafuta masoko. Ningekuwa mimi ndiyo Waziri wa Kilimo, leo ningejiuzulu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani miaka 50 wakulima wa Dumila wanalima, nyanya zinaoza na Serikali ipo. Haiwezekani Serikali inayosema Hapa Kazi Tu, Watanzania wanalima nyanya, wanatumia nguvu zao, wanatumia fedha zao, wanatumia akili yao, wanatumia kila kitu na Serikali hamtoi hata senti 10, wanapata mazao halafu eti baadaye soko hakuna, ng'ombe wanakula, Waziri wa Kilimo yuko hapa amekaa analipwa mshahara! Ni Taifa la Tanzania ndipo unaweza ukaona hali kama hii. Hiyo hapa kazi tu iko wapi? Kama Wakulima wanatumia nguvu zao, wanatumia fedha zao, wanalima, wanajitoa halafu soko hakuna; Serikali imekaa, sijaona tamko hata la Waziri! Sijaona Waziri akisema ni kwa nini na amechukua hatua gani kunusuru watu wa Dumila waweze kupata haki yao, waweze kupata soko? Serikali imekaa, hamna tamko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, ukiangalia dunia ya leo, huu Muswada nilitegemea ungetoa majibu ya namna gani wananchi wanakwenda ku-*access information*. Nilitegemea sheria itasema tutakuwa na *integrated system* ambayo inafanya kila mtu aweze ku-*access*. Yaani *SUA* wakifanya *research* kuhusu kilimo, sehemu nyingine wakifanya *research* kuwe na *system* inayopokea taarifa zote hizi ili mtu leo akiamua kufanya *research* sehemu yoyote anaingia kwenye hiyo *system,* kwenye hiyo *database* ana-*access information.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo *SUA* wanafanya yao huko, leo tena tunakaa hapa Wabunge, hii sheria inapitishwa hawa watafanya huko, hawa watafanya kule; dunia ya leo ambapo *information is power,* sioni kwenye huu Muswada. Ni kama vile tuko miaka 60 nyuma. Yaani hii *system* ya nchi haiko *intergrated,* kila mtu na sehemu yake anafanya kazi yake peke yake. Hawa wanafanya vitu huku, hawa wanafanya huku, *where is technology* kwenye hii nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme kazi ambayo iko tu hapa, watu wakisikia UKUTA, basi vurugu; Mapolisi mtaani, lakini kazi ambayo ni *tangible* ambazo unaziona kabisa za kutumia akili; hatuwezi kuwa na nchi ambayo, yaani kitu kidogo kama hiki anakuja mtaalam na Muswada anashindwa kusema kwamba *research which is pure academic;* tunashindwa kuwa na *system* ambayo watu wanaweza ku-*access information* vizuri na tukafanya *research* zetu vizuri kwa maendeleo ya kilimo na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo tu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa Waheshimiwa namwita Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Ulega ajiandae.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili nami nichangie Miswada miwili iliyoko mbele yetu. Miswada iliyoko mbele yetu ni Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Utafiti wa Kilimo wa mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizi mbili ambazo ziko mbele yetu zimesainiwa na watu wale wale. Utaona hapa kuna Balozi Kijazi pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo wa wakati ule, Mheshimiwa Mwigulu; sheria zote mbili wamesaini watu hao na mwezi uliosainiwa hizi sheria ni mwezi wa Tano. Sheria hizi ukizipitia hapa mbele baada ya Muswada wa Sheria, wanasema; moja, "imetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," Hiyo ni Sheria ya Kilimo na ukija kwenye Sheria ya Uvuvi na yenyewe imetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia kwenye Sheria ya Uvuvi, Kifungu cha (2) kinachozungumzia matumizi ya sheria, kinasema: "sheria hii itatumika Tanzania Bara tu." Wakati ukija kwenye hii Sheria ya Kilimo, hii inatumika kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hapa nafikiri unajaribu kuona *concept* ambayo najaribu kuizungumza hapa. Sheria mbili zimezungumzwa na watu wale wale kwa nyakati zile zile zinazofanana. Zinaigawanya Tanzania kibaguzi kwenye makundi mawili. Swali hili kwa mfano, Sheria ya Uvuvi, Zanzibar peke yake ndiyo imezungukwa zaidi na maji, yaani Kazanzibar kenyewe kamemezwa na maji na shughuli yao moja kubwa ni uvuvi, lakini hapa tunazungumzia suala la Tanzania Bara peke yake, kwa maana nyepesi, Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya ndiyo maswali ambayo kila siku tunasema. Humu ndani tuko kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunahitaji majibu yanayohusu Muungano, yaani kwa maana ya Zanzibar pamoja na Tanganyika. Sasa kama ni hivyo, ndiyo tunakuja na ile hoja yetu ya kila siku kwamba hapa hoja ya Serikali tatu haiepukiki kutokana na mwenendo wa sheria tunazotunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kwenye hii sheria itabidi hii Sheria ya Kilimo, huo upande wa Kiswahili huo, jina hili la Sheria, juu mmekosea kote, kuanzia ukurasa wa 34 mpaka ukurasa wa mwisho wa 63, huku juu mmeandika Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi. Hii *header,* huku juu kote.

Sasa hii inaonyesha *unseriousness,* yaani vitu vidogo kama hivi. Unajua watu wanapimwa uwezo wa kufanya mambo kwa vitu vidogo vidogo. Miezi minne unakosea mambo kama haya, mwisho wa siku utakosea; ndiyo maana

nchi inaingia kwenye mikataba ambayo kila siku ina matatizo. Mambo madogo madogo kama haya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nina swali la kujiuliza la jumla; tatizo la nchi hii ni sheria? Maana kila siku tunatengeneza sheria kama ndiyo *solution* ya matatizo yetu, maana yake hilo ndilo swali Mheshimiwa Waziri utuulize. Maana yake ukiangalia tumekuwa na *institute* kwa miaka yote; na hizi taasisi za kufanya utafiti zimekuwa zikifanya tafiti mbalimbali na zile tafiti hazifanyiwi kazi. Kwa hiyo tatizo lililoko hapa, siyo sheria, ni mtu anayeweza kuratibu hizi tafiti kufanya kazi zake na hizi tafiti zikatekelezwa. Hilo ndiyo tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia, Wizara ingekuwa na utaratibu mzuri wa ku-*coordinate* hizi taasisi, leo hata hii sheria tusingekuwa tunaijadili. Wala tukisema kwamba sheria itakuja kutusaidia, siamini kwamba sheria ndiyo inaweza kutoa *solution* ya matatizo ya kilimo katika nchi yetu. Siamini kitu kama hicho! Ninachoamini ni utayari ambao sisi kama viongozi tukiwa nao ndiyo utakaopelekea *solution* ya tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapozungumzia tafiti za kilimo, maana yake ni nini? Maana yake tunatafsiri kwamba, kilimo kinachohitajika ni kwamba ziletwe mbegu bora, wananchi wazalishe wapate mazao mengi. Leo bila hata hizo tafiti, bado Watanzania wanazalisha sana na inafikia mahali Serikali inashindwa kununua mazao ya wakulima wa kawaida. Kwa hiyo, hapo huwezi kutueleza kwamba tatizo ni sheria, ndiyo Watanzania wanakosa soko; tatizo ni sheria, ndiyo Watanzania wanakosa mbolea; tatizo ni sheria, ndiyo Watanzania wanashindwa kutabiri hata hali ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unakuja kugundua kabisa kwamba tutaendelea kutengeneza sheria kila siku kupata utaratibu, lakini hatutapata majibu sahihi kama tutashindwa kuwa tayari kulitumikia hili Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitaendelea kusisitiza juu ya hili, kwamba uratibu wa shughuli zote, lazima pawepo sasa na *commitment* ambayo tunaweza kutekeleza majukumu haya ambayo tumeyapangia. Ila jukumu la kisheria lipo tu ambalo nina uhakika ukipata watu ovyo kabisa, hawataweza kutekeleza na tutarudi hapa tutatengeneza sheria nyingine ambayo ita-*supersede* sheria ambayo sasa hivi tumeipitisha. Kwa hiyo, hilo linatakiwa lifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria imeeleza hapa, *financing*; tatizo la hizi tafiti zetu, moja, ni *financing. Financing* kwa maana ya kupata fedha kwa ajili ya kuwasaidia watu wafanye tafiti, lakini pili, hizo hizo fedha kutekeleza zile tafiti ambazo zimetekelezwa, yaani ambazo zimefanyiwa kazi.

Kwa hiyo, hayo ndiyo matatizo makubwa. Sasa hapo unasema, Waziri atatoa kibali; kwa mfano, kuna sheria moja nimeipitia hapa, inasema Waziri ataidhinisha fedha ambazo hata kama hazipo kwenye matumizi ya mwaka wa fedha uliopita, zitaidhinishwa baada ya maandishi ya Mheshimiwa Waziri. Sasa pale unakuja kugundua Waziri anaweza akapitisha tu mwanya wake wa fedha kwa sababu tu hazipo katika mwaka ule wa fedha. Yaani ipo ndani ya sheria ambayo imeandikwa humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachotakiwa tukizungumze sisi sote, tafiti lengo lake ni nini? Maana yake kuna tafiti zinazojulikana na kuna tafiti ambazo hazijulikani na kuna tafiti ambazo tayari katika Taifa letu tulitakiwa tupewe majibu; kuna tafiti zimefanyika ambazo mpaka sasa hivi hatujaelezwa zimeleta majibu gani tofauti. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, ni kengele ya pili. Tunaingia sasa na Mheshimiwa Ulega, msemaji wetu wa mwisho. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa fursa hii. Nami moja kwa moja naomba nijielekeze kwanza kwa kuwapa pole wenzetu wa kule Bukoba kwa maafa yaliyotokea ya tetemeko la ardhi na Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi wale wote waliotangulia mbele ya haki, lakini awaponye kwa haraka zaidi wale wote ambao hivi sasa wamekuwa wakiugua maumivu mahospitalini na adha mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue fursa hii pia vile vile kuipongeza sana Serikali yetu kwa kuleta sheria hii inayohusu Taasisi zetu za Utafiti wa Kilimo na Taasisi ya Utafiti Uvuvi. Imekuja wakati muafaka katika kuwasaidia watafiti wetu kuhakikisha kwamba wanaifanya kazi yao vizuri kwa maendeleo ya Taifa letu na kwa maendeleo ya dunia yetu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo *angle* mbili, tatu ambazo ningependa nizizungumzie katika sheria hizi. Nitayazungumza mambo yote mawili kwa pamoja yanayohusu uvuvi lakini pia vile vile nitayazungumza mambo yanayohusu kilimo. Kabla sijakwenda katika kuzungumzia uvuvi na kilimo, nataka nitoe ombi hasa kwa wenzangu, maana unasikia hapa, watu wanajadili Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, mwingine anaanza kuzungumzia mambo ya Polisi na UKUTA, anaacha kuzungumzia masuala yanayohusu utafiti wa uvuvi kwa kuwa hana jambo anaenda kuzungumzia jambo linalohusu nyanya zake kule Kilombero zimepondeka. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni wakati muafaka watu kama hawa, rafiki yangu Mheshimiwa Lijualikali, jamani mtusaidie tupate elimu ya kujua hivi vitu vya kwenda kujadili. Hili jambo linahusu utafiti! Bahati njema sana katika sayansi hakuna *blah blah!* Sayansi inazungumzia *facts!* Sasa mimi nataka nitoe elimu inayohusu *facts* na siyo *blah blah! (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ulega! *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Naam! Ndiyo! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ulega hebu kaa kwanza. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri ni jambo muhimu kuvumiliana na ukijua kupiga, ujue kukinga. Tatizo lenu hamjui kukinga, mnaleta mikwara humu ndani. Nawaombeni, tumebakiwa dakika tano tu kumaliza Bunge. Nawambeni sana, ushabiki wa kufanya fujo ndani ya Bunge hauruhusiwi kikanuni. *Rulling* yangu ndiyo hiyo. Hakuna kumpongeza mtu, mpaka naahirisha Bunge hapa. Endelea Mheshimiwa Ulega. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikia Yalaah, ujue imempata huyo! Ehee! Kwa hiyo, usishituke, imewapata hiyo! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuishauri Serikali juu ya suala hili linalohusu utafiti, kwanza, tuhakikishe kwamba *COSTECH* ndiyo inayopelekewa pesa na baadaye taasisi zetu zinakwenda kushindania pesa kule *COSTECH.* Jambo lililokuwa la msingi hapa ni kuhakikisha kwamba *COSTECH* wanaweka vipaumbele sawa na watu wote wanavyohitaji, maana Taasisi ziko nyingi. Inawezekana kwamba Taasisi nyingine zisipate pesa hizo kutoka *COSTECH.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo la msingi hapa ni kuhakikisha kwamba ili kila taasisi iweze kupata zile pesa, wakati mwingine taasisi zetu za uvuvi na kilimo hazipati kabisa hizo pesa, kwa sababu *COSTECH* inakuwa kwamba, hawa watu wa uvuvi na kilimo labda hawakuingia katika ushindani wa zile pesa ambazo zinagombaniwa kule *COSTECH.* Kwa hiyo, ni jambo la msingi kwamba *COSTECH* wajitahidi kuweka utaratibu ambao utasaidia taasisi zetu zote zihakikishe zinanufaika na pesa hizi za walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu sana, taasisi zetu zimekuwa zinategemea pesa za wafadhili, ambapo maana yake ni nini? Ni kwamba *Donor* anayeleta pesa zile, analeta kufuatana na kile anachokitaka yeye. Anayelipia zumari, ndiye anayechagua nyimbo. Sasa ni jambo la msingi kuhakikisha tunaongeza nguvu kule *COSTECH* na kuipa utaratibu mzuri ili taasisi zetu hizi tunazozitungia sheria leo ziweze kunufaika na pesa za Watanzania badala ya kutegemea zile pesa za *Donors* tu peke yake. Tukitegemea pesa za

*Donors* peke yake, matokeo yake ni kwamba tafiti nyingi hazitafanyika na hivyo matatizo mengi yanayotokana na kutokufanyika kwa tafiti yatajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulisema hilo, nataka nizungumzie jambo la vifaa vya uvuvi. Kwa kipindi kirefu sana tumeona kwamba yanatokea matatizo mengi katika maziwa na bahari kwa ajili ya vifaa vya uvuvi, lakini sheria haijataja juu ya kutafiti ni vifaa gani hasa vilivyokuwa bora. Tunafahamu kwamba wakati wote imekuwa ikizungumzwa *size* ya nyavu kwamba *size* hii ndiyo inayofaa zaidi, lakini tungefurahi kuona kwamba sheria inataja na hivi vifaa vya uvuvi viweze kufanyiwa utafiti ili viendane na hali halisi ya kimazingira na wakati vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumza ni *database*. Tumefanya tafiti nyingi sana, nami nawashangaa wale ambao wanasema kwamba tunatunga sheria hizi za tafiti hazitusaidii kitu. Leo nataka nikuhakikishie, bila hizi tafiti hata hii jeuri ya kusema kwamba hakuna kilichofanyika na hazina faida hizi tafiti, watu wasingekuwa nayo. Hata hivyo wanasayansi tunafahamu kwamba hizi tafiti ni muhimu na hii sheria bado ni muhimu, cha msingi ni kuhakikisha tunakuwa na *database* ya tafiti zetu zote tulizozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi tafiti kama hazikutusaidia leo, zitasaidia vizazi vyetu; ndiyo maana ya elimu! Elimu haishii kwamba itatusaidia leo. Watoto wetu kule mbele watakapokuwa wanakwenda kusoma, wataona kwamba sisi huko nyuma tuliwahi kufanya utafiti wa jambo kadha wa kadha na limewekwa mle katika *archives* au vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nililokuwa nataka nilizungumze la kuishauri Serikali, najua lipo katika mipango yetu, lakini mipango iliyopo ni ya kiuchumi juu ya bandari ya uvuvi. Uwepo wa bandari ya uvuvi utasaidia pia watafiti wetu. Unapokuwa na bandari ya uvuvi maana yake ni kwamba watafiti wetu wanapokwenda kufanya shughuli zao za utafiti wanapata mahali pa kuweza kutia nanga na hatimaye kutoa *results* za utafiti wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nashauri sheria itaje juu ya muda wa ufanyikaji wa tafiti. Wadau wanalalamika sana; wapo watu wanapewa nafasi ya kufanya utafiti kwa miaka tisa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha, waliobakia katika orodha yetu watakuwa *sorted in* kesho asubuhi.

Naomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa kesho Alhamisi tarehe 15 kutakuwa na Semina kwa Wabunge wote kuhusu mambo yafuatayo:

Dhana ya Bima ya Afya na Utaratibu wa Upatikanaji wa Huduma za Matibabu kwa Wabunge; na Uhamasishaji wa Mkakati wa Ugharamiaji wa Huduma za Afya kwa Wabunge. Semina hii itafanyika ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa 7.00 mchana. Wabunge wote wanaombwa kuhudhuria. Imeletwa na Utawala, Bunge.

Usafiri wa Treni *special* kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge siku ya Jumamosi kwenda Dar es Salaam. Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote watakaopenda kusafiri kwa Treni ya *TRL; TRL* imeandaa Treni *special* siku ya Jumamosi kuelekea Dar es Salaam kama ilivyofanyika wakati wa Bunge la Bajeti. Mheshimiwa Waziri Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, atakuwemo kwenye safari hiyo.

Nawashukuru Wabunge wote kwa kazi tuliyoifanya leo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku, Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 15 Septemba, 2016 Saa Tatu Asubuhi)*